# Nipashe

Alhamisi Novemba 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580087

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

rdian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Vifurushi vipya bima ya afya vyazua jambo, waziri atetea

UKURASA 3




UKURASA 13

# Membe awekwa tena kikaangoni

• **CCM** yamtaka afuate taratibu vinginevyo... Nape, January Makamba wawekwa mtegoni...*Ukurasa 2*



DK. Bashiru Alli



Benard Membe

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### IGP AAGIZA ADHABU WANAUME WAKATILI



MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali Simon Sirro, amewaagiza askari kuwashughulikia wanaume...

## Serikali yashusha bei ya nyumba za PSSSF

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Rais Magufuli aombwa kurejesha pesa mitaani



UKURASA 2


**MICHEZO** YANGA, ALLIANCE WATAMBIANA UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# CCM yamvaa tena Membe

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimemwibukia mwanachama wake, Bernard Membe, na kumtaka kufuata na kutii katiba, kanuni za chama kwa kuwa wakati wowote hatua kali zitachukuliwa dhidi yake na yeyote atakayekwenda kinyume.

Sambamba na Membe, CCM imewakemea wanachama wote waliosamehewa na Mwenyekiti wa Taifa, Rais John Magufuli, na kuwataka kuomba msamaha ndani ya chama kwa kuwa msamaha waliopata ni wa Rais kama Mtanzania na nafasi yake na si chama.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema hayo wakati akihojiwa kwenye kipindi cha Konani cha ITV kinachorushwa mtandaoni, alipoulizwa kuhusiana na agizo lake la kumwita Membe na kutotii baada ya kujibu kuwa haitwi kupitia mikutano au vyombo vya habari.

Alisema hawajawahi kumjadili Membe kwenye vikao na alivyoitwa hakuwahi kufika na kwamba kosa halifi bali linaishi kama jinai bali kilichobakia ni utaratibu wa wakati.

"WanaCCM wajue tuko makini kulinda katiba na utamaduni wa chama na wanachama kutii viapo vyao, kuamini kwamba binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja, kusema kweli daima na kujielimisha," alisema.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, mwanachama yeyote atakayevunja hayo kwa tabia, kauli na vitendo, atakuwa amekosa sifa na kwamba ataitwa kwenye vikao na kujadiliwa, kujitetea na uamuzi

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua mradi wa nyumba za NSSF, zilizopo Tuangoma katika Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OWM**

# JPM aombwa aachie fedha mitaani

**Beatrice Moses na Elizabeth Zaya**

MJASIRIAMALI Abel Mpinga, mkazi wa Igunga mkoani Tabora, amemwomba Rais John Magufuli aachie fedha, akidai hali ni mbaya mitaani.

Amedai wajasiriamali wananyang'anywa friji na viambaza (Tv) kutokana na kushindwa kulipa mikopo.

Mpinga alitoa ombi hilo jana baada ya kupewa nafasi na Rais Magufuli aliyekuwa safarini kuelekea Shinyanga.

"Kama itakupendeza, watu wana hali mbaya, kinamama wananyang'wa TV, friji kwa ajili ya mikopo midogo midogo, hali imekuwa ngumu, tunakuomba mheshimiwa uachie fedha.

"Mengine yote hatuna tatizo na wewe, yakikamilika haya, mzee hata ukitawala milele, hakuna shida," Mpinga alisema huku sauti za kushangilia zikisikika kutoka kwa baadhi ya wananchi waliokuwa eneo hilo.

Mpinga pia alimpongeza Rais Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya nchini, akiomba kasi iongezwe katika mradi wa maji ya Ziwa Victoria ili kutatua kero ya maji mkoani Tabora.

Katika majibu yake, Rais Magufuli aliwataka wananchi wafanye kazi kwa bidii, akieleza kuwa ndiyo suluhisho la kutoonekana kwa fedha mitaani.

"Ukitaka hela, wewe fanya kazi, wewe uliyekaa kijiweni unapiga kelele hela hela, cha bure hakipo, lazima niwaeleze ukweli, hata mimi sina, kinachotakiwa ni kuchapa kazi.

Hata maandiko yanasema "asiyefanya kazi na asile," alisema Rais Magufuli.

Alisema wapo wananchi ambao wamekuwa wakijituma kufanya kazi, zikiwamo za kuchimba mifereji ya barabara, wana uhakika wa kupata fedha.

"Kalime, vya bure vimeisha na vitaisha zaidi, ukitaka fedha, nenda hata kwenye madini, mimi sikuja kuleta hela, nimekuja kuwaambia Watanzania wafanye kazi," alisema.

Rais Magufuli alisema serikali inatafuta fedha kwa ajili ya barabara, umeme, hospitali na madaraja, hivyo haiwezi kutafuta fedha kwa ajili ya mtu binafsi na familia yake.

"Tufanye kazi, njia pekee ya kuleta fedha ni kufanya kazi, hata Ulaya wanafanya kazi, wapo wenye shida kuliko huku, ukitaka kutengeneza maisha yako, ni kuchapa kazi," alisema.

**AONYA WATENDAJI**

Akiwa Masumbwe wilayani Mbogwe, Rais Magufuli aliwaonywa viongozi wa eneo hilo kwa kushindwa kutumia fedha za ruzuku ya barabara zaidi za Sh. bilioni nne kwa miaka minne mfululizo.

Alisema tangu aahidi kutengeneza barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kupeleka fedha hizo, hakuna kazi iliyofanyika.

"Mlichaguliwa na wananchi, mkatetee wananchi na siyo kwenda kuchukua posho tu, hawa watendaji wanawachezea, huko wanakotoka kuna barabara za lami, nataka barabara za lami hapa, sitamwachia wala kumsamehe mtu yeyote.

"Niliahidi tangu 2015, lakini hakuna hata barabara moja, na ninyi mtakuwa hakuna siku nitakapoamua, DC (Mkuu wa Wilaya) kasimamie hili na pia wewe mkurugenzi badilika, ninakueleza 'this is last worning' (onyo la mwisho), na wewe mbunge badilika, acha upadri," alisema Rais.

# IGP aagiza adhabu wanaume wakatili

**Na Mwandishi Wetu,** SERENGETI

MKUU wa Jeshi la Polisi Nchini, (IGP) Simon Sirro, amewaagiza askari kuwashughulikia wanaume wanaobainika kuwafanyia ukatili wa kijinsia wanawake na watoto.

Alitoa agizo hilo wakati akizindua Kituo cha Polisi cha Dawati la Kijinsia na Watoto, Kituo cha Polisi Mugumu, kilichofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (Unfpa), kilichojengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 70 chini ya usimamizi wa Shirika la Jukwaa la Utu wa mtoto (CDF).

Alisema serikali haitavumilia watu wanaoendesha vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto na watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

"Naagiza kuanzia sasa askari mkimkamata mtu amemfanyia ukatili mke wake, au amekataa kumsomesha mtoto wake tumieni nguvu za kadri maana sheria inaruhusu," alisema.

IGP Sirro alisema, kwa mwaka 2018 matukio ya ukatili wa mama na mtoto yaliyoripotiwa yalikuwa 43,480, lakini kwa mwaka huu wameishapokea matukio 41,416 hali ambayo inaonyesha watu wamepata elimu na kupungua.

"Wanaume wa Mkoa wa Mara wanatawaliwa na mfumo dume, wanachukulia watoto wa kike kama sehemu ya kutajirikia, acheni tabia ya kudai mahari kubwa inakuwa kama mnawauza na kuwadhalilisha, tutawashughulikia," alisisitiza.

Mkurugenzi mtendaji wa Jukwa la utu wa mtoto, Koshuma Mtengeti, alisema ukatili dhidi ya wanawake na watoto unatokea katika mazingira ya aina zote nyumbani, shuleni, kwenye jamii na mitandao ya kijamii.

"Jambo la kusikitisha zaidi watuhumiwa wa ukatili walio wengi ni wale ambao waathirika wa ukatili wanashirikiana nao kwa karibu na kuwaamini sana, tafiti zinaonyesha mara nyingi ni mtu wa karibu wa familia ambaye anaweza kuwa mjomba, kaka, shangazi, watumishi wa ndani, baba au mama," alisema.

Alisema ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaligharimu taifa katika nyanja za kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kuwa ukatili wa kijinsia huathiri afya, elimu na uhusiano wa waathirika wa ukatili na jamii.

Pia husababisha ongezeko la watoto wanaoishi mitaani kwa kukimbia vipigo nyumbani na hatimaye tabia mbaya zilizo kinyume na maadili kama vile ujambazi, matumizi ya dawa za kulevya na ukahaba.

Koshuma alisema kazi nyingine walizokwisha fanya ni kutoa mafunzo kwa polisi wa dawati la jinsia na watoto zaidi ya 241 jinsi ya kushughulikia upelelezi na kutunza vielelezo kwa ufadhili wa Unfpa.

Mwakilishi Mkazi wa Unfpa, Jacqueline Mahon, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia na mauaji ya vikongwe vinazidi kushamiri kwa jamii.

"Wanawake, wasichana na watoto wanapitia ukatili wa aina mbalimbali ikiwamo ubakaji, ulawiti, vipigo, mauaji ya vikongwe, shambulio ukeketaji, ndoa za utotoni, mimba za utotoni, pamoja na wanafunzi kuzoroteshwa kimasomo,"alisema.

Alitoa wito kwa wakazi wa Wilaya ya Serengeti kutumia dawati hilo ili kutokomeza vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa kwenye kituo cha dawati la jinsia na watoto iwapo wataona jamaa, rafiki, au jirani anafanyiwa ukatili wa kijinsia.

Jumla ya ofisi nne za madawati ya polisi zinatarajiwa kufunguliwa na IGP mkoani Mara.

# Serikali yashusha bei nyumba mradi PSSSF

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeshusha bei za nyumba za miradi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) nchi nzima kwa karibu asilimia 50 baada ya kubaini zinauzwa kwa gharama kubwa na Watanzania kushindwa kumudu kuzinunua.

Nyumba za vyumba viwili vya kawaida zilizokuwa zinauzwa kwa Sh. milioni 66 zimeshushwa hadi Sh. milioni 36.58.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Bunge, Sera, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aitangaza uamuzi huo jana alipohitimisha kutembelea miradi ya PSSSF.

Mradi huo wenye nyumba za gharama nafuu katika eneo la Buyuni, Chanika una nyumba 480 kati ya hizo 204 hazijapata wanunuzi na 276 malipo yake hayajakamilika.

Mhagama alisema mdororo wa ununuzi wa nyumba hizo umesababishwa na makato ya urejeshwaji ya kila mwezi kuwa juu na watumishi wengi kutokumudu bei za nyumba hizo.

Kadhalika alisema lengo la kujenga nyumba hizo ni kuwauzia watumishi na Watanzania kwa bei nafuu na badala ya kukaa nazo.

Alisema menejimenti ya mfuko iliridhia kutumia Mtathmini Mkuu wa Serikali ili kupata tathmini na thamani halisi ya nyumba hizo kuwa bei halisi na soko lililopo.

"Hii nyumba tunaishusha nusu bei na ndio bei ya soko hizi gharama zilikuwa zinawaumiza wananchi na nia ya serikali yetu ni kuwasaidia wananchi wake," alisema Mhagama.

Pia, nyumba 169 zenye vyumba vitatu vya kawaida zilizokuwa zinauzwa kwa Sh. million 67.26, Mthamini Mkuu wa Serikali amesema zinaweza kuuzwa kwa Sh. milioni 35 pamoja na kodi ya Sh. 6,300,000, zitauzwa kwa Sh. milioni 41.3.

"Nyumba 146 zenye vyumba vitatu, viwili vya kawaida na master bedroom zilizokuwa zinauzwa Sh. milioni 74.34 zitauzwa hadi Sh. milioni 39 pamoja na ya Sh. 7,020,000 sasa zitauzwa Sh. milioni 46.02," alisema huku wananchi wakimshagilia.

Waziri Mhagama alisema nyumba yenye vyumba vitatu na master bedroom iliyokuwa inauzwa Sh. milioni 83.78 sasa itanunuliwa kwa Sh. milioni 52 pamoja na kodi ya Sh. 9,360,000 itauzwa kwa Sh. milioni 61.36.

Ameilekeza menejimenti kutekeleza agizo hilo na nyumba zote ambazo hazijanunuliwa ziuzwe kwa bei aliyoisema kwa niaba ya serikali.

"Hizi nyumba watu walikuwa wanashindwa kuzinunua kutokana na gharama kuwa kubwa, natoa mwezi mmoja watu wajipange kuchukua nyumba hizo na soko langu silifungi watu binafsi ambao wanataka waje," alisema.

Vile vile, amewaonya baadhi ya wafanyakazi ambao badala ya kukaa katika nyumba hizo wanageuka kuwa

INAENDELEA UK. 8



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge , Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama (katikati), akitembelea nyumba za PSSSF, zilizopo Buyuni, Chanika, wilayani Ilala, mkoa wa Dar es Salaam juzi, kabla ya kutangaza punguzo la bei kwa nyumba hizo. Kushoto ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Andrew Massawe na (kulia) ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PSSSF, Dk. Aggrey Mlimuka. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Vifurushi vipya bima ya afya vyazua jambo

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unatarajia kuzindua vifurushi vipya vitatu vya bima ya afya vinavyoonyesha gharama ya matibabu kulingana na umri na makundi, baadhi ya wadau wamekosoa utaratibu huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa shirika lisilo la kiserikali la Sikika, lililojishusisha na utetezi wa utawala bora katika sekta ya afya, Irene Kiria, aliiambia Nipashe jana kuwa wanaona vifurushi hivyo si rafiki kwa kila Mtanzania.

"Sidhani kama lengo ni kumfikia kila Mtanzania, hii ni kuongeza wigo kwa watu wanaotaka huduma fulani, wakate kulingana na vifurushi walivyoviainisha," alisema.

Alisema kwa mantiki hiyo, wenye uwezo mdogo watapata huduma kulingana na viwango vyao, vivyo hivyo kwa walio na uwezo mkubwa kifedha.

Hata hivyo, Kiria alisema kuna haja kila mwananchi kuwa na bima ya afya na kuepuka matumizi ya fedha kwa vitu visivyo na tija.

"Una uwezo wa kununua gari, ujiulize gari na afya yako kipi ni kipaumbele chako, uzuri wa bima ya afya inakatwa mara moja kwa mwaka, lakini mtu ana uwezo wa kutumia fedha kwa ajili ya sherehe au msiba. Je, hicho ndiyo kipaumbele chako?" alihoji.

Alisema kama ilivyo nchi nyingine, Tanzania hadi sasa

INAENDELEA UK. 8

# Ongezeko watoto lamduwaza mbunge

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MBUNGE wa Solwa mkoani Shinyanga, Ahmed Salum, ameshangazwa na ongezeko kubwa la watoto vijijini na kuwataka wananchi wapunguze kasi ya kuzaliana ili kuondoa upungufu wa madarasa.

Salum alibainisha jana hayo alipokuwa kwenye ziara jimboni humo iliyokuwa na lengo la kusikiliza kero za wapigakura na kuzitafutia ufumbuzi. Kila alipokuwa kwenye mkutano wa hadhara alikuwa akiona idadi kubwa ya watoto.

Alisema ameshangazwa sana kuona kwenye mikutano hiyo kuna idadi kubwa ya watoto na kuwataka wananchi wapunguze kasi ya kuzaliana ili kutosababisha kuwapo upungufu wa madarasa pale watakapoanza kusoma shule, bali wazae kwa kuachia nafasi na si mfululizo.

"Naona wanaume sasa hivi mna rutuba sana maana kasi hii ya ongezeko la idadi kubwa ya watoto si mchezo na kwa vile nimeleta na huduma ya umeme basi chumbani ni kweupe tu. Ila nawaomba mpunguze kasi ya kuzaliana achieni nafasi, mtanipa changamoto ya kujenga tena vyumba vya madarasa tatizo ambalo nimeshalimaliza," alisema Salum.

Aidha alisema asilimia 90 ya ahadi zake ameshazitekeleza kwa wananchi jimboni humo na katika mwaka ujao wa fedha atakuwa amebakiza sehemu chache sana kukamilisha ahadi hizo, ikiwamo miradi ya umeme, maji ya Ziwa Victoria, ujenzi wa zahanati na miundombinu ya barabara.

Baadhi ya wananchi walipokuwa wakitoa kero zao, walisema changamoto kubwa ilikuwa kufungiwa umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), maji, afya, mitaro kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji mpunga na miundombinu ya barabara. Mmoja wa wananchi, Sofia Malale, kutoka kijiji cha Nyika, alisema kwenye kijiji hicho wanakabiliwa na ukosefu wa huduma ya afya, hali ambayo imekuwa ikisababisha kufuata huduma hizo umbali mrefu kwenye vijiji jirani.


中国水电
SINOHYDRO

**TANGAZO LA KAZI**

Sisi ni **SinoHydro Corporation Ltd** ambao hivi sasa tunatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagililiaji Zanzibar, katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa pamoja.

Tunaajiri waendesha magari mazito ya kubeba nyenzo, malori mazito, mafundi umeme, wapimaji, mafundi vyuma, wachanganya zege na wafanyakazi wenye ujuzi wa fani zinazofanana na hizo.

Tunanunua oil za magari, fito za chuma, simenti, kokoto, mawe ya ujenzi, mavazi maalum ya ujenzi,mabomba ya muundo maalum, bomba za chuma, vifaa umaliziaji ujenzi na bidhaa nyingine kama hizo.

**Pia tunahitaji mashine ndogondogo, vifaa na nyenzo za uendeshaji mashine.**

**Tafadhali peleka maombi yako au maelezo kwa**

**Bw. Yan kwa anuani yyg608@163.com au piga simu namba 0778 460047.**

115529602

# Sababu za kushamiri maambukizi VVU bayana

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MRATIBU wa kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi mkoani Shinyanga, Peter Mracha, ametaja maeneo ambayo yamekuwa yakisababisha kuendelea kuwapo vichocheo vya maambukizi mapya ya ugonjwa huo, hivyo kusababisha hali kuendelea kuwa mbaya.

Alitaja maeneo hayo kuwa ni sehemu za machimbo ya migodi ya madini, maegesho ya malori barabarani na sehemu ambazo kunafanyika biashara ya kuuza ngono hasa Shinyanga mjini na Kahama.

Mracha alibainisha hayo jana kuwa hali ya maambukizi ya VVU mkoani Shinyanga yamepungua hadi asilimia 5.9 ikilinganishwa na mwaka 2012 ilivyokuwa asilimia 7.4.

Pamoja na kupungua huko, alisema hali bado ni mbaya kwa kuwa takwimu za kitaifa maambukizi ni asilimia 4.7.

Alisema tatizo ambalo limekuwa likisababisha maambukizi kutoshuka zaidi na kufikia kiwango cha taifa mkoani Shinyanga ni kutokana na kuwapo na maeneo mengi yenye vishawishi vya ngono.

"Watu wengine ambao wamekuwa wakieneza maambukizi haya ya virusi vya ukimwi kwa kasi ni makahaba na wanaume ambao wamekuwa wakifanya mapenzi kinyume cha maumbile wakiwamo na madereva wa bodaboda ambao hufanya sana ngono zembe," alisema.

Baadhi ya vijana, akiwamo dereva wa bodaboda, Siga Njile, alipohojiwa na Nipashe juu ya nini kifanyike ili kupunguza kasi ya maambukizi hayo, alisema elimu inapaswa kuendelea kutolewa kwa ili watu wajikinge na kuacha ngono zembe.

Alisema mfano wao (bodaboda) wamekuwa wakikumbana na changamoto kwa baadhi ya abiria wanawake hasa nyakati za usiku.

Kwa mujibu wa Njile, wanapowapeleka sehemu husika na kuwafikisha wamekuwa wakidai hawana fedha ya kuwalipa na kuamua kumalizana kwa kufanya mapenzi vichakani bila hata ya kutumia kinga.



Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Benard Konga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa vifurushi vipya vya bima ya afya, utakaofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini humo, leo. Kushoto ni Meneja Uhusiano wa Mfuko huo, Angela Mziray. **PICHA: JOHN BADI**

# Ugonjwa kifua kikuu tishio nchini

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

TANZANIA inakadiriwa kuwa na idadi ya watu 60,000 wanaougua ugonjwa wa kifua kikuu (TB) kwa mwaka.

Pia ugonjwa huo unaambukiza kuliko magonjwa mengine kama mtu anayeugua hajaanza matibabu na kuwa na uwezo wa kuambukiza watu wengine 10 mpaka 20 kwa mwaka.

Akizungumza kwenye kikao cha waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia masuala ya Ukimwi, TB na madawa ya kulevya, Mbunge wa Biharamulo, Oscar Mukasa, alisema zipo njia nyingi za kupambana na kifua kikuu kwa wadau kushirikiana kwenye mapambano.

Mukasa alisema, viongozi wa dini na nyumba za ibada wana fursa kubwa ya kufikisha ujumbe, kuongeza ufahamu na kuleta umoja katika jambo fulani, hivyo wamefika Mkoa wa Mwanza kama kambi rasmi ya wabunge wapambanaji wa kifua kikuu chini ya ulezi wa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai kwa ajili ya kuwaweka pamoja viongozi wa dini na serikali ili nguvu yao na mifumo yao itumike vizuri katika kuleta ufahamu na kuhakikisha kwamba mapambano dhidi ya ugonjwa huo yanafanikiwa.

Mukasa alisema kesho kutakuwa na kikao cha shughuli maalum ya viongozi wa dini mbele ya Spika Job Ndugai kuweka sahihi kwenye maazimio yao kushirikiana na Bunge na Serikali kwa kutumia nyumba zao za ibada na mifumo yao yote katika mapambano dhidi ya TB.

Kikao hicho pia kitahudhuriwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Seleman Jafo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, na viongozi wa dini wakiwamo wa Baraza la Maaskofu Tanzania, Baraza la Kiislamu Tanzania (Bakwata) makanisa ya kipentekoste na mengineyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema kamati hiyo imekwenda kutangaza maazimio ya viongozi wa dini kuhusu mapambano dhidi ya TB huku asilimia sita ya wagonjwa wenye ugonjwa huo nchini wanatoka Mkoa wa Mwanza.

"Mwaka 2018 taarifa zilisema wagonjwa 4,640 nchini walitoka mkoani kwetu, hivyo ni takribani ya asilimia sita ya wagonjwa wote wa TB nchini waliotangazwa wanatoka Mwanza, " alisema Mongella.






# Tril. 2.3/- zasambaza umeme vijiji 8,000

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKALA wa Umeme Vijijini (REA), umetumia Sh. trilioni 2.3 kusambaza umeme katika vijiji 8,000 kati ya 12,268 nchini.

Aidha, wakala huo kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) itafanya tathmini ya watumiaji wa nishati hiyo kwenye maeneo ya vijijini.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Amos Maganga, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kabla ya REA kuanza mwaka 2017 asilimia mbili ya vijiji ambayo ni sawa na vijiji 518 vilikuwa na umeme.

"Baada ya wakala kuingia hadi sasa ni asilimia 66 ya vijiji vina umeme sawa na vijiji 8,000,"alisema.

Kuhusu tathmini hiyo, Maganga alisema lengo la tathmini hiyo ni kujua kama umeme unatumika ipasavyo kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi.

Alisema tathmini hiyo itajumuisha watu kutoka Wizara na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) na kila mmoja atasimama kwa nafasi yake na pia wataangalia wapi panahitaji kuboresha.

"Ziara itakuwa ya mwezi mmoja, tunaimani tutavifikia vijiji vyote ambavyo vimefungiwa umeme huo na ambavyo bado," alisema Maganga. Alisema ziara hiyo itasaidia Wizara ya Nishati kujiridhisha REA ilivyoweka umeme vijijini na matumizi yake. Haya hivyo alisema moja ya mikakati waliyojiwekea ni kuhakikisha hadi mwaka 2021 vijiji vyote vilivyobaki viwe vimefikiwa na umeme wa REA ili kuboresha maisha ya jamii.

Naye, Meneja Takwimu za Kilimo na Mifugo kutoka NBS, Titus Mwisomba, alisema ziara hiyo ni muhimu kwa sababu serikali inapaswa kuwa na takwimu sahihi za idadi ya watu wanaotumia umeme vijijini.

Alisema timu ya wataalamu ambayo itatembelea vijiji vyote kwa mujibu wa taratibu zilipangwa ili kuleta matokeo chanya.

Kaimu Mkurugenzi wa Sera na Mipango kutoka Wizara ya Nishati, Oscar Kashaigili, alisema wamejipanga kuhakikisha takwimu halisi na jamii imepokeaje uwepo wa umeme kwenye maeneo yao.

# Wasanii wapewa tano kutangaza utalii

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewapongeza wasanii kwa kuonyesha utayari wa kushirikiana na wizara katika kunadi vivutio vya utalii.

Kutokana na utayari huo, Kanyasu amewahakikishia wasanii wizara iko tayari muda wote kutoa ushirikiano kwa yeyote atakayetaka kufanya kazi ya kutangaza vivutio hivyo.

Akizungumza na wasanii mbalimbali na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi usiku, Kanyasu alisema kazi ya sanaa nchini inakua kwa kasi, hivyo wasanii hawawezi kuachwa nyuma katika kutangaza na kuhamasisha maendeleo ya utalii.

Mkutano huo uliwakutanisha wasanii mbalimbali wakiwamo wasanii wa filamu, vichekesho, uchongaji na washindi wa Miss Utalii wa miaka minne iliyopita.

Katika mkutano huo, alisema sanaa ni kichochea cha utalii kwa kuwa kupitia tasnia hiyo, Tanzania na vivutio vyake vinajulikana.

Alisema ushirikiano huo wa wasanii ni hatua muhimu kwa katika kufikia azma ya serikali ya awamu ya tano ifikapo mwaka 2020 ni kufikisha idadi ya watalii milioni 2.5.

Akizungumzia mashindano ambayo yanafanyika kwa mara ya nne tangu yalipoanzishwa, Kanyasu aliwapongeza waandaaji kwa kubuni vipengele viwili vya kuwatafuta walimbwende yaani Mlimbwende Utalii wa Tanzania na Mlimbwende wa Utalii wa Kimataifa. Kanyasu alisema ubunifu huo utasaidia kunadi vivutio vya utalii kitaifa kwa kumtumia Mlimbwende wa Utalii wa Tanzania huku vivutio hivyo vya utalii vitanadiwa kimataifa na yule wa kimataifa.

Aliongeza kuwa mashindano hayo yana sura mpya kwa kuzingatia muono wa kitaifa na kimataifa.

Mratibu wa Mashindano hayo, Gideon Chipungahelo, alisema vigezo vya kuwapata washindi hao mbali na ulimbwende watakaokuwa nao, watazingatia uelewa walio nao katika kuvijua vivutio vya utalii vilivyoko nchini.

"Tunamtaka mlimbwende atakayekuwa balozi wa utalii na mwenyekiti ushawishi wa kuwafanya watu wengine wahamasike kutembelea vivutio vya vtalii vilivyopo nchini." Alisisitiza.

Naye Mwakilishi wa Baraza la Sanaa Tanzania (Basata,) Anna Masenge, alisema mashindano hayo yatazingatia maadili ya Mtanzania na kamwe hayatakuwa kichocheo cha kuharibu utamaduni kwa vile waandaaji watazingatia kanuni na miongozo iliyotolewa na baraza hilo.

Alitoa wito kwa wazazi kuwaruhusu watoto wao kushiriki katika kinyang'iro hicho huku akiwatoa hofu kuwa mashindano hayo si uhuni kama wengi wanavyoyachukulia.



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya Bomag, inayofanya upanuzi wa barabara ya Bagamoyo, kutoka Morocco hadi Mwenge, wakiweka lami jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# EPZA yataka programu kuandaa wafanyakazi wa viwandani

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA) imesema Tanzania inaweza kuwa eneo bora zaidi la uwekezaji na kuvutia wawekezaji wengi endapo itakuwa na programu maalum ya kuandaa wafanyakazi wenye ujuzi wa kazi za viwandani.

Mkurugenzi Mkuu wa EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia alisema Tanzania na nchi za nyingine za Afrika zina kila kitu kinachotakiwa na wawekezaji zikiwamo malighafi, vyanzo vya kutosha vya umeme, ardhi ya kutosha na soko kubwa, lakini kukosekana kwa wafanyakazi wenye ujuzi unaotakiwa katika viwanda imekuwa kikwazo kikubwa cha kuvutia uwekezaji zaidi.

Simbakalia alisema hayo wakati akiongea na wahadhiri waandamizi kutoka vyuo 16 vya ufundi vya nchi tatu za Afrika, Tanzania, Kenya na Ethiopia ambazo zinashiriki katika mradi wa Eastern Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

"Wawekezaji pote duniani hufananishwa na ndege anayeruka kwa sababu huenda mara moja kuwekeza pale tu kwenye mazingira rafiki ya kibiashara," alisema wakati wa ziara ya wahadhiri hao katika kituo cha Ukanda maalum wa uwekezaji wa Benjamini William Mkapa, jijini Dar es Salaam, juzi.

Aliwataka wahadhiri waandamizi na vyuo vyao kuelekeza nguvu zaidi kuwaandaa vijana watakaokuwa na ujuzi wa kazi za viwandani ikiwa ni hitaji kubwa kwa wawekezaji wa viwanda kutoka sehemu mbalimbali duniani.

Akiwasilisha mada kwa wahadhiri hao, Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, James Maziku, alisema mapinduzi ya nne ya viwanda duniani yamebadilisha ujuzi unaohitajika katika viwanda.

Alisema serikali kwa kushirikiana na kiwanda cha Tanzania Tooku Garments wameanzisha programu maalumu ya kuandaa vijana watakaofanya kazi katika kiwanda hicho cha nguo.

Katika programu hiyo, serikali huwalipia vijana posho kwa miezi mitatu ya mafunzo yanayoendeshwa na wataalam wa kiwanda cha Tanzania Tooku Garments na baadaye kuwapa ajira.

Kupitia mradi wa EASTRIP unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, vyuo 16 vinatarajiwa kujenga uwezo wa kudahili zaidi ya wanafunzi 20,000 kwa mwaka ndani ya miaka mitano ili kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu.


NMB Karibu yako

## TAARIFA KWA WATEJA

**Mpendwa Mteja,**

Tunatarajia kufanya mabadiliko ya gharama za huduma zetu kuanzia tarehe **27 Disemba, 2019**.

Tunaendelea kuboresha huduma zetu na kuhakikisha zinapatikana kwa gharama nafuu ili kuendelea kuwa benki pendwa kwa kila Mtanzania.

Kwa mwaka huu wa 2019, tumeendelea kutanua wigo wa huduma kwa kuongeza matawi, wakala na ATM nchi nzima ili kuendelea kukupatia huduma kwa urahisi na kubaki Karibu Yako.

Kwa mwaka 2020, tutaendelea kuboresha huduma, kwa kufungua matawi zaidi, kuongeza wakala pamoja na ATM. Pia, tutaendelea kuwa wabunifu kwa kukuletea huduma mpya za kukuwezesha kuboresha maisha yako na biashara yako.

Tunakushukuru kwa kuendelea kuwa mteja wetu na kutupa ushirikiano, ambao, umetuwezesha NMB kuwa benki inayoongoza Tanzania.

Kwa maelezo zaidi au ufafanuzi kuhusu mabadiliko haya, **tafadhali tembelea Tawi lolote lililo karibu nawe au tupigie 0800 002 002.**

Wako,

**Benki ya NMB**

| Huduma | | Gharama Tshs |
|---|---|---|
| Gharama ya mwezi (Monthly fees) | NMB Bonus Account | Bure |
| | NMB Mwanachuo Account | Bure |
| | NMB Wisdom Account | Bure |
| | Personal Accounts / TPDF Account | 1,800 |
| | NMB Mtoto Account | Bure |
| | NMB Chipukizi Account | Bure |
| | NMB ChapChap Account | Bure |
| Ada ya kutoa fedha Ndani ya tawi | Savings Accounts (Bonus AC, Mtoto AC na Business Savings AC) | 4,000 |
| Muamala wa fedha za kigeni kupitia kadi yako ya benki | Muamala wa fedha za kigeni kupitia kadi yako ya benki | 3% |
| Kutoa fedha kwenye ATM | Ada ya kutoa fedha ATM | 1,100 - 1,500 |
| Kutoa fedha kwa Wakala | Kuanzia: TZS 6,000,000 - 6,999,999 | 10,700 |
| | Kuanzia: TZS 7,000,000 - 7,999,999 | 12,600 |
| | Kuanzia: TZS 8,000,000 - 8,999,999 | 13,900 |
| | Kuanzia: TZS 9,000,000 - 10,000,000 | 15,000 |
| Kuweka Sarafu | Kuweka Sarafu | 10% |
| Kutuma fedha - Benki kwenda mitandao ya simu | Kuanzia: TZS 1,000 - 5,000 | 900 |
| | Kuanzia: TZS 5,001 - 20,000 | 1,800 |
| | Kuanzia: TZS 20,001 - 30,000 | 2,700 |
| | Kuanzia: TZS 30,001 - 50,000 | 4,000 |
| | Kuanzia: TZS 50,001 - 100,000 | 5,000 |
| | Kuanzia: TZS 100,001 - 200,000 | 7,000 |
| | Kuanzia: TZS 200,001 - 300,000 | 7,500 |
| | Kuanzia: TZS 300,001 - 400,000 | 8,000 |
| | Kuanzia: TZS 400,001 - 500,000 | 8,700 |
| | Kuanzia: TZS 500,001 - 1,000,000 | 10,000 |
| | Kuanzia: TZS 1,000,001 - 2,000,000 | 11,000 |

215535202

www.nmbbank.co.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Idadi kubwa ya walimu waliofukuzwa inatisha

**TAARIFA** kuwa walimu 4,046 wamefukuzwa kazi ndani ya miaka mitatu kwa utovu wa nidhamu ni za kusikitisha na kutisha, hivyo kuna umuhimu wa kulitafakari suala hili.

Ni jambo la kusikitisha kwa kuwa bado taifa letu lina mahitahi ya walimu kwa ajili ya kuwafundisha watoto wetu katika shule zilizotapakaa maeneo mengi ya nchi.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Winifrida Rutaindurwa, na kufafanua kuwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, idadi ya walimu waliofukuzwa kazi ni sawa na asilimia 70 ya waliopewa adhabu kutokana na makosa ya kinidhamu.

Aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipotoa taarifa ya tume kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuundwa kwake wakati wa kikao kazi cha kaimu makatibu wasaidizi wa wilaya nchini.

Alisema walimu 930, sawa na asilimia 16.2 ya waliopewa adhabu, walipewa onyo na wengine 284, sawa na asilimia 4.9, walipunguzwa mshahara. Vilevile, alisema walimu 244, sawa na asilimia 4.2 ya waliopewa adhabu, walisimamishiwa nyongeza ya mshahara.

Kwamba walimu wengine 237, sawa na asilimia nne ya waliopewa adhabu, walishushwa cheo na walimu 14, sawa na asilimia 0.2 ya waliopewa adhabu, walifidia hasara.

Rutaindurwa alisema makosa ya kinidhamu yaliyofanywa na walimu katika kipindi hicho cha miaka mitatu ni pamoja na utoro kazini (makosa 5,447, sawa na asilimia 76.5 ya makosa yote).

Makosa mengine ni kukiuka maadili (makosa 1,290 sawa na asiliimia 18.1, uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi 162 (asilimia 2.3). Makosa mengine kwa ujumla wake yalikuwa 224, sawa na asilimia 3.1 na vilevile katika kipindi cha miaka mitatu, adhabu zilizotolewa ni 5,753.

Taarifa ya Rutaindurwa kwamba asilimia 76.5 ya makosa yote ni utoro ni suala linalotisha ma kusikitisha. Aidha, hali hiyo inathibitisha madai ambayo yamekuwa yakitolewa mara kwa mara kuwa walimu wengi ni watoto kazini, hivyo hiyo ni changamoto kubwa ambayo inapaswa kufuatiliwa na kupatiwa ifumbuzi na mamlaka husika.

Tunasema hivyo kwa kuwa utoro wa walimu ni kosa kubwa ambalo linawaathiri sana wanafunzi moja kwa moja kitaaluma, kwa kutilia maanani kuwa kwa sasa serikali inatoa elimu bila malipo kwa shule za msingi na sekondari.

Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi, ambayo ndiyo inayomiliki shule zote na walimu bila shaka imepewa taarifa hizi na tunaamini kuwa viongozi wake wakiongozwa na Waziri Selemani Jafo watafuatilia na kuchukua hatua.

Jambo la msingi ambalo serikali inapaswa kulitafutia majawabi ni kwa nini walimu wanakuwa watoto kazini wakati wanalipwa mishahara na serikali?

Kwa upande wetu Nipashe, tunaona kuwa sababu ya utoro wa walimu kazini ni kukosekana kwa taratibu za kuwafuatilia wawapo kazini. Miaka ya zamani idara ya ukaguzi ilipokuwa chini ya Wizara ya Elimu kulikuwapo na ufuatiliaji wa karibu wa walimu kutokana na ukaguzi wa mara kwa mara shuleni.

Hata hivyo, kwa sasa inaonekana ndani ya Tamisemi kuna udhaifu wa ukaguzi katika shule, hivyo, tunaishauri wizara kuangalia uwezekano wa 'kuiamsha' idara hiyo ikiwamo kuiwezesha kwa vifaa na fedha ili itekeleze vyema majukumu yake katika mazingira rafiki. Tunaamini kwa kufanya hivyo, itakuwa ni rahisi kupunguza utoro wa walimu kama siyo kuumaliza kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Sabato Kasika

### TGNP- Mtandao inavyomtaka mwanamama kuchangamka

**HISTORIA** inaonyesha mchakato wa kupigania haki za wanawake kote duniani, ulianza takriban karne moja iliyopita na bado juhudi za kupigania zinaendelea, ili kuhakikisha kile kilichokusudiwa kinatimia.

Nchini kwetu, serikali na wadau mbalimbali zikiwamo asasi za kiraia kama TGNP Mtandao, wamekuwa mstari wa mbele kutetea haki za wanawake ili kuhakikisha wanashiriki kwenye nyanja mbalimbali za maendeleo, bila kusahau mustakabali wa uchumi.

Lengo kuu ni kutaka kuwapo usawa kati ya mwanaume na mwanamke kwenye ngazi za maamuzi na hata kusimamia shughuli za maendeleo, ikiwamo umiliki wa viwanda vya kuzalisha mali, vidogo na hata vikubwa inapobidi.

Hapa ngoja nitaje baadhi ya haki zinazopiganiwa kwa ajili ya kumkomboa mwanamke, ambazo ni usawa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kijamii, kisiasa katika kufikia maendeleo jumuishi.

Nikiri nchini Tanzania, kuna jitihada mbalimbali zilizofanywa na jamii, serikali, asasi za kiraia, sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika kumwinua mwanamke.

Kwa upande wa asasi za kiraia, asasi hii ya TGNP Mtandao, ni miongoni mwa walio mstari wa mbele kupigania haki za mwanamke katika nyanja zote na hasa wakati huu, nchi inaelekea kuwa ya viwanda.

Hii inatokana na ukweli kwamba, haki na usawa katika hilo, ndiyo mambo makuu yanayoshinikizwa duniani kwa ajili ya kufanya mabadiliko, kuhimiza na kuwawezesha wanawake wa nyanja zote kutambua uwezo wao.

Licha ya kwamba mwanamke anachangia katika ukuaji uchumi, bado baadhi ya maeneo hayajashirikishwa kikamilifu, kwani mwanajinsia huyu amekuwa akikutana na vikwazo na anapata ajira zenye vipato vya chini na pia nafasi finyu ya kujiendeleza.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, ili kutimiza, malengo ya maendeleo endelevu kama sehemu ya ajenda ya mwaka 2030, kuna haja ya kuisaidia Afrika kushinikiza ustawi endelevu wa kiviwanda na unaojumuisha kila mtu.

Baadhi ya nchi za Afrika ikiwamo Tanzania, zinapania kuwa na nchi zilizoendelea kiviwanda, lakini kwa mara nyingi idadi kubwa ya wanawake wanaonekana kususia kujitosa katika sekta hiyo.

Lakini ni bahati nzuri serikali ya Tanzania ilishaidhia Itifaki ya Maendeleo na Jinsia ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), inayosisitiza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi kitaifa.

Katika taifa lililoridhia itifaki hiyo ya maendeleo, Tanzania imefanikiwa kufikia asilimia 37 ya wanawake bungeni, asilimia 41 wanawake majaji na asilimia 30 kinamama madiwani. Ni hatua nzuri, japo inahitaji kusonga zaidi.

Kutokana na jitihada hizo, wanawake wanaendelea kuaminika na kuchukua nafasi za juu za uongozi na maamuzi. Tunawashuhudia sasa wachapa kazi kama wakuu wa wilaya, wakurugenzi na vyeo kama hivyo.

Hivyo, wakati huu ambao nchi inaelekea kuwa ya viwanda, bado kuna uhakika kuwa wanawake hawataachwa nyuma, kutokana na ukweli kwamba uchumi unajengwa na Watanzania wa jinsia zote.

Pamoja na jitahada hizo za kuwezesha wanawake, siyo vibaya wadau wengine kama nilivyowataja TGNP Mtandao, wakaendelea kutia joto ili kuhakikisha wanawake hawabaki nyuma kwenye maendeleo ya nchi yao.

Ninaitambua Siku ya Wanawake Duniani, inayoadhimishwa kila Machi 8 ya mwaka, ikilenga kutambua mchango wa wanawake katika nyanja mbalimbali na kumuinua kimaendeleo.

Kuna maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyowahi kuwa na kaulimbiu isemayo: 'Kuelekea Uchumi wa Viwanda: Tuimarishe Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake Vijijini'.

Kwa maana hiyo, wawe wanawake wa mijini na vijijini, wote wanatakiwa kusaidiwa, kwa kila hali ili kuhakikisha wanakuwa na mchango katika Tanzania ya Viwanda.

Hata wanawake wakulima, wanatakiwa kupata elimu ya kukuza biashara zao na kuona thamani ya kile wanachokifanya kwa kuboresha huduma zao na kutengeneza mnyororo mpya wa thamani.

Kwa kufanya hivyo, ni wazi kwamba watakuwa na mchango mkubwa kwenye Tanzania ya Viwanda, kwani viwanda vinavyojengwa vimo ambavyo vinategemea mazao kutoka kwa wakulima, wakiwamo wanawake.

Hivyo, jitihada zinazofanywa na asasi za kiraia, ikiwamo TGNP Mtandao, kwa ajili ya kutambua mchango wa mwanamke hasa wakati huu wa kuelekea Tanzania ya Viwanda, hazina budi kuungwa mkono na wadau wote.

Hata urasimishaji wa vikoba na kuwashawishi wanawake wengi zaidi kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii, ili kuweza kunufaika na mafao na mikopo itolewayo na taasisi hizo, bado ni njia mojawapo ya kumwezesha mwanamke, hizo nazo ziungwe mkono.

## Gharama hizi ipi ni sahihi ?

**MHARIRI,**

*SISI wakazi wa maeneo mengi ya Dar es Salaam tunashangazwa na maelezo mbalimbali wanayotupa wapima ardhi.*

*Awali tulisikia tangazo la serikali kuwa kila mwananchi atachangia Shilingi 150,000 kwa ajili ya mradi wa kurasimisha makazi ya wale wanaookaa sehemu ambazo hazijapimwa.*

*Hilo lilikubalika lakini ghafla tena yakaibuka maelezo mengine yenye gharama zaidi , mwananchi akitakiwa kulipa Sh 180,000 ili kupata jiwe kwa ajili ya makazi.*

*Mkanganyiko wa gharama umewachanganya watu ambao wanaamini kuwa kiwango kilichotangazwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuwa ndicho sahihi.*

*Hata hivyo ni vyema tukapewa ufafanuzi ili kujua kipi ni kipi hasa nyakati hizi ambazo watu wanajali zaidi gharama kutokana na ugumu wa upatikanaji fedha.*

**Mzire Chawala**
**Mivumoni**
**Dar es Salam.**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# 2020 kujiandikisha kupata vitambulisho au kupiga kura?




**Na Salome Kitomari**

HIVI karibuni Watanzania walipiga kura ya kuchagua viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa, ambao umejenga msingi wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Watu takriban milioni 19 kati ya milioni 55 walijitokeza kujiandikisha katika daftari la orodha ya wapigakura, na baadhi walitimiza wajibu wao wa kikatiba kwenye maeneo ambayo uchaguzi huo ulifanyika. Hata hivyo zipo sehemu mbazo uchaguzi haukufanyika kutokana na wagombea kupita bila kupingwa na kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wanatangazwa kuwa washindi, huku maeneo mengine kukifanyika uchaguzi.

Uchaguzi huo umefanyika wakati vyama nane vya upinzani vilitangaza kususia na kutaka majina ya wagombea na vyama vyao yasiwepo kwenye karatasi ya kupigia kura, huku Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikisisitiza kuwa wagombea wote waliowekewa pingamizi, waliokatwa na ambao fomu zao zilipokelewa watashiriki uchaguzi huo.

Aidha, baada ya vyama hivyo kutangaza kujitoa na kuwataka baadhi ya wagombea ambao fomu zao zilipokelewa kuandika barua za kujitoa, huku wengine wakishindwa kuwasilisha barua kwa kuwa ofisi zimefungwa.

'Figisufigisu' zilizonekana mapema kabisa kwa wagombea wa upinzani kukatwa majina yao kwa sababu ambazo hazikuwa za msingi, mathalani ambaowaliandika ACT bila kumalizia Wazalendo na wapo walioandika CDM badala ya kuandika kwa kirefu Chadema.

Wengine walikataliwa kwa kuwa wameathiriwa na lugha mama yaani mahali pa kutamka R anatamka L, huku wengine wakikimbiwa na watendaji ambao ndiyo wenye wajibu wa kupokea fomu za uchaguzi huo kabla ya siku ya mwisho.

Jumapili iliyopita Novemba 24 uchaguzi huo ulifanyika kwenye baadhi ya vijiji, mitaa na vitongoji ambavyo majina ya wagombea yalikuwapo kwenye karatasi za kupigia kura na hadi sasa CCM imeshinda kwenye mitaa yote, vijiji vyote isipokuwa kimoja ambacho mgombea wa CUF ni mshindi.

Kabla ya kufunguliwa kwa milango ya kuchukua fomu za kugombea, wananchi walionyesha 'kujivuta' kwenda kuchukua fomu kutokana na mwamko mdogo kwa sababu nyingi, na kazi kubwa ilifanyika kuhamasisha wananchi kwenda kujiandikisha na hadi sasa mamilioni hawajajiandikisha licha ya kuwa na sifa.

Nguvu kubwa ilitumika kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi kujiandikisha ikiwa ni tofauti na wakati wa Daftari la Wapigakura mwaka 2015, ambao walijiandikisha kwa hiari kutokana na umuhimu wa vitambulisho vya mpiga kura.

Sababu zinazoelezwa kwa wengi kujiandikisha wakati tayari mshindi ameshajulikana, nyingine ni hakuna umuhimu kwa kuwa hata usipopiga kura kutakuwa na washindi.

Itakumbukwa kwa mwaka 2015 idadi ya waliojiandikisha kwenye daftari la kudumu la wapiga kura ilikuwa zaidi ya milioni 23.2 ikilinganishwa na waliojiandikisha kwenye daftari la orodha ya wapigakura 2010 ambao walikuwa ni zaidi ya milioni 19.

Kwa wakati huo, kilikuwa kinatolewa kitambulisho cha mpigakura ambacho kilikubalika maeneo mengi ikiwamo kumwekea mtuhumiwa dhamana, kwa kuwa hakukuwa na vitambulisho vya taifa. Sasa vitambulisho hivyo vipo na ndivyo vinavyotambulika rasmi kwenye maeneo mbalimbali.

Ili kuendelea kushawishi wananchi kwenda kujiandikisha na kupiga kura inahitaji kurejesha mazingira ya kisiasa yenye ushindaji sawa kwa wanaofanya siasa, kuliko kwa upande mmoja kuumia dhidi ya mwingine.

Mathalani, kwa sasa vyama vya upinzani haviruhusiwi kufanya siasa na mara kadhaa wahusika wamekamatwa hata kama walikwenda kwenye jimbo fulani kwa ajili ya majukumu mengine na wametakiwa kuomba kibali cha kwenda sehemu husika.

Wengi wamejikuta wakifanya vikao vya ndani chini ya ulinzi wa polisi kwa maelekezo ya wakuu wa wilaya na mikoa, jambo ambalo ni tishio kwa ukuaji na ustawi wa demokrasia ya vyama vingi.

Kwa yaliyojitokeza sasa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa ndiyo yanaakisi uhalisia wa uchaguzi mkuu ujao, na hasa wakati huu ambao kuna uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa mfumo wa BVR.

Wananchi wanatakiwa kuboresha taarifa zao kama wamehama maeneo mengine iwapo wametimiza umri wa miaka 18, kuondoa waliofariki kwenye daftari, lakini tangu ielezwe kuwa kitambulisho cha taifa ndiyo muhimu kwenye mahitaji yote, wananchi wamejikuta kwenye misururu mirefu ya kutafuta vitambulisho hivyo na hawaoni umuhimu wa kitambulisho cha mpigakura.

Nakumbuka mwaka 2015 ulivyokuja mfumo wa kusajili wapiga kura kielektroniki -BVR, wananchi walijiandikisha kwa kasi kwa kuwa walijua wakipata vitambulisho hivyo vitawarahisishia kwenye kudhamini watu mahakamani, kupata huduma za kibenki na huduma nyinginezo, lakini kwa sasa umekuja utaratibu wa vitambulisho vya taifa.

Ni wakati wa kufikiria kutoa elimu ya kina kwa wananchi ili waendelee kujitokeza kujiandikisha ili kuwa na idadi kubwa ya waliojindikisha na watakaopiga kura, kuliko hali ilivyosasa ambako wengi wameona hakuna umuhimu wa kupiga kura.

Hata uchaguzi uliopita waliojiandikisha walikuwa wengi lakini waliojitokeza kupiga kura wachache sana, jambo ambalo halijapata jibu kiasi kwamba anayekuwa kiongozi wa eneo fulani anakuwa amechaguliwa na wachache, lakini kwa kuwa katiba inaeleza kuwa anayeshinda atahesabika mshindi kati ya wale walioshinda uchaguzi husika. Ni wakati wa kuwahamasisha watu kupiga kura si kukimbilia kupata vitambulisho.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Vifurushi vipya bima ya afya vyazua jambo

INATOKA UK. 3

ilitakiwa iwe na sheria ya kumlazimisha kila raia aingie katika huduma ya bima ya afya.

"Huu ndio mwelekeo na ni uamuzi wa miaka minne au mitano iliyopita," alisema.

Joseph Agustino, mkazi wa Kurasini jijini Dar es Salaam, akizungumza na Nipashe jana kuhusu vifurushi hivyo, alisema serikali iangalie namna ya kupunguza bei ili kila familia ijiunge na mfuko huo.

"Mimi naona gharama ziko juu, angalau ingeshuka chini ya 100,000," alisema, huku akiungwa mkono na Yusuph Athuman, mkazi wa Tandika jijini.

Athuman alidai kila Mtanzania anapenda kuwa na kadi ya bima ya afya, lakini kama gharama hazitapunguzwa, bado tatizo la wananchi kutojiunga na mfumo wa bima ya afya litaendelea nchini.

Hoja hiyo pia iliungwa mkono na Khadija Jumanne, mkazi wa Buguruni jijini, ambaye pia aliomba gharama za kukata bima za afya kwa ajili ya familia zipungue.

**WAZIRI ATETEA**

Jijini Dodoma, jana Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alizungumza na waandishi wa habari kuhusu vifurushi hivyo, alisema ni vya hiari.

Alikiri kuwapo kwa malalamiko kuhusu gharama kubwa za vifurushi hivyo na kueleza kuwa wako kwenye mchakato wa kukamilisha sheria ambayo itashusha viwango vya kuchangia ili wananchi wamudu. Sheria hiyo ambayo bima ya afya itakuwa ni lazima inatarajiwa kupelekwa bungeni Februari mwakani.

Alisema vifurushi hivyo vinavyotolewa na NHIF ni vya hiari wakati serikali ikielekea kwenye mpango wa bima ya afya ya lazima.

"Sisi tulipata malalamiko kwamba mtu ambaye yupo nje ya serikali, anatakiwa kulipa Sh. milioni 1.5, hakukuwa na kifurushi cha mtu mmoja mmoja ndani ya NHIF isipokuwa vya wajasiriamali.

"Kwa hiyo, tulivyofanya, tumechambua hivi vya Sh. milioni 1.5, tukasema hebu tupime ni kiasi gani tunaweza kutoza ili mtu mmoja mmoja aweze kukata.

"Kuna watu wanaviona ni gharama, lakini si gharama ukiangalia na gharama za matibabu, mkiwa watu sita, ni ile ile Sh. milioni 1.5, ukiwa kwa watu sita, kila mmoja Sh. 250,000, lakini maana ya bima mnachangiana, mkikata watu sita, si rahisi wote kuumwa, mkishaweka bima ya mtu mmoja mmoja, nina uzoefu na unatuonesha wanaokata wengi ni wagonjwa," alisema.

Aliongeza kuwa walichukua kiwango cha Sh. 250,000 na kuna baadhi ya gharama kidogo walipandisha ili wanufaika wachangiane.

"Mimi naamini itawasaidia watu wa kipato cha chini, juzi, kuna mtu alinifuata ana gharama ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya kupata huduma pale MOI. Sasa, mtu apime laki tatu (Sh. 300,000) kabla ya kuugua na kulipa Sh. milioni 10 baada ya kuugua ipi nafuu," alisema.

Alitolea mfano huduma za chini ya uangalizi (ICU) kwa siku Hospitali ya Taifa Muhimbili ni Sh. 500,000 kwa mtu binafsi na hospitali zisizo za serikali ni Sh. milioni 1.5.

**UZINDUZI LEO**

Jana, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, aliwaambia waandishi kuwa wanatarajia kuzindua huduma za vifurushi hivyo vya bima ya afya leo.

Alisema vifurushi hivyo walivyovipa majina ya 'Najali', 'Wekeza' na 'Timiza Afya', vinaanzia Sh. 192,000 kwa mtu mmoja hadi Sh. milioni 1.9 kwa familia.

Alisema katika kuboresha huduma hizo, pia wameanzisha huduma ya dunduliza kwa kushirikiana na benki na kampuni za simu, itakayomwezesha mteja kuwekeza fedha kidogo kidogo na zitakapotimia, atalipia bima yake.

Alisema pia wanatarajia kuanzisha huduma ya bima kwa makundi maalum wakiwamo wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga na mama lishe.

Alibainisha kuwa mfuko huo kwa sasa una wanachama milioni 4.6, sawa na asilimia 8 ya Watanzania na kwamba lengo ni kufikia asilimia 50 ya Watanzania kufikia mwakani.

■**Imeandikwa na Ibrahim Joseph (DODOMA), Mary Geofrey na Romana Mallya (DAR).**



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa stendi mpya ya mabasi ya mikoani katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CCM yamvaa tena Membe

INATOKA UK. 2

utafanywa na umma kujulishwa. Alisema hiyo si kwa Membe peke yake.

"Wakati utafika Watanzania na wanachama wataelewa nilikuwa na maana gani kumwita nilivyokuwa Geita. Membe ni mwanachama mwenye haki zote za kikatiba, lakini ana wajibu kama mwanachama," alisema.

"Kama anataka kuwa mwanachama wa CCM kama walivyo wanachama mamilioni na wengine hawajulikani hata majina lakini wana mchango mkubwa na wametupa ushindi tunaojivunia, (Membe) afuate utaratibu na asipofuata atalazimishwa kufuata na hatakuwa wa kwanza.

"Ukifanya rejea ya maisha ya CCM kama chama cha siasa utabaini kwamba vikao vya chama ndivyo hujadili wanachama tabia, vitendo na mwenendo wao. Majina mengi yamejadiliwa kwenye vikao. Sipendi kuzua mjadala upya," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema Membe ni mwanaCCM na anapaswa kufuata utaratibu na kwamba hajavunja utaratibu kwa wakati huu na kwamba hawajatangaza kwa kumwita, kwa kuwa kuna wakati alionekana kama mwanachama bora na pekee kuliko wengine.

**MAKAMBA, NAPE BADO**

Kuhusu Nape Nnauye na January Makamba ambao walimwomba Rais na Mwenyekiti wa CCM msamaha, Dk. Bashiru alisema wanapaswa kuomba pia chama radhi kwa sababu ya kauli zao.

"Mwenyezi Mungu ni mwingi wa huruma na ametoa nafasi ya toba, CCM ni chama cha watu si malaika na aliyekukosea leo anaweza kujirudi na kusahihisha. Kukiri makosa ni tabia tabia nzuri ya mwanasiasa," alisema.

Alisema wako waliofukuzwa moja kwa moja lakini walirejeshwa na kusamehewa hata kama walitukana au kuhujumu matusi si sehemu ya siasa ndani ya chama na nidhamu ndiyo msingi.

"Kukiri makosa ni tabia nzuri ya mwanasiasa, tulifukuza watu waliandika barua wameandika barua tumewasamehe. Hata mimi ni mtu wa kukosea, masuala ya kutokosea yapo mbinguni hapa duniani ni watu wa kukosea tunapokea tunasamehe.

"Kufukuza ni jambo endelevu kama itathibitika unadhoofisha chama. Tutachukua hatua ndani ya chama. Kwa wale waliosamehewa na Rais, aliwasamehe kama Mtanzania, matusi ya kumtukana Rais yeye anaweza kusamehe, lakini ya kumtukana Mwenyekiti wa chama lazima wajibu," alisema.

"Wanamashtaka ya kujibu kwenye chama, wakileta maombi ya msamehe ndani ya chama ni sawa, msahama ni wa Rais kama Mtanzania, kama mzazi na raia. Ndani ya chama wote watakaothibitika kwamba kwa vitendo vyao au kauli zao wamedhalilisha chama na uongozi wake wana mashataka, wataulizwa, watajitetea halafu uamuzi utafanywa kwenye vikao," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Bushiru, sauti zilizovuja za Makamba na Nape na waliokuwa makatibu wakuu wa CCM, Abdulrahman Kinana na Yusuph Makamba, zilikwera sana kwa kuwa zilikuwa za ovyo na si za wana CCM bali waharibifu na kwamba wakibaini wengine watawafukuza kabisa.

"Ukiwa mbunge ndani ya CCM unakuwa mjumbe wa kamati ya wabunge wa CCM ambao mwenyekiti wao ni Waziri Mkuu ambaye ni mjumbe wa Kamati Kuu. Kama una jambo linakukera si sahihi kuongea hivyo kwa kuwa wana nafasi ya kuongea na Katibu Mkuu wakati wowote," alifafanua.

## Serikali yashusha bei nyumba mradi PSSSF

INATOKA UK. 3

madalali kwa watu wengine.

"Mfanyakazi afaidike na mtu binafsi naye afaidike kama ilivyokuwa na mtu anaishi kupitia mgongo wa mtu fulani wajitokeze hadharani tunataka kumtambua mwenye nyumba ni nani," alisema.

"Maagizo ya Rais wetu mnayajua mifuko iwekeze ipate faida kwa wakati ihudumie mafao ya wanachama sasa tukiendelea kuziacha hizi nyumba bila faida yoyote mafao kwa wanachama yatakosekana miaka sita inatosha huu ni mwaka mwingine naomba maagizo yangu yasimamiwe vizuri," alisema.

Pia, alisema kuna miradi ya aina hiyo mikoani inayoitwa ya bei nafuu wakati nyumba zinauzwa bei kubwa na kusema agizo la kupunguza bei ni la nchi nzima.

Serikali pia, imeagiza taasisi ambazo ni wadau wa mradi huo ikiwamo manispaa ya Ilala kutengeneza miundombinu ya barabara na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa) kutengeneza miundombinu ya maji.

Aidha, alisema serikali inatoa wito kwa taasisi za kifedha kuchangamkia fursa ili kutoa mikopo nafuu kwa kuwa serikali imeonyesha mfano wa kupunguza bei za nyumba.

Waziri ameagiza bodi ya wadhamini pamoja na menejimenti ya mfuko kuhakikisha wasimamizi wa majengo wanatimiza wajibu wao.

"Pia Menejimenti ipime utendaji wao wa kazi na ifikapo Januari 31, 2020 itoe taarifa ya utendaji wao wa kazi kwa wale ambao hawajatimiza malengo waliyoelekezwa wataondolewa," alisema Waziri.

Mradi huo ulianzishwa mwaka 2011 na kukamilika 2013 ukiwa ni sehemu ya kimkakati wa PSPF na sasa PSSSF wa kuondoa tatizo la makazi kwa watumishi wa umma kama sehemu ya maandalizi pindi watakavyostaafu.

Baada ya mradi kukamilika ulitangazwa kwa watumishi walianza taratibu za kununua nyumba hizo na mtumishi mwenye umri mdogo kulipa kwa muda usiozidi miaka 25.

## HABARI KITAIFA

# ZAECA yaja na kasi mapambano rushwa

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), imewataka wananchi kushirikiana na mamlaka hiyo kutoa taarifa sahihi wanapoona kuna ubadhirifu wa mali za umma au vitendo vya rushwa.

Akizungumza na wanakijiji wa Semewani Shehia ya Kwale Wilaya ya Chakechake, Ofisa Elimu kutoka Mamlaka hiyo, Kassim Yussuf Ali, aliwataka wananchi hao wasiogope kuwafichua wanaotenda vitendo hivyo.

Alieleza kuwa kuundwa kwa mamlaka hiyo kumedhihirisha kuwa serikali inaamini falsafa yake inayosimamia utawala bora, uwazi na uwajibikaji, hivyo aliwataka wananchi hao kuziunga mkono juhudi hizo za serikali kwa kutoa taarifa katika mamlaka husika pale wanapoona kuna dalili ya vitendo hivyo.

"Niwaombe wananchi wote wasiogope kuwafichua wahalifu wa vitendo vya rushwa na wanaohujumu uchumi kwani mamlaka hii imeundwa na serikali ili kuwatetea wanyonge wa nchi hii kwa kuwa mapato yao yanachukuliwa na watu wachache katika Taifa hili," alisema Kassim. "Lakini pia nawaomba wananchi kuiunga mkono mamlaka hii kwa kutoa taarifa sahihi pamoja na kushirikiana kutoa ushahidi, kwani hapa ndipo tunaposhindwa kufanya kazi vizuri kutokana na wananchi kushindwa kutoa ushahidi wanapohitajika," alieleza.

Aliwaeleza wananchi hao kuwa rushwa imegawika katika makundi matatu ambayo ni ya ngono, muhali na ya hongo.

Kassim alieleza kuwa rushwa ya hongo hutumika zaidi katika kipindi cha uchaguzi ambapo baadhi ya viongozi ambao hawajiamini katika nafasi wanazogombea, huwarubuni wananchi kwa kuwapitia mgao wa khanga au bahasha ambazo ndani yake huingiza fedha ili waweze kuchaguliwa.

"Kwa upande wa rushwa ya ngono, hili limetawala sana katika idara mbalimbali za serikali na binafsi... jambo hili linawaathiri sana kinamama hasa pale wanapokwenda kuomba nafasi za ajira kwa kuwa huombwa rushwa hiyo na baadhi ya watendaji wanaoshughulikia nafasi hizo," alifafanua.

Kassim alieleza kuwa rushwa ya hongo nayo imekuwa ikiathiri Taifa, hasa wananchi wenye kipato cha chini wanakosa huduma muhimu ambazo ni haki yao.

Hata hivyo, aliwapongeza masheha kwa kuonyesha ushirikiano mkubwa kwa mamlaka hiyo, hasa pale wanapowanahitaji wananchi katika shehia zao kwa ajili ya kuzungumza nao.

Naye Khamis Kombo Mohammed kutoka mamlaka hiyo, alisema lengo la mkutano huo ni kuwaelimisha wananchi juu ya athari zinazopatikana katika rushwa na kuelewa mamlaka ambayo imepewa jukumu la kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Wananchi hao waliishukuru ZAECA kwa kwenda kutoa elimu ya rushwa katika shehia yao na kuwaomba wawe na kawaida ya kuwaelimisha ili wapate kuelewa mambo mbalimbali.



Wachimbaji wadogo wa migodi ya Msasa Nyarugusu na Nyakagwe, wakiingia kwenye mgodi wa mfano wa Nsangano, mkoani Geita hivi karibuni, ambao umejengwa kwa zege tofauti na mazoea ya wachimbaji wadogo wanaotumia magogo ambayo huhatarisha usalama wao na kuharibu mazingira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watunukiwa kubuni miradi ya maendeleo

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WAJUMBE 40 wa vituo vya taarifa na maarifa nchini wametunukiwa vyeti vya heshima baada ya kufuzu elimu ya ajira kwa wanawake na vijana kwa kuanzisha viwanda na kubuni miradi ya maendeleo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Kibena Kingo, alisema hayo wakati akifunga mafunzo ya siku saba ya kuwajengea uwezo wa uzalishaji kiuchumi wajumbe wa vituo vya taarifa na maarifa vilivyo chini ya Mtandao wa Jinsia Tanzania TGNP-Mtandao, walioandaa kwa kushirikiana na SUGECO.

Kingo alisema elimu waliyoipata wanawake na vijana itawasaidia kupambana na changamoto ya ukatili wa kijinsia na kuhakikisha inakomeshwa katika vijiji na kata kupitia miradi hiyo ya kuwawezesha kiuchumi.

Alisema wakijituma vizuri kwenye uchumi wa viwanda kwa kuimarisha kilimo na kuhifadhi chakula badala ya kufanya biashara, wataona kuna tija na kuwaondoa katika kilimo cha kimaskini.

Awali, Mkurugenzi wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi, alisema wameamua kuwapa vyeti vya heshima mapema wajumbe hao baada ya kuonyesha nia na hali ya kujituma kijasiriamali na kilimo kufikia uchumi wa viwanda.

Alisema mpango wao wa maendeleo wa miaka mitano unazungumzia kilimo na viwanda na kwamba matamanio yake ni kuwaona wanabadilika na kuendana na mpango huo zaidi.

Meneja uendeshaji na ubunifu kutoka SUGECO, Joseph Massimba, alisema ajenda kuu katika mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo waweze kuibua, kuandaa, kuanzisha na kuendesha kwa ufanisi miradi ya kiuchumi itakayochangia kuleta kipato ikiwa ni pamoja na kurudisha maarifa wanayopata kwa jamii wanayotoka na kuwa na mtazamo chanya.

# Ramani mpya Tanzania kutengenezwa kisasa

**Na Romana Mallya**

HATIMAYE ramani mpya ya Tanzania itatengenezwa kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya setalaiti ambayo itawezesha kupima, kupanga, kumilikisha na kutoa hati miliki za ardhi mijini na vijijini.

Hayo yalisemwa juzi jioni jijini Dar es Salaam na Mratibu wa Mradi wa Takwimu za Ardhi na Miundombinu kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Eric Mwaikambo.

Dk. Mwaikambo alisema hayo katika mkutano wa siku mbili wa 'Geospatial Information Road Show' ambayo ni teknolojia ya kupima taarifa za ardhi.

Mkutano huo ulishirikisha zaidi ya maofisa wa serikali 200 na wataalamu wa fani hiyo kutoka Tanzania na kampuni kubwa 12 za Korea Kusini.

Alisema utekelezaji wa mradi huo utakapoanza utashirikisha wataalamu wa Korea Kusini na Tanzania na baada ya wazawa kuuelewa wataendelea kwenye maeneo mengine ya nchi.

Alisema kwa kuanza utakwenda kutengeneza ramani za msingi nchi nzima zikiwamo za uwiano mkubwa zitakazotengenezwa katika miji mikuu 26 ya mikoa.

"Hii itasaidia urasilimishaji na kupunguza uhaba wa viwanja vilivyopangwa na kupimwa mjini, itasaidia katika shughuli za sensa ya makazi," alisema.

Pia alisema ramani za msingi za uwiano zimelenga matumizi makubwa kuwezesha kupima, kupanga, kumilikisha na kutoa hati miliki.

Alisema ramani za uwiano mdogo zitasaidia kupanga ardhi vijijini kwa kuyapima mashamba na kutoa hati miliki za kimila.

Dk. Mwaikambo alisema mradi huo utaiwezesha Tanzania kubadili ramani iliyopo ambayo ilitengenezwa kwa mfumo wa karatasi na sasa kuwa ya kielektroniki ambayo itarahisisha shughuli mbalimbali.

Alisema mradi huo kwa sasa upo katika hatua ya mwisho za maandalizi na unatarajiwa kuanza mapema mwakani.

Alisema unaweka miundombinu ya kurahisisha upimaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya satelaiti ambapo vitafungwa vifaa vya kielektroniki miji 26.

Balozi wa Korea Kusini nchini, Tae Ick Cho, alisema teknolojia bora katika kukuza uchumi ndiyo silaha kubwa na pekee ya kimaendeleo na yenye kuleta ushindani katika soko la dunia.

Alisema hilo litafanikiwa endapo taifa litajikita zaidi katika kuwekeza zaidi katika teknolojia ya sasa ambayo imeteka soko la dunia kwa sasa.

Naye Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani kutoka Wizara ya Ardhi, Hamdouny Mansour, ambaye alimwakilisha waziri wa wizara hiyo, William Lukuvi, alisema ushirikiano kati nchi hizo ni wa kindugu na kupitia Geospatial Information Road Show wataendelea kupeana taarifa za kisekta ili kufikia malengo waliyojiwekea.

# Mbao zakamatwa zikisafirishwa nje

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

VIKOSI vya ulinzi na usalama Mkoa wa Kaskazini Pemba vimefanikiwa kukamata mbao 200, zenye thamani ya zaidi Sh. 4,000,000 Chanjaani Mtambwe ambazo zilikuwa zinataka kusafirishwa nje ya kisiwa hicho.

Akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama, Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Hemed Suleiman Abdalla, alivipongeza vikosi hivyo na kuwataka kuendelea kufanya kazi bila ya woga.

Alivitaka vikosi hivyo kuendelea kufanya kazi kwa moyo wa imani, kwani hilo ndilo jukumu walilopewa na serikali, hivyo ni wajibu wao kuwafichua wale wote ambao wanavunja sheria na kuwafikisha kwenye vyombo husika.

"Natoa agizo kuanzia sasa magari yote makubwa ambayo yanamilikiwa na kampuni za meli yafanyiwe ukaguzi ili kijulikane kilichomo ndani na ndio baadaye yaruhusiwe," alisema Hemed.

Aliviagiza vikosi hivyo kuendelea kuwatafuta watuhumiwa wote waliohusika na vitendo hivyo ili wachukuliwe hatua za kisheria.

Pia Wizara ya Kilimo ijue kuwa hili sio la vikosi pekee bali ni letu sote, hivyo tuendelee kushirikiana katika kupiga vita huu uharibifu wa mazingira, ambao unafanywa na baadhi ya wananchi wasioipendelea mema nchi yetu," alisema. Naye ofisa kutoka Idara ya Misitu na Mali zisizorejesheka, Mussa Said Bakar, alieleza kuwa mbao hizo zimekatwa sehemu ambazo kuna kamati maalum ya uhifadhi wa mazingira za wilaya.

# 'Mitandao kijamii itumike kiuchumi'

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Intanenti Tanzania (ISOC) kimesema kutokana na mabadiliko ya teknolojia katika mitandao ya jamii, kunahitaji kuangalia namna vijana wanavyotumia mitandao hiyo katika manufaa ya kiuchumi.

Kauli hiyo ilitolewa jijini Dar es Salaam na Rais wa ISOC Tanzania, Nazarius Kirama, baada ya kutembelewa na kufanya mazungumzo na Meneja wa Mahusiano ya Jamii Afrika, Victor Ndonnanga.

Alisema kundi la vijana ndilo linatumia kwa kiwango kikubwa mitandao hiyo, na kwamba kuna umuhimu wa kutumia mitandao hiyo kwa faida kupitia fursa za kibiashara na si vinginevyo. Alisema matumizi ya mitandao ya jamii imekuwa ikitumika vibaya kwa baadhi ya watu kwa kutuma vitu visivyo na maadili na manufaa kwa jamii na wakati mwingine kuchangia kuwaharibu vijana hao kuiga vitu visivyo na manufaa kwao.

Alisema ISOC ina mpango wa kuanzisha mpango wa kuzunguka nchi nzima kuanzia mwakani kuwaelimisha vijana namna ya kutumia mitandao hiyo kwa faida za kujiongezea kipato na si kwa matumizi ya kutumia vibaya.

"Sasa hivi kuna sheria ya makosa ya mtandao inayowabana wale wote wanaotumia vibaya mitandao ya kijamii, kwa hiyo sisi tumejipanga kwamba tuanze mapema kuwafundisha vijana hawa kabla hawajakumbwa na mkono wa sheria," alisema Kirama.

Alisema matumizi mabaya ya mitandao ya jamii yanachangia baadhi ya vijana kukosa sifa za kuajirika na hivyo kuongeza idadi ya wasio na ajira. Pia alitoa wito kwa wanawake kutumia mitandao hiyo katika kutangaza biashara zao badala ya kutangaza maovu.

# Pinda atoa neno mataifa kuadhimisha siku katiba

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema wakati mataifa yakiadhimisha siku za katiba, ni muhimu kutafakari na kuzitumia hekima zilizoachwa na waasisi wa bara hilo ili kuubadilisha ulimwengu.

Pinda aliyasema hayo juzi jioni wakati Ubalozi wa India nchini ukiungana na nchi yao kusherehekea Siku ya Katiba yao iliyotimiza miaka 70. Alisema wakati India ikisherehekea miaka 70 ya Katiba, wananchi wake pamoja na wa Bara la Afrika wana jukumu la kurekebisha utaratibu wa dunia. "Ni jukumu la mabilioni ya watu kutoka India na wa Bara la Afrika kuubadilisha utaratibu wa ulimwengu.

"Siku kama hii, ' Siku ya Katiba' ni fursa muhimu ya kutafakari yaliyofanywa na waasisi," alisema. Alisema India na Tanzania walianzisha mahusiano ya kihistoria kabla ya mwaka 1961 na kuwa na uhusiano wa kidiplomasia ulioasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na Hayati Mahtma Gandhi ambaye ni Baba wa Taifa hilo.

Aidha, Pinda alisema amekubali mwaliko huko kwa sababu anaamini India imedhamiria kulinda maadili ya ujamaa na kuheshimu nguzo za demokrasia ya Katiba yao.

Alisema mwenendo wa kiuchumi kati ya nchi hizo mbili umeongeza uhusiano katika sekta mbalimbali zikiwamo elimu, kilimo, maji, utalii, teknolojia na afya.

Naye Balozi wa India nchini, Sanjiv Kohli, alisema serikali yao imekuwa imara na kuwa na wananchi wanaoelewana kwa sababu ya kuheshimu demokrasia na haki za binadamu.

Kohli alisema katika miaka yote imekuwa yenye manufaa kwa sababu Katiba imempa raia haki ya kuchagua viongozi kidemokrasia na kuheshimu haki za binadamu. Alisema katika miaka yote India ni rafiki mkubwa Tanzania kwa sababu wanashabihiana mambo mengi katika kulinda demokrasia na haki za binadamu.



Ofisa wa Jeshi la Polisi Kamishna Msaidizi wa Polisi, Fatuma Mtambo, akitoa mada kuhusu ukatili wa kijinsia kwa wafanyakazi wa kiwanda cha Tanzania Distilleries Limited (TDL) jijini Dar es Salaam jana, yakiwa ni maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia. Kampuni ya TBL Group inashiriki katika kampeni za kutokomeza vitendo hivyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# H'shauri Nzega yakusanya mil. 345/-

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

HALMASHAURI ya Mji wa Nzega imekusanya zaidi ya Sh. milioni 345 kutoka mapato ya ndani katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Philemon Magessa, alitoa taarifa hiyo wakati wa kikao cha robo ya kwanza ya Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema kiasi hicho ni sawa na asilimia 17.26 ya makisio ya kukusanya Sh. bilioni 1.999 ndani ya mwaka huu wa fedha.

Hata hivyo, alisema uelewa mdogo wa baadhi ya wafanyabiashara katika ulipaji kodi na ukwepaji wa ulipaji tozo mbalimbali umesababisha kasi ndogo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Katika kukabiliana na tatizo hilo, alisema wameamua kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulipaji kodi na kuendelea kutumia vikosi kazi katika ukusanyaji wa mapato.

Magesa alisema pia wanawafikisha kwenye vyombo vya sheria wadaiwa sugu wa kodi mbalimbali.

Katika hatua nyingine Halmashauri ya Mji wa Nzega imetenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya ununuzi wa gari ambalo litatumika kukusanya taka katika maeneo mbalimbali.

Magesa alisema halmashauri hiyo inazalisha taka ngumu tani 1,200 kwa mwezi na uwezo wa kuziondoa ni tani 1,035 ambayo ni sawa na asilimia 86.25.

Alisema katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, mwaka huu, taka ngumu zilizozalishwa ni tani 3,600 na tani 3,050 sawa na asilimia 84.7 zilipelekwa kwenye shimo la taka.

Magesa alisema kutokana na hali hiyo wameamua kutenga kila mwezi fedha ili hatimaye waweze kununua gari ambalo litasaidia kufikia asilimia 100 ya uondoaji wa taka hizo.

Kadhalika, alisema halmashauri imeendelea kusimamia usafi wa mazingira kwa kuwa na utaratibu wa kufanya usafi kila Alhamisi ya wiki na Jumamosi ya mwisho mwa mwezi.

# DC ajifagilia ujenzi wa madarasa

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amesema kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi kwenye wilaya hiyo, amejenga madarasa 149 ya shule za msingi na sekondari katika halmashauri mbili za Arusha DC na Meru.

Akizungumza na wanahabari, Muro alisema Wilaya ya Arumeru ina Halmashauri mbili za Arusha DC na Meru DC zenye jumla ya tarafa sita, kata 53 na majimbo mawili ya uchaguzi ambayo ni Arumeru Mashariki na Magharibi.

Alisema kampeni aliyoianzisha mwanzoni mwa mwaka huu ya ujenzi wa madarasa, amefanikikiwa kujenga madarasa 149, ambayo yamegharimu Sh. bilioni mbili.

"Ndugu waandishi wa habari leo nimeona niwaletee mrejesho wa kampe ya ujenzi wa madarasa niliyoianzisha mwanzoni mwa mwaka huu, kuwaeleza tumefikia wapi," alisema Muro.

Aliema katika Halmashauri ya Meru wamejenga vyumba 35 vya madarasa ya shule za msingi na sekondari vyote vipo hatua za mwisho kukamilika.

Kati ya vyumba hivyo, 42 ni vya shule ya sekondari na idadi iliyobaki ni vya shule ya msingi, na vipo kwenye hatua za mwisho kukamilika.

Pia alisema wamejenga majengo mawili ya utawala ambayo yapo katika hatua za mwisho kukamilika pamoja na ujenzi maabara mbili za sayansi sambamba ujenzi wa jengo jipya na la kisasa la wadhibiti ubora wa elimu.

Katika Halmashauri ya Meru, alisema wamejenga vyumba na majengo 82, na Halmashauri ya Arusha DC, wamejenga madarasa 34 yaliyokamilika na yameshaanza kutumiwa.

Alisema madarasa ya shule za sekondari na msingi yaliyopo katika hatua ya mwisho kukamilika ni madarasa 73, ambayo yapo kwenye Halmashauri ya Arusha DC. Kwa mujibu wa Muro, kupitia kampeni hiyo kwenye wilaya hizo, wameshajenga vyumba vya madarasa 107 kwa shule za msingi na sekondari.

Aidha, Muro alisema kampeni hiyo imewapa fursa ya kujenga vyumba 149, na lengo la serikali ilikuwa wajenge vyumba 107, hivyo alisema wamevuka lengo walilojiwekea.

Kuhusu uandikishaji wa wanafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza, alisema katika wilaya hiyo, idadi imeongezeka kwa asilimia 100.




Balozi wa Jumuiya ya Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, kabla ya kutiliana saini mkataba wa msaada wa fedha kiasi cha Euro milioni 10 na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Liberat Mfumukeko (wa pili kulia), jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wamwomba RC kukamilisha ujenzi

**Na Allan Isack,** BABATI

WAKAZI wa Kijiji cha Himiti, Kata ya Bonga Halmashauri ya Mji wa Babati, mkoani Manyara, wamemwomba Mkuu wa Mkoa huo, Alexander Mnyeti, kuwasaidia kumalizia ujenzi wa miundombinu ya zahanati ili ianze kutoa huduma kwa wananchi.

Ombi hilo, walilitoa juzi wakati wa ziara ya kikazi ya Mkuu huyo wa Mkoa kukagua miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi wa eneo hilo na kuzitatua. Mmoja wa wananchi hao, Hamis Juma, alisema serikali ilipoanzisha mpango wa kujenga zahanati kila kijiji wananchi hao waliitikia wito huo kwa kufahamu umuhimu wa kupata zahanati katika eneo hilo.

Juma alisema wameiunga mkono serikali kwa kuchangia ujenzi wa zahanati hiyo ili kupata huduma hiyo karibu na kuepuka kutembea umbali mrefu.

Salma Mohamed, alisema zahanati hiyo walianza kujenga mwaka 2009 na mpaka sasa haijafunguliwa wala haina miundombinu ambayo inaonyesha dalili ya kufunguliwa kwa siku za karibuni.

"Kero hii inatusumbua muda mrefu, zahanati tunayo ila imebaki gofu, kinamama tunadhalilika kwani tunajifungulia kwenye bajaji wadogo, tunaomba Mkuu wa Mkoa uangalie jambo hili na mtuwekewe umeme," alisema Mohammed.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Dk. Damas Kayera, alithibitisha kuwa zahanati hiyo imejengwa muda mrefu uliopita, na wananchi walifanya bidii ya ujenzi kwa kushirikiana na halmashauri, lakini bado kuna mapungufu madogo ya kurekebisha.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo, timu ya mkoa ilifika eneo hilo, mwezi Aprili na kukagua zahanati hiyo, kama itaweza kutoa huduma na walibaini kuwa kuna matatizo ya ukosefu wa maji, umeme na shimo la kuweka kondo la nyumba.

Mkurugenzi wa Mji wa Babati, Fortunatus Fwema, alisema wanasubiri maombi ya Tamisemi ili kukamilisha ujenzi na kuanza kutibu wagonjwa.

"Tumepeleka maombi mkoani, wametusaidie kufikisha Tamisemi ili waruhusu mfumo wa kutoa fedha kwa hiyo wakitoa tu hata kesho tunaanza mchakato wa ujenzi," alisema Fwema.

Hata hivyo, Mnyeti aliwaambia wananchi hao, amesikia kilio chao, na kabla mwaka haujaisha, zahanati hiyo itaanza kufanya kazi.

Aliwapongeza wananchi hao kwa kuchangia maendeleo na kwamba serikali iliwaunga mkono kwani awali walichanga Sh. milioni 16 na serikali ilitoa Sh. milioni.

## Wananchi wawapa tano trafiki

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WAKAZI wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wamewapongeza askari Polisi wa Kikosi cha Usalama Barabarani kwa kupunguza ajali.

Wamedai mafanikio hayo yametokana na askari hao kutowabugudhi watumiaji wa vyombo vya moto hususan waendesha bodaboda.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao walidai askari hao wamekuwa wakitoa elimu ya usalama barabarani bila kuwakamata madereva ovyo kwa ajili ya kujipatia fedha.

Mmoja kati ya madereva wa bodaboda, Ally Juma, alisema askari wa usalama barabarani hawawanyanyasi wala kuomba rushwa kama awali.

"Miaka iliyopita kipindi kama hiki cha mwishoni mwa mwaka huwa tunasumbuliwa kwa kuombwa rushwa za sikukuu, lakini sasa wanafanya kazi ya kutoa elimu ya usalama barabarani ili kupunguza ajali," alisema.

Alisema askari wa usalama barabarani wa eneo hilo sasa hawaonei watu na kama mtu akikamatwa anakuwa na kosa linalostahili adhabu.

Mkazi wa Mji Mdogo wa Mirerani, Nyinda Baruti, alisema askari hao wanapaswa kupongezwa kwa namna wanavyofanya kazi zao tofauti na miaka iliyopita.

"Mkuu wa Askari Kikosi cha Usalama Barabarani wa Wilaya ya Simanjiro, Nicolaus Mushi, anastahili pongezi kwa namna vijana wake wanavyofanya kazi ya usalama barabarani," alisema Baruti.

Alisema trafiki wa maeneo mengine wanapaswa kuiga wa Mirerani ambao wanatoa elimu kuliko kukamata ovyo pikipiki za watu kwa makosa ambayo hayana maana.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Agostino Senga, alisema askari wa kikosi hicho wanatekeleza wajibu wao kuhakikisha ajali zinapungua au kumalizika.

Senga alisema elimu imeendelea kutolewa kwa askari hao ili wawatumikie watumiaji wa barabara.

"Hivi sasa mambo yamebadilika kwa hiyo hata askari wetu nao wamebadilika, kwa kutimiza wajibu wao kwa wadau wa barabara, ndiyo maana unasikia pongezi hizo," alisema.

# Wakulima kanda ya kaskazini wafundishwa kutambua udongo

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

WAKULIMA wa mpunga, mahindi na vitunguu mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara wamepongeza juhudi za Kampuni ya Mbolea ya Yara Tanzania kutoa elimu ya upimaji udongo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao hayo.

Hayo yalibainika hivi karibuni wakati wa mahojiano na wakulima wa mikoa hiyo, katika ziara ya waandishi wa habari kujifunza namna mbolea ya Yara inavyotumiwa na wakulima.

Walisema elimu hiyo inawawezesha kufahamu aina ya udongo na mazao wanayopaswa kupanda, tofauti na awali walifanya kwa mazoea.

"Uzalishaji wa mazao na hasa zao la mpunga hapa Moshi limeongezeka baada ya kuweka kwenye utekelezaji elimu tuliyopewa," alisema Ikunda Joseph, mkulima anayejihusisha na kilimo cha mpunga na vitunguu.

Alisema kampuni hiyo imesambaza maofisa ugani wanaotoa elimu kwa wakulima ikiwamo kujua aina ya mbolea, ambayo wanapaswa kuiweka kwenye vitendo na kuonyesha mabadiliko.

"Tumenufaika kwa kiasi kikubwa na elimu inayotelewa, wamekuwa wakitoa elimu na kuhamasisha kuhusu umuhimu wa kupima afya ya udongo na kwa hakika tumeanza kuona faida yake," alisema Jonathan Mjema mkulima wa mpunga kwa zaidi ya miaka 20.

Mjema alieleza faida za elimu hiyo kuwa inamwezesha mkulima kutambua aina ya udongo na zao ambalo linapaswa kulimwa katika eneo husika.

"Upimaji wa afya ya udongo inatuwezesha wakulima kutambua zao gani linafaa katika maeneo yetu ya uzalishaji, elimu hiyo imetufanya tutoke kwenye kilimo cha mazoea na sasa tumeongeza uzalishaji kwa zaidi ya mara mbili tofauti na hapo awali," alieleza.

Mjema aliiomba kampuni kwa kushirikiana na wadau wengine kwenye sekta ya kilimo kuendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kumkwamua kutoka kwenye kilimo cha mazoea na kujikita katika kilimo biashara hali itakayochochea ukuaji wa uchumi.

Naye mkulima wa mahindi na vitunguu Aikael Laswai, alisema kwa zaidi ya miaka 10 amenufaika na elimu hiyo ikiwamo namna sahihi ya kutumia mbolea.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Salum Hamdun, akizungumza na wadau wa utalii wa Mkoa wa Kilimanjaro, katika kikao kilichofanyika katika Hoteli ya Salsarenero jana, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kuanza kwa msimu wa utalii. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Vijana Same watakiwa kujifunza Tehama

**Mary Mosha,** SAME

VIJANA wilayani Same mkoani Kilimanjaro wametakiwa kujifunza Tehama, itakayowasaidia kutumia vyema teknolojia kuleta mabadiliko kwenye maisha yao.

Akizungumza jana na gazeti hili wilayani humo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Sinyamule, alisema elimu hiyo ni muhimu kwa kuwa ndiyo njia bora zitakazotumika kuwakomboa vijana kwenye ulimwengu wa utandawazi.

Alisema mabadiliko ya utandawazi yanakuja kwa kasi, na kwamba lazima kuelimisha vijana namna ya kukabiliana nayo na kuwa na uelewa chanya.

"Katika wilaya yetu tunavijana wanapata changamoto kubwa ya matumizi ya mitandao mfano mikopo ya elimu ya juu (HESLB). Tumeanzisha uhamasishaji maalum wa matumizi bora ya mtandao ili kuingia kwenye soko la ajira kidunia," alisema na kuongeza:

"Siku za hivi karibuni tumepokea mifuko 100 kutoka kwa wahisani wetu wa benki ya Posta (TPB) ambayo itawasaidia shirika binafsi (compassion) kuanzisha kituo cha Tehama chenye wataalamu kitakachowasaidia vijana kupata elimu."

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Daniel Malonga, alisema msaada wa saruji walizopata utawasaidia kukamilisha ujenzi wa maabara hiyo itakayowasaidia vijana kuleta mabadiliko.

"Katika kituo chetu tunakabiliana na changamoto ya ukosefu wa maabara ya kompyuta ambayo tunatarajia ianza mapema mwezi huu na kukamilika mwishoni mwa mwaka huu," alisema Danieli.

Naye Mwenyekiti wa kamati ya ujenzi ya kituo, Marunda Michael, alisema ujenzi huo umekamilika kwa asilimia 80 na kuiomba serikali kuendelea kuwapa ushirikiano ili waweze kuwasaidia vijana wilayani humo.

# Vijana kutoka Afrika kupanda M/Kilimanjaro

**Na Zanura Mollel**
KILIMANJARO

WADAU wa mashirika binafsi yanayojihusisha na masuala ya vijana kutoka nchi za Zimbabwe, Uganda na Tanzania wameanza kupanda Mlima Kilimanjaro kwa lengo la kuongeza idadi ya kundi hilo kufikia nchi 55 za Afrika kupanda mlima huo, ifikapo Mei 2020.

Kiongozi wa timu ya vijana hao kutoka Tanzania, Emanuel Motta wa kutoka kampuni ya Origin Trails, alisema lengo ni kufika kilele cha mlima huo na kutimiza azima ya kuhakikisha kila kijana kutoka nchi za Afrika anapanda mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika.

Aidha, alisema kuwa vijana kutoka nchi za Afrika wanatarajia kupanda mlima huo wakifikisha ujumbe wa Afrika tunayoitaka na utekelezaji wake, huku wengine wakiwa na mabango maalumu yaliyochorwa kwa usanifu unaoonyesha Afrika tunayoitaka.

Naye Mkurugenzi wa Great Africa Art Banner kutoka Zimbabwe, Munyaradzi Muzenda, alisema kwa mara ya kwanza vijana kutoka nchi zote za Afrika watapanda mlima huo katika maadhimisho ya Siku ya Umoja wa Afrika Mei 2020, kama ishara ya kuunganisha bara la Afrika na kudumisha umoja.

"Tunatarajia kuwa na idadi kubwa ya vijana watakaopanda mlima mwakani Mlima Kilimanjaro utatumika kama nyezo ya kuliunganisha bara la Afrika kwa vijana kuungana kuwa na sauti moja, nguvu moja katika kusukuma gurudumu la maendeleo na kuhakikisha amani na mshikamano katika bara hili," Alisema Munya.

Mwakilishi kutoka Shirika la Sister Sister Organization lililopo nchini Uganda, Ayaa Musuya, alisema tayari wameanza kampeni ya kuhamasisha vijana kupanda mlima huo kupitia mitandao ya kijamii na kuwasajili kwa ajili ya zoezi hilo ambalo litaambatana na mashindano ya sanaa kwa vijana ya kuchora bango lenye picha ya Afrika tunayoitaka.

Kwa mujibu wa Ayaa, washindi watakaoibuka katika mashindano hayo wataungana na waliojisajili kupanda mlima huo na kupeleka bango litakaloshinda la Afrika tunayoitaka katika kilele cha Mlima Kilimanjaro.

ama
ALHAMISI NOVEMBA 28, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Mgonjwa atolewa figo nzito kupindukia**



Ukurasa 18

Simulizi ya utitiri mimba kijijini mabinti sekondari waishio 'geto'



Ukurasa 17

**Chanjo inavyohamisha afya kutoka shida hadi ubora**



# Mazito yasiyo mfano ukeketaji uliojikita kwa wafugaji Longido

Ukurasa 14



Upasuaji wa mgonjwa mwenye figo kubwa ulipofanyika. **PICHA: MTANDAO.**

## Mgonjwa atolewa figo nzito kupindukia

**New Delhi,** INDIA

MADAKTARI nchini hapa wamemfanyia upasuaji mgonjwa na kutoa figo kubwa la aina yake, ikiwa na uzito wastani wa kilo 7.4, ambao wanaufafanisha sawa na uzani wa watoto wawili wachanga waliozaliwa.

Kwa mujibu wa vyombo vya afya nchini hapa, hiyo inavunja rekodi ya figo kubwa kutolewa kwa mgonjwa. Kwa kawaida figo hilo huwa na uzito kati ya gramu 120 hadi 150, hivyo rekodi hiyo ya figo ni uzito wastani mara 50 ya ilivyozoeleka.

Daktari aliyehusika katika oparesheni ya kutoa figo hiyo, anasema ugonjwa wa figo uliosababisha kufanyika oparesheni unaitwa 'autosomal dominant polycystic' mara nyingi wagonjwa wanakutwa na figo kubwa.

Dk. Sachin Kathuria, kutoka Hospitali ya Sir Ganga Ram ya mjini hapa, anasema figo haitolewi, isipokuwa pale inapoonekana kupata maambukizo.

"Mgonjwa huyu alikumbwa na athari na maambukizi mabaya ambayo yalikuwa yanagomea dawa za antibaiotiki na figo kubwa ilimpa tabu mgonjwa kupumua, hivyo hatukuwa na mbadala, zaidi ya kuiondoa," anasema.

Dk. Kathuria anaongeza kwamba pamoja na wao matabibu kugundua kuwapo figo kubwa, lakini bado ukubwa waliokutana nacho baada ya upasuaji, umewashanghaza, ni zaidi ya matarajio.

AFYA

# Mazito yasiyo mfano ukeketaji uliojikita kwa wafugaji Longido

• Ngariba mstaafu aanika shida kuu • Simulizi mkasa wa kimila hadi kifo • Mganga amkeketa mjamzito mara tatu • Hospitali kwa amri Polisi; nusu waendao walikeketwa



Wanafunzi wa Shule ya Wasichana Lekule, katika Kata ya Lumbwa, Longido wakiimba nyimbo zenye maudhui ya kukemea ukeketaji na ndoa za utotoni, kwenye mahafali ya tano ya kidato cha nne mwaka huu.

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

MSINGI wa ukeketaji ni tendo linalohusu kuondoa viungo vya uzazi kwa mwanamke, lengo ni kuwapunguzia hamasa ya tendo la ndoa, kwa imani inajengea uaminifu kwa waume zao.

Keketa ni neno ambalo mzizi wake uko katika msamiati unaobeba maana kuharibu. Hivyo, inapotamkwa 'kukeketa' ni ukatili dhidi ya mwili wake.

Wanawake wengi duniani waliokeketwa, hawakuwa tayari kufanyiwa kitendo hicho, lakini kutokana na mila na desturi za makabila yao, hawakuwa na namna ya kuchukua hatua vinginevyo. Ni hali inayochangia wanawake kujiona hawana thamani duniani.

### KEKETA VS TOHARA

Hata hivyo, katika uhusiano wa kijinsia kuna mgongano baina ya maneno 'ukeketaji' na 'tohara.' Sehemu kubwa ya umma duniani wanashindwa kutofautisha maneno hayo na kushindwa kubainisha namna yanavyotumika. Ukeketaji unafanyika kwa wanawake na tohara kwa wanaume.

Ni maeneo ambayo yana maana sawa katika tafsiri tofauti, yakibeba ujumbe wa kuondoa viungo vya uzazi vya mwanamke na mwanaume.

Kiafya, si sahihi kuondoa kiungo cha mwanamke, kwani inamwachia kovu ambalo kila anapofanya tendo la ndoa anahisi maumivu makali, badala ya kinyume chake. Hiyo inaenda mbali ikiwamo kujifungua.

Tohara kwa wanaume inatajwa katika sura moja ni tendo la kimani, pia katika mustakabali wa kawaida wanaume waliofanyiwa tohara hufurahia zaidi tendo la ndoa, kuliko ambao hawajafanyiwa.

> **Jamii ya Kimasai inaamini ili mtoto wa kike aolewe, ni lazima afanyiwe ukeketaji, lakini sasa amebaini ni dhambi na ukatili kwa mtoto wa kike.**

### SHIDA MILA

Mila za baadhi ya makabila na hasa jamii za wafugaji, wakiwamo Wamasai waliotawanyika sana ukanda wa Kaskazini na kwingineko nchini, wakiwa na ngome mkoani Arusha, wanadaiwa kuwa mstari wa mbele kwa ukeketaji, hususani zikitajwa wilaya za Monduli, Ngorongoro na Longido.

Ndani ya Longido kwenye jumla ya vijiji 49, kata 18 na tarafa nne, asilimia 95 ya jamii ya wakazi ni wafugaji, huku asilimia tano waliobaki wako katika kilimo, na biashara, baadhi yao ni waajiriwa kwa mujibu wa uongozi wa wilaya.

### HARAKATI ZILIVYO

Bado ukeketaji kwa wanawake unaendelea kutokana na mila na desturi kandamizi, huku jamii inaelezwa kusuasua kukubali haja ya kuachana nayo, eneo baya zaidi inatajwa kuendekeza ukeketaji, ambayo katika sura ya pili, kuna vita vikali vya kuipinga.

Nipashe imebaini kwamba katika kuhofia mikono ya sheria, wakazi wake sasa wanawakeketa watoto wachanga, kukwepa mikono ya sheria serikalini na wanaharakati, wanajamii na wanaopinga vitendo hivyo.

Mbinu za wanaopinga ukeketaji, hujielekeza kupambana na wazazi, pia mangariba wanaojihusisha na ukeketaji kwa watoto na jamii zao, jambo linalofanya makundi hayo mawili yanayokinzana yaishi kwa kuwindana.

Maeneo ya Longido yanayotajwa kukithiri tabia hizo ni Tarafa za Kitumbieine, Enduiment na Engarenaibor, huku kata sugu zikiwa ni; Nondoto, Olmolog, Sinya, Lang'atadapash Gelaymerugoi.

Ofisa Ustawi wa Jamii, katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Atuganile Chisunga, anasema kikwazo kikubwa katika ufuatiliaji na udhibiti matukio ya ukeketaji kwa mtoto wa kike, ni kukosekana ushirikiano wakati wa kuwasaka mangariba na wazazi wanaoshinikiza kitendo hicho.

Mratibu wa Kitengo cha Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto katika Hospitali ya Wilaya Longido, Yosiah Mruve, anasema mwaka jana, nusu ya wajawazito waliofika hospitalini kujifungua waligundulika wamekeketwa.

Yosiah anainisha takwimu hizo za mwaka 2018, kwamba jumla ya kinamama waliofika kujifungua walikuwa 2160, kati yao waliobainika kukeketwa ni kinamama 1,144 sawa na asilimia 52.9

### MZEE WA MILA

Mzee wa mila katika Tarafa ya Longido, Thomas Ole Ngulupa, anaeleza ukeketaji wa mabinti uko chini ya kinamama katika jamii yao ya Kimasai, akikana wanaume wa jamii za kifugaji hawajui siri iliyoko katika ukeketaji na hawashirikishwi kwa chochote.

Anasema, dai la kimila lililopo ni kwamba mtoto wa kike anapokeketwa, ni tendo linalomvusha kufikia utu uzima. Hata hivyo, anakiri baada ya kelele na sheria za serikali, wazee wa mila waliamua kuungana na kuwataka kinamama wa jamii hiyo, waache vitendo hivyo vinavyoangukia kundi

AFYA

# Mazito yasiyo mfano ukeketaji uliojikita kwa wafugaji Longido

la ukatili kwa wanawake.

Ole Ngulupa anakiri, baada ya hatua hiyo, sasa ukeketaji umepungua na wameweka taratibu za sherehe za kuwavusha watoto rika pasipo kukeketwa, kama ilivyokuwa zamani.

**MKASA UNAOSIKITISHA**

Mnamo Januari 8 mwaka jana, katika kijiji cha Nondoto binti (jina lake tunalo) aliyekuwa na ujauzito wa miezi saba, hakuwa amefanyiwa kitendo cha ukeketaji.

Hata hivyo, mila na desturi za jamii ya Kimasai, zinamlazimisha afanyiwe ukeketeji na baada ya tendo hilo, hakupona, kutokana na majeraha katika sehemu za siri.

Binti huyo anaeleza, alimtaarifu mzazi wake na wakaamuru afanyiwe ukeketeji kwa mara ya pili, wakidai kapatwa na ugonjwa unaoitwa 'kilawalawa.'

Wazazi hao walichukua hatua ya kumpeleka binti huyo kwa mganga wa kienyeji tena, aliyeeleza hayo ni maradhi ya kansa, hivyo ni lazima akeketwe tena kwa mara ya tatu na ukafanyika.

Hiyo nayo iliishia binti kupatwa na maumivu makali yaliyoambatana na kidonda kikubwa sugu. Inaelezwa wakati wote wa msukosuko huo, wazazi hao walikua wakimtibu binti kwa dawa ya kienyeji na baada ya wazazi kuona hali ni mbaya haponi, ndipo wakampeleka hospitali.

Ananukuliwa maelezo yake, kwamba huko alipewa tiba ya vidonge na kutakiwa kutumia sabuni yenye dawa na alitekeleza, lakini hali yake ilizidi kuwa mbaya.

Dk. Elifurahi Urio, ni Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya Longido, alithibitisha kumpokea binti huyo na alitibiwa siku mbili na hali yake ilipozidi kuwa mbaya, ikiwamo alichokitamka "kutosikika kama mtoto anacheza tumboni kwani alikua na ujauzito wa miezi saba."

Anasema walichukua hatua ya kumpatia mgonjwa huyo uhamisho kwenda Hospitali ya Rufani Mkoa wa Arusha -Mount Meru. Mwisho wa simulizi ilishia mzazi huyo kupoteza maisha na mtoto alipona.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Longido, Atunagile Chisunga, anasema, hata wakati wa kumchukua binti huyo kwenda kumtibu, walinyimwa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa serikali za mitaa na walitishwa kupigwa na vijana Morani wa Kimasai.

Anaeleza mafanikio yalipatikana kupitia Jeshi la Polisi wilayani humo, walipomchukua binti huyo mjamzito na wakamfikisha katika Kituo cha Afya Longido, kulikoanza taratibu za matibabu.

Ofisa Ustawi Jamii, anasema aliendelea kufuatilia hali ya binti huyo hadi alipopokea taarifa ya kifo chake, akiacha mtoto mchanga wa kike. Hivi sasa mtoto huyo analelewa na kituo cha malezi kilichopo jijini Arusha, tangu mwezi Februari mwaka huu.



Ofisa wa Shirika la Tembo Trust, akizungumzia kuwanyima wajawazito mlo sahihi kunavyosababisha utapiamlo wilayani Longido, Arusha. **PICHA: MTANDAO.**

> "Nimefanya kazi hii kwa muda mrefu, ni kazi inayohitaji mtu mwenye roho ngumu na asiyeogopa, lakini kwa sasa nimeacha.

**NGARIBA**

Ngariba mkongwe aliyestaafu kazi hiyo, Nalepo Laizer, anasema jamii ya Kimasai inaamini ili mtoto wa kike aolewe, ni lazima afanyiwe ukeketaji, lakini sasa amebaini ni dhambi na ukatili kwa mtoto wa kike.

Mama huyo anatoa mfano wa uzoefu wake, aliwahi kumkeketa binti mmoja aliyetokwa damu nyingi na ilishindikana kupelekwa hospitali kwa kuogopa mikono ya kisheria na hadi sasa binti hajapata mtoto.

"Nimefanya kazi hii kwa muda mrefu, ni kazi inayohitaji mtu mwenye roho ngumu na asiyeogopa, lakini kwa sasa nimeacha," anasema na kufafanua alikosimamia: "Mimi nilikua ngariba kweli kweli, lakini watoto wangu wa kike sijawakeketa."

Anafafanua kinachoteka msimamo wa jamii ya Kimasai, ni kwamba ukeketaji unabeba imani kubwa kwamba binti atapata mume. Huadhimishwa kwa sherehe kubwa ya kimila na ishara kwa binti ni kwamba anavalishwa kaniki.

Kuhusu ukeketaji watoto wachanga, ni matokeo ya kuogopa mikono ya kisheria. Ngariba huyo mstaafu anaiasa serikali kupitia vyombo vyenye mamlaka kuwa utaratibu wa kuwakagua watoto wachanga, pindi wanapopelekwa katika vituo vya afya kwa ajili ya kliniki.



Nalepo Laizer, ngariba aliyeacha kazi hiyo na sasa ni mwanaharakati anayepiga vita ukeketaji katika jamii ya kifugaji, wilayani Longido. **PICHA ZOTE: ZANURA MOLLEL.**

"Naishauri serikali ikifanikiwa kufanya jambo hili, tutakomesha kabisa. Lakini, kazi niliyo nayo kwa sasa nikuzunguka sehemu mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu juu ya ukeketaji na kutoa taarifa za wanaofanya kitendo hiki ili wachukuliwe hatua mapema," anasema.

**MHANGA UKEKETAJI**

Msichana aliyekeketwa (jina tunalo), ana simulizi kwamba wamekuwa wakipata wakati mgumu kutokana na mila batili ndani ya jamii yao, ikiwamo kipindi cha ujauzito wanawake hunyimwa kula vyakula vyenye virutubisho, kwa madai wasipate matatizo wakati wa kujifungua.

Pia, anasema wakati wa tendo la ndoa huwa wanapata maumivu makali na daima hawafurahii tendo hilo, akihimiza: "Mimi nimepitia kwenye mila hiyo najua adha inayotupata watoto wa kike, naomba serikali isimame kidete kukemea tena kwa sauti kubwa jambo hili."

AFYA

## AFANDE POLISI JINSIA:

# Kinababa fungukeni, tunajua ukatili jinsia mnaupata, mkipigwa mripoti

• Serikali yalia mateso ya vipigo, ukeketaji • Wiki 2 za ubia UNFPA, operesheni jinsia • Serikali yaanika mitaa iliko vikwazo vyake

**Na Sabato Kasika**

JUMATATU wiki hii, imeanza siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake, wasichana na watoto, zikiwa na kaulimbiu "Kizazi chenye usawa, simama dhidi ya ubakaji".

Kabla ya kuanza kwa maadhimisho ya siku hizo 16 wiki iliyopita, wadau mbalimbali walikutana jijini Dar es Salaam kujadili hali halisi ya ukatili ilivyo katika jamii nchini na kutaja mbinu kadhaa za kuukomesha.

Wadau hao ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Jeshi la Polisi, TGNP Mtandao na Children's Dignity Forum (CDF), waliokutanishwa katika warsha maalum na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) Tanzania.

Warsha hiyo ilihusu kujenga uwezo wa wanahabari kuhusu ukatili wa kijinsia, hasa wakati huu wa siku 16 za kupinga ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto.

Hayo yamefanyika, kwa kulenga kutoa fursa kwa wanawake, wanaume, vijana wa kike na kiume na wanaharakati wengine ndani ya wiki mbili zilizopo, kukuza uelewa wa umma juu ya mchango wa wanawake katika maendeleo.

Vilevile, lengo ni kutafakari matokeo ya harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi na kutafakari pia mafanikio hayo.



Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, SSP Faiza Suleiman, akitoa neno kwenye warsha. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

### YALIYOJIRI

Katika warsha hiyo, ilibainika kuwa baadhi ya jamii kuendelea kukumbatia mila potofu, ni moja ya sababu zinazochangia kuwapo kwa vitendo vya ukatili kwa wanawake, wasichana na watoto nchini.

Ofisa Msimamizi wa Dawati la Mpangokazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa), kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Seto Ojwando, ndiye aliyetoa mada kwenye warsha hiyo.

Anafafanua kuwa serikali na wadau mbalimbali wanajitahidi kupambana na vitendo vya ukatili, kupitia mbinu mbalimbali, ikiwamo utoaji elimu, ingawa tatizo bado lipo.

Seto anasema, baadhi ya wanajamii wanaendelea kukumbatia mila potofu na kunyima ushirikiano hata pale wanapofanyiwa ukatili. Ni tatizo linalotajwa kuendelea kuwapo nchini.

"Hili bado ni tatizo, watu wanafanyiwa ukatili wa kijinsia, ukiwamo ubakaji, ukeketaji na vipigo, lakini wakati mwingine wanamalizana na watuhumiwa bila ya kufikishwa kwenye vyombo vya dola. Niwaombe tushirikiane katika vita hii," anasema Seto.

> **Tatizo lililopo ni mfumo dume, kuwa mwanaume hawezi kupigwa na mwanamke au kufanyiwa ukatili, lakini ukweli wapo tena wengi tu.**



Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, SSP Faiza Suleiman, akitoa neno.



Ofisa Msimamizi wa Dawati la Mpangokazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa), kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Seto Ojwando.

Pia, anasema elimu ni muhimu katika vita dhidi ya ukatili, kwa vile kuna baadhi ya wanaofanyiwa ukatili huo, wanaliona bado ni jambo la kawaida, hivyo ipo haja ya kuendelea kuwaelimisha.

Kauli ya Seto inaungwa mkono na Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, Mrakibu Mwandamizi (SSP) Faiza Suleiman, anayekiri kuendelea kuwapo ukatili wa kijinsia katika jamii.

Anaeleza imani yake kwamba ukatili hauishii kwa wanawake tu, lakini wanaume nao ni waathirika wa ukatili huo, ila ni wagumu kutoa taarifa kwenye mamlaka za kisheria, ikiwamo kwenye vituo vya polisi.

"Tatizo lililopo ni mfumo dume, kuwa mwanaume hawezi kupigwa na mwanamke au kufanyiwa ukatili, lakini ukweli wapo tena wengi tu. Ushauri wangu ni kwamba, wanaume fungukeni," anasema SSP Suleiman.

SSP Sulemain anasema, wanaume wakifunguka watakuwa wamechangia kwa kiasi kikubwa vita vya kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii, ambao umekuwa mgumu kumalizika, licha ya juhudi mbalimbali za kuumaliza.

### KUTOKA UNFPA

Jacqueline Mahon, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA) Tanzania, anasema kuelekea mwaka 2030, UNFPA imejiwekea malengo kutokomeza mila potofu na ukatili wa kijinsia kwa mwanamke, msichana na mtoto.

Anasema, kati ya Novemba 25 hadi Desemba 10 ya kila mwaka, Umoja wa Mataifa, serikali na wadau wa maendeleo, katika masuala ya jinsia huadhimisha siku 16 za harakati za kupinga unyanyasaji wa kijinsia.

"Tunafanya kazi na wadau watekelezaji kama vile Jeshi la Polisi Tanzania, Jukwaa la Utu wa Mtoto, TGNP Mtandao na Serikali ya Tanzania, katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinisa Dhidi ya Wanawake na Watoto," anasema Mahon.

Anasema, katika kudhibiti ipasavyo vitendo vya ukatili vinapotokea, UNFPA na Jukwaa la Utu wa Mtoto, wanaendelea kufanya kazi na Jeshi la Polisi Tanzania ambalo liko mstari wa mbele kudhibiti vitendo hivyo.

Jacqueline anasema zinahitajika juhudi za kitaifa kutokomeza ukatili wa kijinisa kwa mtu mmoja mmoja, familia, jamii na vyombo vya habari.

### WADAU WENGINE

Mwakilishi toka asasi ya asasi ya Children's Dignity Forum (CDF), Winifrida Makuru, anawashauri waandishi kuepuka kuandika habari zinazoweza zikachochea vitendo vya ukatili.

"Kuna habari nyingine ukisoma unakuta ni kama zinaendeleza ukatili, hivyo ushauri wangu kwenu ni kwamba mngejikita zaidi kuandika zile ambazo zinakemea vitendo hivyo, katika jamii," anasema Makuru.

Makuru anasema, waandishi wa habari ni watu muhimu katika vita ya kupambana na vitendo vya ukatili kwa kuibua matukio hayo kwenye jamii huku mamlaka husika zikichukua hatua za kuyadhibiti.

Naye mwakilishi kutoka TGNP Mtandao, Beatrice Ezekiel, anasema, vita ya dhidi ya vitendo vya ukatili ni kila mmoja, hivyo jamii iendelee kuelimishwa ili iachane na mila potofu zinazochangia ukatili.

"Pamoja na wadau wote, mimi ninaamini vyombo vya habari vina nguvu kubwa sana na vinaweza kusaidia kukomesha ukatili huo, hivyo vitusaidieni sana kupambana na vitendo vya ukatili," anasema Beatrice.

### SIKU 16 ZIKOJE?

Historia inaeleza kuwa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ni kampeni maalum ya kimataifa inayoongozwa na Kituo cha Kimataifa cha Wanawake katika uongozi tangu mwaka 1991.

Chimbuko lake linatokana na kupinga unyanyasaji wa kijinsia na mauaji ya kinyama ya kina dada wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominica mwaka 1960.

> **Tunafanya kazi na wadau watekelezaji kama vile Jeshi la Polisi Tanzania, Jukwaa la Utu wa Mtoto, TGNP Mtandao na Serikali ya Tanzania.**

Mwaka 1991, Umoja wa Mataifa (UN) ulichagua Novemba 25 iwe siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia, na kilele chake huadhimishwa Desemba 10 ya kila mwaka.

Siku hizo, pia zinatoa mwanga wa uelewa kwa jamii kwa siku nyingine muhimu kama Novemba 29, ambayo ni siku ya Kimataifa ya Watetezi wa Haki za Wanawake.

Aidha, baada ya siku hiyo, Desemba mosi ya kila mwaka ni Siku ya Ukimwi Duniani na kisha Desemba 6 huwa ni siku ya Mauaji ya Kikatili ya Montreal (Canada) 1989, wanawake 14 waliuawa, pia Desemba 10 ni Siku ya Haki za Binadamu Duniani.

# Chanjo inavyohamisha afya kutoka shida hadi maisha bora




Mkurugenzi wa tiba kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Maghembe, akizungumza katika mkutano na Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (Mewata). **PICHA: YASMINE PROTACE**

**Na Yasmine Protace**

MAANA ya chanjo ni nini? Kitaalamu inatajwa kuwa mandalizi ya kibaoilojia, inayotoa kingamwili dhidi ya ugonjwa ya baadhi ya magonjwa, hasa ya kuambukiza.

Hiyo inatajwa kuwa njia bora ya kujikinga dhidi ya baadhi ya magonjwa, yakitajwa baadhi kama kifua kikuu, tetekuwanga na pepo. Ndio inatumika kuwalinda watoto wadogo dhidi ya magonjwa hatari.

Hivi karibuni, Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (Mewata), kimewataka kuweka msisitizo kwenye masuala ya utoaji elimu kuhusiana na chanjo nchini, ili idadi ya watoto wanaopatiwa chanjo kufikiwa.

Mkurugenzi wa Tiba kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Magembe, katika ufunguzi wa mkutano wa mwaka wa chama cha Mewata, anasema elimu ya afya kwa wananchi inatakiwa kushushwa hadi chini ili taarifa kuwafikia walengwa wengi.

"Suala la chanjo ni la kuwekea msisitizo, hivyo endapo tutashirikiana katika utoaji wa elimu hususan pale wizara inapokuwa na kampeni za chanjo ili watoto wetu wachanjwe na kufikia azma ya serikali ya kuwa na watoto waliokingwa kwa chanjo inatimia" anasema.

Dk. Grace anakishukuru chama hicho kutoa huduma za afya kwa kinamama, hususani katika kukabili saratani ya mlango wa kizazi na ile ya matiti.

Anasema wanawake ni taifa kubwa na kauli mbiu ya serikali ya awamu ya tano ni uchumi wa kati kupitia viwanda hivyo hatuwezi kuwa na uchumi wa kati endapo wananchi wake ni wagonjwa hususani wanawake ambao ni wazalishaji.

Daktari huyo anasema serikali inatambua mchango wa Mewata katika kukabili maradhi ya saratani, hivyo imejenga vituo kutoa huduma katika zaidi ya vito 400, asilimia 70 ya afya inatoa huduma ya upasuaji nchini.

Pia, anaongeza kuwa hivi sasa magonjwa yasiyoambukiza yanachangia asilimia 40 ya vifo nchini. Serikali kupitia wizara inayohusika na afya, ilifanya tathmini ya sera ya afya na kubaini magonjwa hayo yanaongezeka kwa kasi kubwa, pia kuua wengi.

Dk. Grace ababainisha shida ya saratani ya mlango wa kizazi, ni kati ya magonjwa yanayoongoza kusababisha vifo vya wanawake kwa takribani asilimia 50, ikifuatiwa na saratani ya matiti.

Pia Mkurugenzi huyo anaitaka Mewata kutafuta namna ya kushughulikia unyanyasaji na ukatili wa kijinsia kwa wasichana, maana vitendo hivyo vinaongezeka kila siku.

Rai yake kwamba, Mewata izidi kutoa elimu kwa jamii, ili kuhakikisha jamii inabadilika, kwani mabinti hao sasa inakamilika, akisistiza kwamba kisaikolojia inaathiri malezi ya watoto.

AFYA

# Simulizi ya utitiri mimba ki mabinti sekondari waishio

**Na Marco Maduhu**, CHATO

• Wenyewe tabu; vijana kijijini janga • 'Tufanye bado wamelala • Mkoa waishia kulalama, kijiji c

CHANGAMOTO ya uhaba wa mabweni katika shule nyingi, hasa zilizoanzishwa katika ngazi ya sekondari ya kata nchini.

Imekuwa tatizo kwa mabinti wanaoishi umbali mrefu kwenda kupanga vyumba mitaani maarufu kama 'mageto' na kujikuta wanaambulia ujauzito unaokatisha masomo yao.

Shule nyingi za kata zimekosa mabweni ya kuhifadhi wanafunzi kwa mabinti wanaoishi umbali mrefu, hususani maeneo ya vijijini, wengi wanaamua kupanga 'mageto' ili wawe karibu na shule, lakini wanajikuta wanaangukia kufanya ngono na kuishia kupata ujauzito.

Shule ya Sekondari ya Kata Kachwamba, iliyopo kwenye kijiji cha Igalula, Kata ya Kasenga wilayani Chato, in upungufu wa mabweni ya kuhifadhi wanafunzi hasa wa kike wanaoishi umbali mrefu na sasa wanaamua kupanga vyumba mitaani na wanaishia kuambulia ujauzito.



Baadhi ya wasichana wanaosoma katika Shule ya Sekondari Kachwamba wilayani Chato, wakiwa kwenye 'mageto' yao walikopanga.

### MKUU SHULE

Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kachwamba, Agustine Joseph, anasema ukosefu huo wa bweni unawaathiri sana taaluma za wanafunzi wasichana, kutokana na kuishi katika 'mageto' wengi wanashindwa, kwa sababu ya kuendekeza ngono mitaani.

Anataja maeneo wanakotoka ni vijiji vya Kasenga, umbali wa kilomita saba, Magiri na Mwekako, zote umbali wa kilomita tano, hivyo wanaamua kupanga 'mageto' mitaani wawe karibu na shule, lakini bahati mbaya wengi wanaangukia kuambulia mimba na kuacha masomo.

"Upangaji huu wa 'mageto' kwa wanafunzi hapa shuleni kwetu umekuwa ukiathiri sana taaluma za wanafunzi, hasa wa kike pamoja na kuambulia ujauzito.

"Kwa takwimu za mwaka jana, wanafunzi watano walipewa mimba na kuacha masomo na mwaka huu kuanzia Januari hadi Oktoba, wameshapewa watatu," anasema Joseph.

Anaongeza: "Hivi sasa hatutarajii mimba tena za wanafunzi kuongezeka kutokana na msaidizi wa kisheria kutoka Shirika la Chalao wilayani Chato, Deogratius Mulima, kuja hapa shuleni na kutoa elimu ya kujitambua kwa wanafunzi, pamoja na kuacha ngono zembe katika umri mdogo,"

### MWENYEJI AKIRI

Agnes Marco, ni mwanafunzi wa shule ya Kachwamba aliyepanga katika 'geto', anakiri kuwapo changamoto kwenye nyumba hizo za kupanga, wanafunzi wanafanya mapenzi wenyewe na wengine kuwa na uhusiano na wanakijiji.

> **Kwa takwimu za mwaka jana, wanafunzi watano walipewa mimba na kuacha masomo na mwaka huu kuanzia Januari hadi Oktoba, wameshapewa watatu.**

Anasema, mwanafunzi anapopanga 'geto' uamuzi wa mengi uko katika mikono yake, kwa sababu ya kuwa mbali na wazazi wake.

Eneo mojawapo analolitaja ni pindi mwanafunzi anapokuwa mbali na wazazi na anapungukiwa fedha, anaangukia kujiingiza uhusiano wa aina hiyo, kupata fedha za kujikimu na ndio mwanzo wa safari za kuangukia ujauzito na kuacha masomo.

Anafafanua sura ya pili, ni pale wanafunzi kati yao wenyewe wanaendekeza mapenzi, katika mikusanyiko yao ya kujisomea usiku katika makazi hayo.

Mwanafunzi huyo anasema, kadri wanavyojumuika na kukaribiana ndipo kunakuja simulizi za kutamaniana ki mapenzi, hatimaye inakuwa mazoea yao.

"Naiomba sana serikali itusaidie kujenga mabweni kwenye shule yetu hii ya Sekondari Kachwamba, ili kutunusuru sisi wanafunzi wa kike tupate kutimiza ndoto zetu, sababu suala hili la kupanga 'mageto' huwa lina vishawishi vingi. Hata ukiwa mgumu, mwisho wa siku utajikuta unafanya mapenzi bila kutegemea," anasema Marco

"Tatizo jingine, wazazi wetu huwa hawaji hata kututembelea na hawajui mtoto wao wanaishi katika mazingira gani, yeye ni kuruhusu tu kwenda kupanga na kutuma chakula pamoja na pesa ya matumizi, lakini hawafuatilii maendeleo ya shule na mwisho wa siku anashangaa mtoto wake anarudi na ujauzito," anasema.


Mwenyekiti wa Kijiji cha Igalula, wilayani Chato mahali iliko Shule ya Sekondari Kachwamba, Makoye Butondo, akifafanua ilivyo mikasa hiyo. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU.**

### UONGOZI KIJIJI

Mwenyekiti wa kijiji cha Igalula iliko shule hiyo, Makoye Butondo, anakiri shida ya wanafunzi waliopanga Mageto kufanya ngono zembe ma kijiji chake sasa kimeweka mikakati ya msako majira ya usiku kwenye 'mageto' hayo.

Butondo anasema, na mimba za wanafunzi wa shule hiyo, wale waliopangishaa 'mageto' hayo wamejiwekea mkakati wa kufanya doria usiku wakiwa na ulinzi shirikishi, kwa kukagua vyumba wanapolala wasichana, kubaini kama wanafanya mapenzi.

Aidha anasema wanapokuwa kwenye doria hiyo mara nyingi huwa wanawakuta wanafunzi kwa wanafunzi wakifanya mapenzi kwenye 'mageto' hayo, wamekuwa wakiwakamata na kuwapatia adhabu kali, ikiwamo kuwachapa viboko, kufanya usafi wa mazingira kwenye ofisi ya kijiji pamoja na kuwaita wazazi wao.


Butondo anaendelea kwamba, mara baada ya kubaini tabia hiyo ya wanafunzi kufanya mapenzi waliamua kuwaamuru wavulana kupanga vyumba mbali, hivyo tatizo sasa ni wanakijiji kuwatorosha nyakati za usiku, kwenda kufanya nao mapenzi kwenye nyumba zao.

"Upangaji huu wa 'geto' kwa wanafunzi wa kike ni tatizo kubwa sana la upataji wa mimba, na mpaka sasa wanafunzi watatu tayari wameshapewa ujauzito na wanakijiji, na watuhumiwa wame-

# ijijini 'geto'

## nini' wazazi haamua







Baadhi ya wasichana wa Shule ya Sekondari Kachwamba wilayani Chato, wakiwa kwenye 'mageto' yao.

shakimbia kusikojulikana ingawa tayari wanafahamika," anasema Butondo.

"Sasa hivi tunachokifanya ni kuimarisha ulinzi mkali, ambapo mwanakijiji akionekana tu na mwanafunzi tunamwita na kuanza kumhoji, pamoja na kupitisha 'roll call' ya majina ya wanafunzi wa kike nyakati za usiku ili tubaini nani hayupo na kaenda wapi, lengo tuweze kutokomeza mimba kabisa shuleni hapa,"anaongeza.

Josephat Kolinel, ni kijana anayeishi kijijini Igalulam, mahali iliko shule hiyo ya kata, anakiri vijana wamekuwa wakijenga uhusiano na wanafunzi wanaopanga kwenye 'mageto' anabainisha baada ya mkondo wa sheria na elimu kuchukua nafasi, sasa wanaogopa kuwasogelea.

"Mimi ni kijana ambaye naishi kwenye kijiji hiki na shughuli yangu kubwa ni bodaboda. Baada ya elimu ya kisheria kutolewa kuwa ukimpatia mimba mwanafunzi unafungwa jela miaka 30.

"Sasa hivi tumekuwa tukiwaogopa hata kuwapakia kwenye bodaboda, anaweza hata kukubambikizia mimba ukafungwa," anasema Kolinel.

### MAOFISA SERIKALI

Ofisa Elimu wa Kata ya Kasenga, wilayani Chato, Daniel Ngosha, anasema suala la mimba kwa wanafunzi wa shule hiyo ya kata imekuwa tatizo. Serikalini wamekuwa wakihamasisha wazazi wajenge mabweni, lakini mwitikio wake umekuwa hafifu.

Anasema mkakati uliopo ni kuendelea kutoa elimu ya kujitambua

> **Mimi ni kijana ambaye naishi kwenye kijiji hiki na shughuli yangu kubwa ni bodaboda. Baada ya elimu ya kisheria kutolewa kuwa ukimpatia mimba mwanafunzi unafungwa jela miaka 30.**



Msaidizi wa Kisheria kutoka Shirika la Chato Legal Aids Organisation (CHALAO), Deogratius Mulima, akielezea adha ya mimba za wanafunzi kwenye Shule ya Sekondari Kachwamba, iliyoko Chato.



Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kachwamba wilayani Chato, Augustine Joseph, akielezea shida ya mabinti wanafunzi wake wanaoshi 'geto.'

kwa wanafunzi, pamoja na wanakijiji kutambua umuhimu wa kuwaaacha wanafunzi watimize ndoto zao.

Msaidizi wa Kisheria kutoka Shirika lisilo la kiserikali, wilayani Chato, Deogratius Mulima, anasema mara baada ya kusikia tatizo hilo la mimba kwa wanafunzi katika shule ya Kachwamba, waliamua kwenda kutoa elimu ya wanafunzi kujitambua na madhara ya ngono katika umri mdogo.

Pia anasema waliwekeana mikakati na wanafunzi wa kike, marufuku kutembea mitaani mmoja mmoja na kuacha kujisomea na wavulana kwenye 'mageto' yao nyakati za usiku.

"Nimeguswa na tatizo la mimba za wanafunzi kwenye shule hii ya kata Kachwamba. Takwimu nilizopewa kuanzia Januari hadi Oktoba tayari wanafunzi watatu wameshapewa ujauzito na kuacha masomo, ndipo nikaanza kutoa elimu ya kisheria, kujitambua, na madhara ya ngono katika umri mdogo.

"Nilipomaliza kutoa elimu kwa wanafunzi, nikahamia kwa wanakijiji, ikiwamo kuwafuatilia wale ambao wamewapatia ujauzito wanafunzi. Kwa bahati mbaya, mara baada ya kusikia wanatafutwa wakakimbia kusikojulikana. Nina imani mimba kwenye shule hii tena haiwezi kuogezeka na zitakoma kabisa," anasema.

### KAULI YA MKOA

Ofisa Taaluma Mkoa wa Geita, Kaitila Mafwimbo, anasema takwimu za wanafunzi wa sekondari waliopewa ujauzito mwaka jana na kuacha masomo kuwa ni 170 na mwaka huu kuanzia Januari hadi Oktoba, kuna mimba tatu tu.

Mafwimbo anaainisha takwimu za mimba mwaka jana za wanafunzi wa sekondari kwa kila halmashauri, idadi katika mabano: Nyang'wale (73); Mbogwe (10), Geita Mjini (34); Chato (53), Bukombe na Geita Vijijini hakukuwapo na mimba.

Denis Bandisa, ni Katibu Tawala mkoani Geita, anabainisha mkakati uliopo wa kutokomeza mimba shuleni ni kuhamasisha wananchi wajenge mabweni, pamoja na kupeleka watoto wao kuishi kwenye mabweni hayo na siyo kuwazuia.

Anaeleza chimbuko la mimba kimkoa ni kuendelea kuwapo ni wazazi wenyewe wa Geita kutotambua umuhimu wa elimu, kwani walipaswa kuanzisha ujenzi wa maboma ya mabweni kisha serikali ikiyamalizia, lakini mwitikio wake umekuwa hafifu, ikizingatiwa kuna wazazi hawapendi watoto wao waishi bwenini.

"Mkoa wetu huu wa Geita bado tuna safari kubwa sana ya kutoa elimu kwa wazazi kutambua umuhimu wa elimu. Mfano kwenye Shule ya Sekondari Nyang'wale, bweni la wanafunzi wa kike lipo, lakini wazazi hawataki kupeleka watoto wao wakaishi hapo shuleni," anasema Bandisa.

Anataja pia adha ya umbali mrefu wa kutoka shule, lakini unachangia mikasa hiyo, ambayo dawa yake ni kuwaweka bwenini, pamoja na wazazi ya kutambua umuhimu wa elimu.

AFYA

# Dk. Msaki: Haya hapa makubwa tuliyonayo Hospitali Sekou Toure

## • Ghorofa 5 mpya mama & mtoto • Usafishaji figo, tiba moyo zaja • Siku wanaojifungua 60; ‘kisu’ wanne



Jengo jipya la Mama na Mtoto, hospitalini Sekou Toure. **PICHA ZOTE: ATHONY GERVAS.**



Mganga Mfawidhi wa Hospitali Sekou Toure, Dk. Bahati Msaki.

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

***KATIKA mwendelezo wa simulizi ya maudhui ya tiba na afya kutoka Mkoa wa Mwanza na Hospitali ya Rufani Mkoa Sekou Toure, sehemu ya tatu wiki hii, Mganga Mfawidhi, Dk. Bahati Msaki, ana ufafanuzi wa huduma na mageuzi makubwa yanayofanyika kukidhi mahitaji ya wagonjwa wake. Endelea naye;***

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza -Sekou Toure, ni tegemeo la kutoa huduma za afya kwa wagonjwa katika mkoa huo,pia mingine ya jirani Kanda ya Ziwa.

Nafasi hiyo imekuwa ikiipa wakati mgumu wa kukabili ongezeko la wagonjwa wa aina mbalimbali, wakiwamo wa rufaa na kawaida wanaofika kupatia matibabu.

Katika kupambana na maboresho ya huduma za afya katika hospitali hiyo, serikali iliamua kufanya upanuzi mkubwa wa huduma za wagonjwa, baada ya kuanza ujenzi wa jengo kubwa la ‘mama na mtoto.’

Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk.Bahati Msaki, anaelezea namna serikali ilivyotupia jicho lake katika kuboresha huduma za afya kwenye hospitali hiyo, ikiwamo uwekezaji mkubwa wa vifaa na majengo.

> **“ Pia kwa siku hospitali yetu inapokea kinamama wajawazito 60 kwa ajili ya kujifungua na tunazalisha kati ya 20 na 30 wa kawaida, tunazalisha kwa njia ya upasuaji ambao ni watatu hadi wanne kwa siku.**

Hapana shaka katika madai hiyo, tabasamu la furaha ya Dk. Bahati haifichiki, akielekeza pongezi kwa mkuu wa nchi na muasisi wa mradi huo, Rais Dk. John Magufuli kuhakikisha Wizara ya Afya, Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inasimama pazuri katika uwajibikaji wake.

Pia, anamtaja Waziri Ummy Mwalimu, kwamba ni ‘mwanamke shujaa’ aliyeshika dhamana ya wizara akihakikisha huduma bora za afya zinawafikia wananchi wote kila kona ya nchi, ikiwamo upatikanaji dawa hospitalini Sekou Toure.

Dk. Bahati anaiambia Nipashe kuwa serikali imeshatoa pesa kiasi cha Sh. bilioni 10, kwa ujenzi wa jengo la mama na mtoto, ili kuondoa msongamano mkubwa katika wodi za mama na mtoto, wagonjwa wa upasuaji na kawaida.

“Sasa tayari tumeshapokea zaidi ya Sh. bilioni nne, ili kuendelea na ujenzi huo,” anasema, Dk. Bahati na anaongeza: “Ujenzi huo unatarajia kukamilika mwakani Juni 2020.

### CHANGAMOTO JE?

Dk. Bahati anasema, kinachowakwamisha sasa katika hospitali hiyo ni uhaba wa vyumba vya kufanyia oparesheni za dharura kwa wagonjwa, hali ambayo inamfanya kunapokuwapo na dharura operesheni zingine zinasimama na kuisababisha msongamano.

“Hospitali yetu bado kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya upasuaji, mfano inapotokea wagonjwa wa dharura, operesheni zingine zinasimama kwanza na kusababisha kuwepo msongamano mkubwa,” anasema Dk,Msaki.

Aidha, anaeleza kuwa jengo hilo la mama na mtoto likikamilika litakuwa na vyumba viwili vikubwa vya upasuaji, vyumba vya kujifungua kinamama wajawazito, kiliniki ya mama wajawazito na watoto, chumba cha dawa, maabara na mapokezi.

### MZIGO WAKE

Dk. Bahati anasema, hospitali ya Sekou Toure, imekuwa mpokeaji mkuu wa wagonjwa mbalimbali kutoka wilaya zote za Mkoa wa Mwanza na mikoa jirani ya Kanda ya Ziwa.

“Idadi ya wagonjwa wa nje, pia wamekuwa wakiongezeka siku hadi siku, kila siku pamoja na wagonjwa wa mikoa jirani ya kanda ya ziwa, ikiwemo,Geita, Shinyanga, Mara na Simiyu,’ anasema.

Kwa mujibu wa mganga huyo mfawidhi, mikoa hiyo imekuwa ikitegemea huduma za matibabu katika hospitali ya Sekou Toure, ikiwamo wagonjwa wa rufaa.

“Pia kwa siku hospitali yetu inapokea kinamama wajawazito 60 kwa ajili ya kujifungua na tunazalisha kati ya 20 na 30 wa kawaida, tunazalisha kwa njia ya upasuaji ambao ni watatu hadi wanne kwa siku,’ anasema.

Anataja idadi ya madaktari hospitalini, bingwa wapo 12, wakiwemo wa upasuaji kinamama, mifupa, mionzi na magonjwa ya moyo, shinikizi la damu, figo, kansa na kisukari.

### MAFANIKIO

“Mafanikio mojawapo, tumepunguza vifo vya kinamama wajawazito hadi kufikia asilimia 50 mwaka huu. Mwaka jana 2018 tulipokea kinamama wajawazito elfu kumi, lakini vifo vilikuwa 17 kwa mwaka mzima,” anasema na kuongeza: “Mwaka huu tangu januari hadi sasa 2019 vifo vyao ni vinane tu, kinamama tuliowapokea.”

Anasema vifaa vya kutoa huduma kwa wagonjwa katika hospitali hiyo vinatosheleza pasipo shaka na kwa sasa inatarajia kufungua huduma ya kusafisha figo na tayari imeshapokea mashine ya kutolea huduma hiyo.

Dk. Bahati anasema, pia wanatarajia kupokea mashine ya mionzi CT scan moja kwa ajili ya kutoa huduma hospitalini hapo.

***• Soma zaidi Alhamisi ijayo, kupata yanayojiri kiafya kutoka mtazamo wa Sekou Toure, Mwanza.***

***• Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa mawasiliano (+255) 0682 86 92 44 na barua pepe: anthonygervas@yahoo.com***



# Wasiojulikana wavunja, waiba mali za mil. 10.7/- shuleni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wasiojulikana wamevunja na kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 10.7 kwenye Ofisi ya Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Uhuru iliyopo Kata ya Mwakibete jijini Mbeya.

Taarifa ya kuvunjwa kwa ofisi hiyo ilitolewa juzi na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Hatibu Lugga, wakati wa mkutano wa dharura wa wazazi ulioitishwa kwa ajili ya kujadiliana changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Alisema vifaa vilivyoibiwa ni pamoja na mashine kubwa ya kudurufu maandishi (mashine ya fotokopi) yenye thamani ya Sh. 8,000,000 ambayo walipewa kama msaada na baadhi ya wadau wa elimu mkoani humo.

Alivitaja vitu vingine ambavyo viliibiwa ni kompyuta ya mezani, redio na fedha taslimu ambazo zilikuwa zimehifadhiwa kwenye kasiki ndani ya ofisi hiyo.

"Waliingia usiku hapa na wakavunja geti, wakavunja mlango na kasiki na kuiba hivyo vitu ambavyo vyote kwa pamoja vina thamani ya Sh. milioni 10.73, sasa ni jambo ambalo limetushtua sana hivyo tunatakiwa kuimarisha ulinzi ili kukabiliana na masuala haya," alisema Lugga. Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Tito Nyondo, alisema alisema chanzo cha wizi huo ni ukosefu wa ulinzi imara kwa madai kuwa wamekuwa wakiomba kibali cha kuwachangisha wananchi fedha za kumlipa mlinzi lakini kibali hicho kimekuwa kikicheleweshwa.

Alisema walituma barua ya kuomba kibali cha kuwachangisha wananchi fedha za kumlipa mlinzi tangu Juni mwaka huu katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, lakini kibali hicho kimechelewa kutolewa na kwamba tangu kilipotolewa haijapita hata wiki moja ndio tukio limetokea. Alisema endapo kibali kingetolewa mapema pengine tukio hilo lisingetokea kwa madai kuwa wazazi wako tayari kuchangia lakini kilichokuwa kinachelewesha ni kibali hicho.

"Tumekuwa tukishirikiana na Ofisa Mtendaji wa Kata yetu kufuatilia kibali hicho, lakini hatuelewi sababu ya kuchelewa kutolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, sasa madhara yake yameanza kuonekana kwa vifaa vya shule yetu kuibiwa," alisema Nyondo.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwakibete, Lugano Mwamsojo, alisema kwa mujibu wa taratibu ni kosa kuwachangisha wazazi mchango wa aina yoyote bila kuwa na kibali cha serikali.

Alisema kutokana na utaratibu huo ndio maana walikuwa hawajaanza kuwachangisha wananchi mchango kwa ajili ya kuajili walinzi katika shule hiyo.

Diwani wa Kata ya Mwakibete, Lucas Mwampiki, alisema yuko tayari kuwahamasisha wananchi kuchangia maendeleo ya aina yoyote endapo kibali kitatolewa, na kwamba kinachokwamisha ni kuchelewa kutolewa kwa kibali hicho.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, na kwamba mtu mmoja ambaye alikuwa mlinzi wa shule hiyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kutokana na tukio hilo.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mhandisi MaryPrisca Mahundi (kushoto), akipeana mkono na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Usambazaji Mbolea Petrobena EastAfrica, Peter Kumalilwa (kulia), baada ya kupokea shehena ya mbolea ya tumbaku wilayani kwake ikiwa ni maandalizi ya msimu ujao wa kilimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC Chunya afagilia kampuni ya mbolea

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI ya Wilaya ya Chunya, imepongeza kampuni ya usambazaji wa mbolea za Yara na pembejeo zingine za kilimo ya Petrobena EastAfrica, kwa kusambaza mbolea kwa wakati katika wilaya hiyo, ikieleza hali hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji mazao msimu ujao wa kilimo.

Akizungumza baada ya kupokea shehena ya mbolea ya kupandia na kukuzia tumbaku kutoka kampuni hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alisema kuwasili kwa mbolea hiyo kabla ya msimu ni ishara njema kuwa wakulima watazalisha kwa wingi na kuinua uchumi wa wilaya.

"Naishukuru kampuni ya Petrobena kwa kuonyesha dhamira ya dhati ya kuinua sekta ya kilimo kwa kusambaza mbolea kabla ya msimu hali inayompa mkulima msukumo wa kufanya kazi ya kilimo kwa kujituma zaidi," alisema Mahundi.

Alisema jukumu lililobaki ni kwa wakulima kuchangamkia kununua mbolea hiyo ili msimu wa kilimo utakapoanza wasipate tabu ya mbolea, hali itakayosaidia kuongeza uzalishaji ukilinganisha na misimu iliyopita ya kilimo kutokana na kuchelewa kwa mbolea.

"Serikali imejipambanua katika kukuza uchumi na kuondokana na umaskini, hiyo hatua zinazofanywa na wadau kama Petrobena ni ishara kuwa azma ya Serikali inatekelezeka kwa vitendo kwa kuwapatia wananchi mahitaji muhimu katika shughuli zao ikiwamo kilimo," alisema Mahundi.

Alisema upatikanaji wa pembejeo za kilimo ilikuwa ni changamoto kubwa kwa wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya, Petrobena imekuwa mkombozi katika kuhakikisha mbolea inawafikia wakulima kwa wakati hali itakayochochea uzalishaji wa tumbaku kuongezeka. "Kuongezeka kwa mavuno ya tumbaku yatapelekea soko la kukua na kufanya uchumi wa wilaya yetu kuongezeka na kuwa sehemu ya kuchangia pato la taifa," alisema Mahundi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Petrobena East Africa, Peter Kumalilwa, alisema kuwa kampuni yake imedhamilia kufikisha kwa wakati mbolea kwenye mikoa yote inayozalisha tumbaku hapa nchini kabla ya msimu.

Alisema mbolea zinazosambazwa kwa sasa ni za kupandia na kukuzia ili msimu utakapoanza wakulima wasihangaike kwenda kutafuta mbolea na badala yake waelekeze nguvu kwenye mashamba. "Sisi tumejipanga kuhakikisha tunafanikisha mageuzi katika sekta ya kilimo na kuunga mkono azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025 inafanikiwa kwa vitendo," alisema Kumalilwa.

Alisema mbali ya Chunya kampuni imeshasambaza mbolea ya tumbaku kwa ajili ya kupandia na kukuzia katika mikoa mbalimbali inayolima zao hilo hapa nchini ikiwamo Tabora na Songwe, na kwamba lengo ni kuongeza uzalishaji na kumsaidia mkulima kuondokana na umaskini.

## DAS akerwa wanafunzi wanaoficha mafataki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Rungwe, Mnkondo Bendera, ameshauri wanafunzi wa kike wanaopata mimba na kutotoa ushirikiano kuwabaini waliowatia mimba hizo, kufungwa jela ili kupunguza tatizo hilo.

Alitoa ushauri huo jana kwenye Kikao cha Ushauri cha Mkoa wa Mbeya (RCC) ambapo alisema tatizo la mimba shuleni limekuwa sugu katika mkoa huo kwa maelezo kuwa pamoja na hatua zinazoendelea kuchukuliwa lakini bado matukio hayo yanaendelea.

Alisema ili kuimarisha vita dhidi ya matukio hayo inatakiwa watoto wa kike wanaoshirikiana na wazazi wao kuwaficha wanaowapachika mimba na wao wakamatwe na kupelekwa rumande ili iwe fundisho kwa wengine.

"Haiwezekani hawa watoto wadogo wakatushinda, tunatakiwa kuongeza hatua za kuchukua ili kukomesha matukio haya ya mimba, nashauri kuwa pamoja na kuwakamata wanaowasababishia watoto hawa mimba pia na wao wakamatwe na kupelekwa rumande," alisema Bendera.

Akitoa ufafanuzi kuhusu ushauri huo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariamu Mtunguja, alisema sheria za nchi hazijatoa ruhusa ya kuwekwa ndani watoto hao.

Alisema ushauri wa Bendera ni mzuri na utazingatiwa isipokuwa kuwasweka ndani watoto wanaopata mimba, na kwamba serikali itaendelea kuwashughulikia wanaume wanaowasababishia mimba wanafunzi.

Awali Katibu wa Sekretarieti ya Mkoa, Conrad Mlinga, alisema ili kukabiliana na matukio ya mimba shuleni inatakiwa kuimarisha ujenzi wa mabweni na hosteli kwenye shule za sekondari mkoani humo.





# Walimu 4,000 wafukuzwa kazi kwa utovu nidhamu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Winifrida Rutaindurwa, amesema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, walimu 4,046, sawa na asilimia 70 ya waliopewa adhabu kutokana na makosa ya kinidhamu, walifukuzwa kazi.

Aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipotoa taarifa ya tume kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuundwa kwake wakati wa kikao kazi cha kaimu makatibu wasaidizi wa wilaya nchini.

Alisema walimu 930, sawa na asilimia 16.2 ya waliopewa adhabu, walipewa onyo na wengine 284, sawa na asilimia 4.9, walipunguzwa mshahara.

Vilevile, alisema walimu 244, sawa na asilimia 4.2 ya waliopewa adhabu, walisimamishiwa nyongeza ya mshahara.

"Walimu wengine 237, sawa na asilimia nne ya waliopewa adhabu, walishushwa cheo na walimu 14, sawa na asilimia 0.2 ya waliopewa adhabu, walifidia hasara," alisema.

Rutaindurwa alisema makosa ya kinidhamu yaliyofanywa na walimu katika kipindi hicho cha miaka mitatu ni pamoja na utoro kazini (makosa 5,447, sawa na asilimia 76.5 ya makosa yote).

Aliongeza kuwa makosa mengine ni kukiuka maadili (makosa 1,290 sawa na asilimia 18.1, uhusiano wa kimapenzi na wanafunzi 162 (asilimia 2.3).

"Makosa mengine kwa ujumla wake yalikuwa 224, sawa na asilimia 3.1 na vilevile katika kipindi cha miaka mitatu, adhabu zilizotolewa ni 5,753," alisema.

Katibu huyo pia alisema katika kipindi hicho cha miaka mitatu, tume imefanikiwa kutekeleza majukumu mbalimbali yanayoakisi malengo ya kuanzishwa kwake.

Alisema moja ya majukumu hayo ni kuratibu na kushughulikia masuala ya kiutumishi ya walimu, akibainisha kuwa walimu 11,581 waliajiriwa na 14,507 walisajiliwa, 11,774 walithibitishwa kazini, 85,799 walipandishwa cheo na 5,760 walibadilishiwa vyeo baada ya kujiendeleza.

"19,450 waliandikiwa vibali vya kustaafu kazi, maombi ya walimu 57 ya kuajiriwa upya kwenye utumishi wa umma baada ya kutumikia adhabu za kufukuzwa kazi yalishughulikiwa na mafao ya walimu 932 yanayohusu pensheni, mirathi na mikataba yalishughulikiwa na tume," alifafanua.

Rutaindurwa pia alisema tume ilitolea uamuzi mashauri 1,280 yaliyorithiwa kutoka iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD).

Alisema mashauri 6,191 yalihitimishwa wilayani, 403 yako kwenye hatua ya uchunguzi na mengine 403 yanasubiri kufanywa vikao.

Akifungua kikao hicho, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Seriklai za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema serikali haitaendelea kumlinda mtumishi yeyote anayefanya kazi kinyume cha kanuni za utumishi.

Waitara alisema idadi ya walimu waliofukuzwa kazi ni kubwa, lakini serikali haiwezi kuwalinda watumishi ambao wamekiuka maadili ya utumishi wa umma.

"Walimu hawa ni pengo kubwa sana, lakini lazima misingi ni taratibu zifuatwe katika utumishi wa umma, hatuwezi kuendelea kuvumilia walimu wanaojihusisha na mapenzi na wanafunzi wao," alisema.

Waitara alitoa wito kwa tume kuendelea kutoa elimu kwa walimu ambao wamekuwa na tabia ya kujihusisha kimapenzi na wanafunzi wao kuwa kuwa hali hiyo inatishia ustawi wa elimu katika maeneo mbalimbali nchini.



Wafanyakazi wa Shirika la Maendeleo (WWF) na Vodacom Tanzania Foundation wakishiriki zoezi la usafi lililofanyika eneo la Chang'ombe jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaandaa sheria kilimohai

**Na Faustine Feliciane,** DODOMA

SERIKALI imesema inaandaa sheria kuhusu kilimohai ili kuisaidia nchi kuwa na sera ya taifa ya kilimo hicho.

Akizungumza kwenye kongamano la kitaifa la kilimohai jijini hapa, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema kabla kipindi cha kwanza cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano kumalizika, serikali itakuwa imeandaa sheria hiyo ili ya kulinda na kuendeleza kilimohai nchini.

Alisema mahitaji ya mazao yanayotokana na kilimohai yamekuwa makubwa duniani na Tanzania inatambua umuhimu wa kilimo hicho endelevu.

"Ni lazima sasa tukigeukie kilimo cha asili na serikali kwa kutambua umuhimu wake tumeona kuna umuhimu wa kuja na sheria ya kilimo hai ambayo itatupelekea kuja na sera ya taifa ambayo itawafanya sasa wakulima kujikita zaidi kwenye kilimohai," alisema.

Hasunga alisema serikali iko tayari kupokea maoni na mapendekezo yatakayopatikana kutoka kwa wakulima kupitia kongamano hilo la kitaifa.

"Niwahakikishie wakulima, kile mtakachojadiliana hapa na mapendekezo yake tutayafanyia kazi kikamilifu na naagiza kwa waandaaji, kufikisha mezani kwangu mapendekezo yote yatakayojadiliwa hapa juu ya kilimohai," waziri huyo aliagiza.

Mkutano huo wa siku mbili umeandaliwa na Shirika la Kuendeleza Kilimohai Tanzania (Toam) na washirika wake, ukiwezeshwa na Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Ubalozi wa Ufaransa nchini.

# Wataka mahakama za familia kuukabili ubakaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kutunga sheria maalum inayoshughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia na mahakama za familia ili kuharakisha kesi za ubakaji ambazo zimekuwa zikikwama kwa kukosa ushahidi. Ombi hilo lilitolewa jana na Mratibu wa Kitaifa wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia jijini hapa.

Alisema kumekuwapo na mtazamo tofauti kwa jamii hasa ya kutoa taarifa na ushahidi pale matukio ya ubakaji yanapotokea kutokana na wanaofanya vitendo hivyo kuwa watu wa karibu na wa kuaminika. "Kesi nyingi zinaharibika na zingine kushindwa kukamilika kutokana na kukosa ushahidi kutoka katika familia, majirani au watu wanaohudumia familia, mara nyingi kesi za ubakaji zimekuwa na hofu, aibu au kuogopa kunyanyapaliwa pale mtu anapoamua kusimama kusimama haki kutendeka.

"Sisi tunaona umefika wakati sasa kuwa na sheria maalum ya masuala ya kijinsia na mahakama za familia ili kushughulikia kesi za ubakaji," alisema.

Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Wanawake (UN-Women), Hodan Addou, alisema mwanamke mmoja kati ya watatu duniani anafanyiwa ukatili wa kijinsia.

"Inakadiriwa wasichana milioni 15 duniani wamekumbana na vitendo vya ubakaji, huku kwa Tanzania ikiwa na wastani wa asilimia 17 ya watu waliofanyiwa ukatili wa kijinsia," alisema.

"Ukizuia ubakaji, utaokoa zaidi ya Dola za Marekani 122,000 na katika nchi nyingi za Afrika zaidi ya nusu ya gharama za ubakaji hulipwa kupitia vyanzo vya mapato vya serikali ikiwamo afya, huduma za jamii na mfumo wa mahakama nchini," alisema.

Aliongeza kuwa serikali ikiwekeza katika kuzuia vitendo hivyo, itaimarisha hali ya afya na maisha bora kwa wanawake na watoto na hatimaye kuokoa maisha yao.

Akizindua kampeni hiyo, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema serikali itaangalia ombi hilo, lakini kwa sasa wataendelea kusimamisha sheria zilizopo ili kukomesha vitendo hivyo. Alisema serikali imekuwa ikitumia gharama nyingi katika kushughulikia waathirika wa vitendo vya ukatili badala ya kuelekeza fedha hizo katika kutoa huduma nyingine za kijamii.

"Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, baadhi ya nchi hutumia hadi asilimia 3.5 ya pato ghafi la taifa kugharamia ukatili wa kijinsia, serikali ya awamu ya tano haiwezi kuvumilia vitendo hivi kwa kuwa vinaathiri maendeleo," alisema.

Alitoa wito kwa wadau kutumia kampeni hiyo, kufanya tathmini maeneo yote yanayohusiana na vitendo vya ubakaji ili kubainisha kiwango cha tatizo hilo na kupendekeza mikakati ya kushughulikia suala hilo. Aliagiza walimu wakuu wa shule msingi na wakuu wa shule za sekondari nchini, kutoa idadi ya mimba kila baada ya miezi mitatu.

"Kuwapo kwa ukatili wa kijinsia nchini kunachangia taifa kutofikia uchumi wa kati wa viwanda kwa sababu nguvu kazi nyingi inapotea kwa kutofikia malengo yao," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa ya uhalifu wa kibinadamu iliyotolewa na Jeshi la Polisi kwa mwaka 2018, kati ya matukio 11,759, matukio ya ubakaji yalikuwa ni 7,617, sawa na asilimia 64.7.



# Rais atia saini miswada mitatu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MISWADA mitatu iliyopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika mkutano wa Septemba, mwaka huu, imetiwa saini na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na kuwa sheria kamili.

Hayo yalisema jana na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, katika kikao cha baraza la wawakilishi huko Chukwani.

Alisema miswada hiyo iliyotiwa saini na kuwa sheria kamili ni pamoja na marekebisho ya sheria namba 10 ya Kuweenzi Viongozi Wakuu wa Serikali.

Zuberi alisema muswada mwengine ni wa kuanzisha utawala wa Baraza la Wawakilishi na ule wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Sheria ya Mawakili.

Alisema kama zilivyo taratibu za Baraza la Wawakilishi, miswada hiyo ilipelekwa kwa Rais wa Zanzibar kwa ajili ya kupata baraka akiwa ni sehemu ya baraza hilo.

"Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi napenda kuwajulisha wajumbe kwamba miswada mitatu ya sheria iliyopitishwa na wajumbe sasa ni sheria kamili baada ya kutiwa saini na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi," alisema.



Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, akimsikiliza, Mwenyekiti wa Makampuni ya Kilimanjaro Fast Ferries na Azam Marine Said Salim Bakhressa wakiwa katika chumba cha kuongozea boti hiyo ya Kilimanjaro VII baada ya kuizindua jana. **PICHA: IKULU**

# Utatuzi mgogoro msikiti ngoma nzito

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Khamis Juma Mwalimu, amesema mgogoro wa Msikiti wa Suni Jamaat ulioko Ghofu, bado haujatatuliwa kutokana na pande zote mbili kushindwa kuaminiana na kujenga uadilifu.

Mwalimu alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua lini mgogoro wa msikiti huo utapatiwa ufumbuzi.

Alikiri kwamba mgogoro wa msikiti huo umechukua muda mrefu na vikao 10 vimefanyika kwa kuzikutanisha pande mbili zinazohusika.

Waziri alisema mgogoro huo umekuja baada ya eneo lililojengwa msikiti kuvunjwa makaburi ya watu waliozikwa hapo.

Hata hivyo, alisema suala hilo kwa sasa limepelekwa moja kwa moja katika Mahakama ya Ardhi kwa ajili ya kupata tafsiri ya nani mwenye umiliki halali wa ardhi ya eneo hilo.

"Mheshimiwa Spika, suala hili tumelipeleka katika Mahakama ya Ardhi ili kupata tafsiri sahihi nani mwenye umiliki halali wa eneo hilo," alisema.

Alisema mara baada ya kupata tafsiri sahihi kazi ya kuupatia ufumbuzi mgogoro huo utaendelea kwa ajili ya kuweka utulivu katika kufanya ibada. Mwalimu alisema serikali haifurahishwi hata kidogo kuona misikiti inatawaliwa na migogoro kwa waumini wake kiasi ya kuhatarisha amani na utulivu.

"Tutasimamia amani na utulivu katika nyumba za ibada na kuona kwamba migogoro haina nafasi tena kwani athari zake ni kuwagawa waumini," alisema.

## Zanzibar yajitosheleza kwa chakula na mboga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imesema imepiga hatua kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM kutokana na Zanzibar sasa kujitosheleza kwa chakula na mboga baada ya wakulima wengi kuhamasika.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Makame Ali Ussi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chake Chake, Suleiman Sarhani, aliyetaka kujua utekelezaji wa ilani katika uzalishaji wa chakula na mifugo umepata mafanikio kwa kiasi gani.

Aliyataja mafanikio hayo kuwa ni pamoja na kufikisha elimu kwa wakulima hadi vijijini hatua ambayo imesaidia wakulima kulima kwa njia za kisasa.

Pia alisema taasisi mbalimbali za utafiti zimeanzishwa ambazo zimefanya kazi kubwa katika utafiti wa chakula na mifugo.

Naibu Waziri huyo alisema uzalishaji wa chakula umeongezeka kwa asilimia 100 ikiwamo matunda ambayo mengi hivi sasa yanazalishwa Zanzibar tofauti na miaka ya nyuma yalikuwa yakiingizwa kutoka Tanzania Bara.

"Uzalishaji wa chakula umeongezeka pamoja na serikali kupunguza gharama za pembejeo kwa asilimia 75, hatua ambayo imeleta mafanikio makubwa," alisema.

Alisema serikali imejikita katika sekta ya uvuvi ikiwamo kuwawezesha wavuvi kuvua bahari kuu kwa kutumia boti za kisasa zenye uwezo wa kufika eneo hilo.

Naibu Waziri alisema tayari boti moja ya kisasa imewasili nchini na kwa sasa iko katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu kabla ya kuanza kazi za uvuvi bahari kuu.

Aidha alisema boti nyengine inatarajiwa kuwasili nchini na kuanza kazi za uvuvi katika eneo la bahari kuu.

"Tunataka kuona kwamba wavuvi wetu wanalifikiya eneo la bahari kuu lenye utajiri mkubwa wa hazina ya samaki," alisema.

# SMZ yapata gawio la bilioni 25/-

**Na Iddi Haji, Maelezo,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imepata faida zaidi ya Sh. bilioni 25 yakiwa ni malipo ya huduma za matumizi ya mkonga wa taifa, serikali mtandao Visiwani Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji Wakala wa Mkonga wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman, amesema kwamba fedha hizo zimelipwa kutoka katika kampuni ambazo zinatumia huduma zao.

"Tumepata fedha hizo ambazo kutoka Kampuni ya simu ya ZANTEL ikiwa ni malipo kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2024," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema kwamba serikali mtandao imekuwa na faida kubwa kwa wananchi ambapo sasa huduma za afya, kodi na elimu zimekuwa zikitolewa kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

Alisema katika sekta ya afya, kumekuwa na mafanikio makubwa katika huduma, vituo vya afya 24 Unguja na Pemba vimeunganishwa katia mfumo wa serikali mtandao.

"Leo hii mgonjwa anaweza kufanyiwa vipimo kama vya X-ray katika Hospitali ya Kivunge Mkoa Kaskazini Unguja na vipimo vile vitasomwa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja bila ya mgonjwa au daktari kulazimika kusafiri," alisema Mkurugenzi Mhandisi Shukuru.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kutumia huduma za serikali mtandao, huduma za vyeti vya kuzaliwa imekuwa rahisi kwa sasa kwani wananchi wanapata vyeti vya kuzaliwa katika wilaya zao.

"Sasa hivi Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar wanatumia huduma hizi, watu wanapata vyeti vyao vya kuzaliwa katika wilaya zao, wanaomba huko na taarifa zao zinatumwa Makao Makuu na kufanyiwa kazi," alisema zaidi Shukuru.

Mbali ya sekta hizo, pia Kampuni ya Uunganishaji Maudhui ya ZMUX inatumia mkonga wa taifa katika kurusha matangazo ya Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

Akizungumzia sekta ya kodi, Mkurugenzi Mtendaji huyo alisema kwamba Bodi ya Mapato Zanzibar ni moja ya watumiaji wakubwa wa huduma za serikali mtandao ambapo sasa huduma za kodi zimeunganishwa katika mtandao mmoja.

Alisema wamepokea maombi ya kampuni za simu, TTCL, na kampuni ya Comnet kutaka kutumia huduma za mkonga wa taifa.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano, Dk. Mzee Suleiman, alisema kumekuwa na mafanikio katika matumizi ya Tehama hasa baada ya kukamilika kwa mkonga wa taifa.

Dk. Mzee alisema mwaka 2011, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alitoa agizo la kuhakikisha Zanzibar inaongeza kasi ya matumizi ya Tehama katika shughuli mbalimbali. Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kuna vituo 10 vya kuwafundisha wananchi matumizi ya teknolojia ya Tehama, na kwamba mafunzo hayo yanatolewa bure kwa wananchi.



Meneja Mwandamizi wa Idara ya Biashara ya Kadi wa Benki ya NMB, David Ngusa (kulia) akimkabidhi zawadi ya fedha shilingi 50, 000 mshindi wa matumizi ya huduma mpya ya kulipia kupitia QR code & NMB mastercard, Dereva wa Bodaboda wa Kituo cha Makumbusho, Charles Kombole, aliyefanya miamala mingi kwakulipwa na mteja wake kupitia huduma ya MastaBoda. Washindi wa huduma hiyo walikabidhiwa zawadi zao katika vituo vyao vya kazi jijini Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bodaboda mkoa wa Dar es Salaam, Michael Masawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushauri kubadilishwa kwa sheria usalama barabarani

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI imeshauriwa kubadilisha Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, kwa kuongeza sheria na kanuni zitakazomlinda mtoto awapo katika vyombo vya usafiri.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti Mtendaji wa Shirika la Mtandao wa Watoto na Vijana Mwanza (MYCN), Shaban Maganga mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema sheria hiyo ya sasa bado ina mapungufu mengi hususani ukosefu wa masuala ya usalama wa watoto katika vyombo vya usafiri, hivyo ni muhimu kwa serikali kubadili sheria hiyo ili kumlinda mtoto dhidi ya ajali zinazotokea ambazo mara nyingi zimekuwa zikisababisha vifo au ulemavu wa kudumu.

"Sheria ya Usalama Barabarani Tanzania ya mwaka 1973, haijataja vizuizi/vifaa vya usalama vya watoto katika vyombo vya usafiri kama vile mikanda ya watoto au viti maalum vya watoto ambavyo husaidia kumkinga mtoto pale ajali inapotokea," alisema Maganga.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa shirika hilo, Baraka Mukama, alisema shirika hilo limekuja na mradi uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 160 kwa ajili ya kushawishi mabadiliko ya sheria ya usalama barabarani kwa kuhimiza matumizi ya vifaa vya usalama barabarani kwa watoto katika vyombo vya usafiri, ikiwamo magari binafsi, magari ya shule na mabasi yaendayo masafa marefu.

"Mradi huu utakuwa katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam na umejikita katika kuongeza mwamko kwa jamii katika masuala ya usalama barabarani. Jamii inapaswa kuelewa kuwa watoto wana haki ya msingi ya kulindwa hasa hasa katika masuala ya usalama barabarani," alisema.

Naye Hamadi Selemani, mjumbe wa bodi kutoka shirika hilo, aliiomba serikali kutilia mkazo suala hilo kwani imekuwa ikitumia gharama nyingi sana katika kulinda usalama wa mtoto kwa kutoa kipaumbele katika masuala muhimu ikiwamo afya na elimu ambapo huduma hizo ni bure kwa watoto, lakini ajali za barabarani zinaondoa watoto hao kabla ya kuwa watu wazima na kuanza kufanya kazi na kulipa kodi kwa serikali.

# Amana kuifuata serikali Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali kuhamia Dodoma, Benki ya Amana imeanza maandalizi ya kufungua tawi lake jijini humo mwanzoni mwa mwaka ujao.

Mkurugenzi wa benki hiyo, Dk. Muhsin Masoud, aliyasema hayo wakati wa hafla ya kusherehekea miaka minane ya benki iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi.

"Amana Benki inaendelea kukua na jitihada za kufikisha huduma zake maeneo mbalimbali ya nchi zinaendelea. Mwaka huu, tumefanikiwa kufungua tawi la tisa Zanzibar na maandalizi ya kufungua tawi la 10 mkoani Dodoma mwaka 2020 yanaendela," alisema.

Alibainisha kuwa kwa sasa, benki hiyo ina mawakala zaidi ya 400 maeneo mbalimbali kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa baadhi ya huduma zake.

Dk. Masoud alisema dira ya benki ni kuwa chaguo la kwanza na kiongozi katika utoaji huduma za kibenki zinazozingatia misingi ya kiislamu.

"Dira hii inafuatwa na dhamira ya kutoa huduma za kisasa na za kipekee kwa kuzingatia maadili kwa njia iliyo wazi kwa kupitia teknolojia za kisasa," alisema.

Aliongeza kuwa katika kupanua huduma zake, benki hiyo imeanzisha pia huduma ya kulipa ada za shule ili kutua mzigo huo kwa wazazi na walezi.

Dk. Masoud alisema elimu ni jambo la muhimu katika jamii hivyo wanaamini huduma hiyo itasaidia wazazi na walezi ambao wanakumbana na vikwazo katika kulipa ada.

Mkurugenzi huyo alisema utaratibu wa kutoa mkopo huo wa ada utahitaji masharti madogo ikiwa ni pamoja na shule anayosomea mtoto kumdhamini.

# RC aitwisha zigo Tarura

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MWENYEKITI wa kikao cha Bodi ya Barabara mkoani Rukwa, Joachim Wangabo, ameuagiza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), kuhakikisha barabara zilizopo chini ya mamlaka yao zinapitika licha ya mvua kubwa zinazonyesha mkoani humo.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua kikao cha kwanza cha bodi hiyo katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisema katika maeneo tofauti mkoani humo kumekuwa na mvua nyingi ambazo huenda zikasababisha baadhi ya barabara kukatika na madaraja kusombwa na maji, hivyo wajipange kwa kuhakikisha kuwa wanayafahamu maeneo hayo na kuyafanyia matengenezo ya mara kwa mara ili yasilete usumbufu kwa wananchi.

"Hivi sasa mvua zinanyesha na sitaki kusikia kuwa wananchi wanakosa mawasiliano kutokana na kukatika kwa barabara au daraja kusombwa na maji, hakikisheni mnayafanyia matengenezo maeneo hayo mara kwa mara ili wananchi wasipate shida hiyo," alisema Wangabo, ambaye ni mkuu wa mkoa huo.

## Miili 16 ya waliofariki katika lori yarejeshwa Uingereza

**LONDON,** Uingereza

MIILI ya Wavietnam 16 kati ya 39 waliofariki wakati wa usafirishaji haramu wa binadamu waliokuwa wamepakiwa katika lori kwenda Uingereza mwezi uliopita, imerejeshwa nyumbani kwao jana na imekabidhiwa kwa familia zao.

Miili hiyo iligunduliwa Oktoba 23, katika mji wa Grays nchini Uingereza, Mashariki mwa London.

Polisi walisema waliofariki wana umri kati ya miaka 15 na 44 na kati yao 31 wakiwamo wanawake wanane wanaaminika kuwalipa wasafirishaji hao wa binadamu kinyume na sheria ili kusafiri kwenda Uingereza. Watuhumiwa kadhaa wamekamatwa nchini Uingereza na Vietnam.

Miili hiyo iliwasili kwa ndege mjini Hanoi, mji mkuu wa Vietnam na tovuti ya habari ya shirika la VNExpress ilichapisha picha za magari ya wagonjwa ambayo yalisafirisha miili hiyo kwenda katika jimbo la kusini mwa Hanoi. **DW**

## Namibia waanza kupiga kura

**WINDHOEK,** Namibia

UPIGAJI kura umeanza nchini Namibia jana katika uchaguzi wa kumchagua Rais na wabunge wakati hali ngumu ya maisha na kashfa za rushwa zinaweza kuwa changamoto kwa chama tawala kupata viti vingi vya ubunge.

Taifa hilo lenye wakazi wachache, limekuwa likitawaliwa na chama cha South West Africa People's Organisation Swapo, tangu nchi hiyo kupata uhuru kutoka Afrika Kusini mwaka 1990.

Rais Hage Geingop, ambaye anawania kuchaguliwa tena baada ya muhula wake wa kwanza kukumbwa na mdororo wa kiuchumi na kuchochea hasira dhidi ya chama cha Swapo, alikuwa wa kwanza kupiga kura katika shule ya msingi katika mji mkuu Windhoek, Namibia.

Alieleza kujiamini kuwa atashinda, lakini amesema iwapo hatashinda atakubali matokeo, kwa kuwa yeye ni muumini wa demokrasia.

"Hii sio vita, na huu siyo mwisho wa dunia. Tunatimiza tu haki yetu ya kidemokrasia," aliwaeleza waandishi habari nje ya kituo cha kupigia kura.

Lakini mwanachama wa Swapo ambaye anagombea kama mgombea huru wa kwanza nchini humo, daktari wa zamani wa meno Panduleni Itula (62), ameungwa mkono na vijana wasio na ajira. **DW**

# Rais Trump aalikwa kusikiliza tuhuma

**WASHINGTON DC,** Marekani

BUNGE la Congress nchini Marekani limemualika Rais wa Marekani, Donald Trump, katika kikao chake kitakachosikiliza tuhuma zinazomkabili kitakachofanyika Desemba 4, mwaka huu.

Mwenyekiti wa chama Kamati ya Congress ya masula ya sheria kutoka Chama cha Democratic, Jerrold Nadler, alisema kuwa Trump anaweza kuhudhuria na kuwahoji mashahidi.

Alisemaa kikao hicho kitawezesha kuanzishwa kwa hatua nyingine katika mashtaka, yanayomhusisha na Rais wa Ukraine Volodymyr, ambaye Rais Trump alimpigia simu.


**Kamati ya masuala ya ujasusi ilikamilisha wiki mbili za kusikiliza, kufuatia wiki kadhaa za vikao vya faragha vya kuwahoji mashahidi.**

Katika mawasiliano ya simu hiyo, Rais Trump alimtaka Zelensky amchunguze Joe Biden, ambaye kwa sasa ndiye mgombea aliye mstari wa mbele kuwania kiti cha urais kwa tiketi ya Chama cha Democratic katika uchaguzi wa urais mwakani, na mtoto wake wa kiume Hunter Biden, ambaye awali aliwahi kufanya kazi kampuni ya nishati ya Ukraine Burisma.

Uchunguzi unataka kubaini, ikiwa Rais Trump alitumia tishio la kuzuia msaada wa Jeshi la Marekani kwa Ukraine ili kuifanya imchunguze Biden na mwanaye. Rais Trump amekana kufanya kosa lolote na ameutaja uchunguzi kuwa ni "hila".

Wiki iliyopita, Kamati ya masuala ya ujasusi ilikamilisha wiki mbili za kusikiliza, kufuatia wiki kadhaa za vikao vya faragha vya kuwahoji mashahidi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ujasusi, anayeongoza uchunguzi huo, Adam Schiff, alisema kamati za masuala ya kigeni na intelijensia - sasa zinaifanyia kazi ripoti yao, ambayo itatolewa Desemba 3, mwaka huu. **BBC**



Rais Uhuru Kenyatta wa Kenya akiwa na Raila Odinga. **PICHA: MTANDAO**



## Benki na majengo vyachomwa moto

**TEHRAN,** Iran

TAKRIBAN benki 731 na majengo ya serikali 140 yamechomwa moto katika ghasia za hivi karibuni nchini Iran, Waziri wa Mambo ya Ndani Abdolreza Rahmani Fazli, alisema katika taarifa zilizochapishwa na shirika rasmi la habari la nchi hiyo IRNA jana.

Alisema zaidi ya vituo 50 vilivyotumiwa na majeshi ya usalama vilishambuliwa na kiasi ya vituo 70 vya kuuzia mafuta vilichomwa moto, bila ya kutoa ufafanuzi mashambulio hayo yalikofanyika.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Iran IRNA, Rahmani Fazli pia alisema zaidi ya watu 200,000 walishiriki nchi nzima katika machafuko hayo yaliyoanza Novemba 15 baada ya tangazo la ongezeko la bei ya mafuta.

Shirika la kutetea haki za binadmu la Amnesty International lenye makao yake mjini London limesema siku ya jumatatu limerekodi kiasi waandamanaji 143 waliouawa katika maandamano, machafuko mabaya ya kuipinga Serikali nchini Iran tangu Jeshi la Polisi kuzima maandamano ya mapinduzi ya kijani mwaka 2009 yaliyokuwa yakipinga udanganyifu katika uchaguzi. **DW**

# Kampuni 32,000 zanufaika biashara nje

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara ya Tanzania (TanTrade), kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli, imezisaidia kampuni 31,891 kupatiwa taarifa za kibiashara kuhusu bei na masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi.

Kati yao wafanyabiashara 405 waliunganishwa na masoko na kuuza tani 102,000 za mahindi, tani 2,000 za karanga, 5,000 za soya, 50 za ufuta, saba za majani ya mpapai, kilo 200 za unga wa ubuyu, mbili za iliki, 5,000 za muhogo na 3.2 za tangawizi ya unga.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade, Latifa Khamis, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia utendaji wa miaka minne ya uongozi wa Rais John Magufuli.

Alisema miongoni mwa bidhaa zilizoonyesha uhitaji mkubwa katika masoko ya nje ni pamoja na matunda, samaki na mazao ya bahari (mwani), jamii ya mikunde, asali, kahawa, chai, korosho, viungo na vyakula.

Khamis alisema mauzo hayo yalitoka katika nchi za India, ukanda wa kusini mwa Afrika, China, Japan, Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Falme za Kiarabu, Misri, Marekani, Vietnam na Ulaya.

"Mbali na kusambaza taarifa za uhitaji wa bidhaa mbalimbali TanTrade kwa kushirikiana na wanunuzi kutoka nchi mbalimbali iliratibu semina za kutangaza fursa za biashara katika nchi zao ikiwa ni muendelezo wa kimkakati wa kupenya katika masoko yao," alisema Khamis.

Alisema katika semina mbalimbali zilizoratibiwa, wafanyabiashara na wadau 425 walishiriki ili kutambua fursa za masoko ya nje na taratibu za kuyafikia masoko hayo katika nchi za Uswidi, Ufaransa, Ukraine, China na Rwanda.



Picha ya pamoja ya wanafunzi wanaocheza Kung-Fu (CHISHAKU), baada ya kumaliza mtihani wa mafunzo ya 12 ya mchezo huo katika viwanja vya Chuo Kikuu cha Ardhi, jijini Dar e Salaam. Waliosimimama watatu kulia ni masta wa mafunzo hayo, Hussein Hwago na kulia ni Jimson Mswayoga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu wataja chanzo cha upangaji holela miji

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

MWENYEKITI wa Bodi ya Usajili wa Wataalamu wa Mipango Miji, Prof. Wilbert Kombe, amesema tofauti kubwa kati ya mipango ya kiuchumi na ile ya maendeleo ya ardhi ni chanzo kikubwa cha kutokuwapo miji iliyopangika.

Prof. Kombe alisema hayo jana katika mahojiano maalum wakati wa kikao cha siku tatu cha wataalamu wa mipango kinachoendelea jijini Dodoma.

Alisema kwa sasa mipango, sera na utekelezaji kuhusu masuala ya mipango miji vipo lakini tatizo kubwa ni tofauti katika mipango ya kiuchumi na maendeleo kwenye sekta ya ardhi kwa ujumla.

Kombe aliongeza kuwa tatizo lingine linalochangia suala hilo ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusiana na manufaa wanayoweza kuyapata katika ardhi iliyopangwa

"Mtu ukipanga ardhi yako unaongeza thamani hata kabla haijaongezewa huduma nyingine kama vile maji na umeme ndyo maana kuna tofauti kubwa kati ya anayeuza ardhi iliyopangwa na yule ambaye haijapangwa," alisema Prof. Kombe.

Alihimiza uwapo wa ushirikiano baina ya serikali na sekta zingine katika masuala mbalimbali yanayohusu upangaji miji ili kuepuka kuwa na maeneo yasiyopangwa ambayo husababisha kuwa na makazi holela.

Msajili wa Bodi ya Wataalamu wa Mipango Miji, Hellen Mtutwa, alisema mkutano wa wataalamu wa mipango miji unaoendelea unawakutanisha wataalaumu wote wa sekta hiyo kutoka serikalini na sekta binafsi ili kuboresha mipango miji nchini.

Pia alisema ushirikishwaji wa sekta mbalimbali katika mipango miji ya maeneo mbalimbali nchini si tu utarahisisha upangaji miji bali utaepusha hasara kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa City Plan Consultants (T) Limited, Dk. Juma Mohamed, aliiomba serikali kuipa kipaumbele mipango ya maendeleo ya ardhi kwa kuwa ardhi ndiyo kila kitu husuan katika masuala yanayohusu shughuli za binadamu.

Dk. Mohameda alisema tatizo kubwa kwa wananchi wengi ni kutegemea matokeo ya haraka kwenye sekta hiyo wakati suala hilo linaweza kuhitaji mipango ya muda mrefu hasa katika masuala ya mipango kabambe.

# Wanaojenga kando mito, maziwa, bahari kukiona

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewaonya watu wote waliojenga na wanaoendelea kujenga kwenye fukwe ya mito, maziwa na bahari bila kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana,

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hali hiyo imekuwa ikijitokeza maeneo mbalimbali nchini na kuonya watu kuacha tabia hiyo mara moja kabla ya kukabiliana na mkono wa sheria.

""NEMC inaagiza wote wanaojenga sehemu za fukwe ni vizuri wakatumia Ofisi za NEMC zilizopo katika kanda zate nchini ili kufanya EIA kwani majengo mengi hayana mifumo mizuri ya majitaka na wamekuwa wakiyaelekeza baharini au ziwani," alisema.

Dk. Gwamaka alisema NEMC imejipanga kuwatawanya wataalum wake katika maeneo mbalimbali ya fukwe kufanya ukaguzi na endapo watabaini ukiukwaji wa sheria na kanuni za mazingira basi hatua kali za kisheria ikiwamo faini ya Sh. milioni thelathini itatolewa kwa mhusika au kufikishwa mahakamani.

"Katika maeneo hayo sheria inawataka watu wasijenge ndani ya mita 60, lakini majengo mengi yamejengwa ndani ya mita hizo, hivyo wataalamu wetu watazunguka na kwa watakaobainika watalazimika kufuata sheria hiyo," alieleza Dk. Gwamaka.

Aliongeza kuwa NEMC imeamua kufanya kazi bila kuangalia

cheo au umaarufu wa mtu yeyote ambaye anakwenda kinyume cha sheria, kanuni na taratibu zote zinazoongoza mazingira.

"Tunajua ni kwa namna gani uwekezaji katika maeneo ya fukwe zetu unavyoliingizia taifa letu mapato na kutengeneza ajira kwa Watanzania, lakini hiyo isiwe sababu ya kuathiri mazingira yetu ambayo ni urithi na hazina ya vizazi vilivyopo na vijavyo," alisema.

"Tukikuta ukiukwaji wa mazingira faini yetu ni milioni 30, hivyo tunawaomba wahusika waweke miundombinu yao vizuri kabla mkondo wa sheria haujachukua nafasi yake," alisema na kuongeza kuwa NEMC kuchukua hatua stahiki.

Aidha Dkt. Gwamaka alieleza madhara ya kuelekeza maji taka baharini yanaathiri viumbe hai vya maji-ni pamoja na binadamu wanaotumia maji hayo kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kunywa na kupikia.

"Athari zinazotokana na ujenzi holela na usiozingatia tathmini ya athari ya kimazingira unachangia madhara makubwa kwa viumbe hai vya majini na binadamu hivyo ni vyema NEMC ikasimamia nguvu zote," alisema.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA /MASHAMBA

**IWANJA KINAUZWA**

PO CHANIKA BUYUNI PLOT 256, QM 947 BLOCK 14. HATI IPO EI NI SHILINGI MILIONI 14. KWA AWASILIANO: 0743 113 138 / 757 305 222.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311

N THE DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.91 OF 2019
In the matter of the Estate of the LATE
JASSON MWAKAJWANGA
And
In the matter of the Application for letters of
Probate and Administration of estate by
MTUMWA LADISLAUS LIPINGU

**GENERAL CITATION**
(Rule 75 of Probate Rules GN No. 369 of 1963)

ll persons claiming to have any interest in the Estate of the ove named deceased are hereby cited to come and see the oceedings if they think fit before the grant of probate (or tters of Administration) is made to the above named etitioner.

bjections to the grant should be filed on or before 16th day Dec 2019.

esented for filling this 27 day of November, 2019

115535602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CHRISTINE STEPHEN SHEKIDELE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 991 ABD TOYOTA PICK-UP HILUX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/509417/2019.**

115534902




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

nu: +255 26 2324455
x: +255 26 2323233
rua Pepe: ps@mow.go.tz
vuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 18/04/2019

## TANGAZO

. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 29/11/2019 kampuni ya **ESTIM CONSTRUCTION COMPANY LTD** inatarajia kusafirisha mashine (wheel loader) kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **LUGOBA** kutumia barabara ya **MOROGORO, CHALINZE SEGERA** kupitia **VIGWAZA.** Gari hilo lenye namba za usajili: **T 595 AZB/ T 106 AYZ**

. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 20 |
| Upana | - | mita | 3.00 |
| Kimo | - | mita | 4.8 |

. Njia itakayotumika: **MOROGORO, CHALINZE SEGERA,** kupitia **VIGWAZA hadi LUGOBA.**
Gari zitasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115535702

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No; 242/2019

Ombi la UWESU SAID YUNGI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SIHIANA ABDALAH KITWANGA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 26/11/2019

115535302

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BID-

HAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KANE AVUNJA REKODI YA DEL PIERO UEFA




**LONDON,** England

HARRY Kane amekuwa mchezaji aliyefunga kwa haraka zaidi mabao 20 kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kane alifunga mara mbili wakati Tottenham ikitoka nyuma ya mabao mawili na kushinda 4-2 dhidi ya Olympiacos ukiwa ni mchezo wa kwanza kwa kocha Jose Mourinho akicheza nyumbani tangu achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo, na akifuzu kwenye hatua inayofuata.

Nahodha huyo wa England, Kane, bao lake la 20 alifunga ukiwa ni mchezo wake wa 24 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiipiku rekodi iliyowekwa na Alessandro Del Piero aliyefunga katika mechi 26.

Mshambuliaji huyo amefunga mara saba katika mechi nne zilizopita kwa klabu yake na nchini yake yalitosha kumfanya aweke rekodi ya kufunga mabao 20 kwa haraka zaidi.

"Siyo mchezaji mbaya kumpita," alisema Kane akiiambia BT Sport wakati alipozungumzia kuhusu kuivunja rekodi hiyo ya mchezaji wa zamani wa Italia, Del Piero.

"Lilikuwa suala la kufuzu, bila kujali tulifanyaje tulitakiwa kushinda na tulishinda.

"Tunafurahia na kujaribu kuendelea na kasi hii kwenye mechi ya ligi Jumamosi.

"Sasa tunarudi kwenye Ligi Kuu kwa kasi zaidi, kwani tunatakiwa kupata pointi tatu katika kila mchezo wa ligi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi."

Mourinho mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu nyumbani utawakutanisha Spurs na Bournemouth na utachezwa Jumamosi.

# Fernandes aamua kujifunga Sporting

**LISBON,** Ureno

NAHODHA wa Sporting CP, Bruno Fernandes amemaliza uvumi juu ya majaliwa yake baada ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Ureno.

Fernandes mwenye umri wa miaka 25, amekuwa akiripotiwa kuwaniwa na miamba wa Ligi Kuu England, Manchester United pamoja na Tottenham na Real Madrid ya Hispania.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ureno, mkataba wake umeripotiwa kwamba, ulikuwa ukimalizika mwaka 2023, ingawa kulikuwa na kipengele cha kuuzwa kwa euro milioni 100.

Fernandes alitajwa kuwa mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu Ureno, Primeira Liga, kwa misimu miwili mfululizo, baada ya kujiunga na Sporting kutoka Sampdoria mwaka 2017.

"Kwa upande wangu najisikia fahari kubwa na inaonyesha utambulisho mzuri, ni ishara kwamba, ninafanya vizuri," amesema Fernandes akiiambia tovuti ya Sporting.

"Nimekuwa nikifanya kila kitu kinachowezekana kujaribu kuwa kwenye ubora wangu kuisaidia klabu.

"Mkataba mpya ni kwa sababu ya kile nilichokifanya uwanjani, lakini inaonyesha kwamba, napenda kuwa hapa Sporting na najisikia fahari kuiwakilisha klabu hii."






# *Lewandowski: Nimeathirika na kupenda kufunga mabao*

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski amedai kwamba, 'ameathirika' na kupenda kufunga mabao wakati alipoingoza Bayern Munich kuibuka na ushindi wa 6-0 dhidi ya Red Star Belgrade kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Lewandowski alikuwa kwenye wakati mzuri Jumanne hiyo na kufunga mabao manne ndani ya kipindi cha pili kwenye Uwanja wa Rajko Mitic.

Jitihada zake ziliifanya timu hiyo kushinda mechi nne mfululizo, huku akifunga mabao 16 na hawajaruhusu bao chini ya kocha wa muda, Hans-Dieter Flick.

Na kwa mujibu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ameathirika na kupenda kufunga kwenye kila mechi.

"Lazima nikiri... nimeathirika na kupenda kufunga mabao," alisema Lewandowski ambaye tayari amefunga mabao 27 katika mechi 20 alizocheza kwenye mashindano yote msimu huu.

Aliongeza akiiambia Sky Sport: "Jambo la muhimu ni jinsi tulivyocheza vizuri, tulilinda vizuri, tulifurahia, bila kujali tulichezaje, tulifuata mpango wetu."

# Tuchel: Sina hofu ya kumpoteza Neymar

**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amesema alimweka benchi Neymar kwa ajili ya manufaa ya mchezaji mwenyewe kwenye mchezo dhidi ya Real Madrid na hakuhofia kumkwaza mchezaji huyo.

Neymar, ambaye alianza kwenye mchezo wa Ijumaa iliyopita dhidi ya Lille, alimwingiza kipindi cha pili wakati wakitoka sare ya kufungana mabao 2-2 juzi Jumanne jijini Madrid.

PSG walianza kufungwa kwa mabao ya Karim Benzema kabla ya Kylian Mbappe na Pablo Sarabia kusawazisha.

Tuchel alibainisha kwamba aliamua kumtumia kwa muda mfupi Neymar ili asipate maumivu baada ya kutoka kupona hivi karibuni.

"Hapana, sikuhofia kumkwaza, sidhani kama tutampoteza Neymar," alisema Tuchel baada ya mchezo huo.

"Ilikuwa ni kwa sababu ya manufaa kwa mchezaji mwenyewe, hatuna tatizo na hilo. Nilizungumza nae na nilimwambia ataanzia benchi. Tulifanya hivyo hivyo kwa Kylian kwenye mchezo dhidi ya Galatasaray.

"Amekuwa nje ya uwanja kwa wiki sita, alicheza mchezo mmoja tu na kwa upande wangu sikutaka kuhatarisha afya yake."







# MOURINHO AMWOMBA RADHI ERIC DIER

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, ameomba radhi kwa Eric Dier kwa kumtoa uwanjani kwa sababu ya mbinu zake za kusaka ushindi katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Olympiacos ya Ugiriki juzi Jumanne.

Mchezo huo ulikuwa wa kwanza kwa Mourinho nyumbani tangu alipochukua nafasi ya Mauricio Pochettino kwa miamba hao wa London wiki iliyopita.

Lakini Spurs walikuwa nyuma kwa mabao 2-0 mapema na kocha huyo akaamua kumtoa Dier na nafasi yake kuchukuliwa na Christian Eriksen katika dakika ya 29.

Kwa miaka mingi, Mourinho amekuwa hana desturi ya kufanya mabadiliko ya wachezaji mapema na amekuwa tayari kufanya mabadiliko mara chache kipindi cha kwanza kama mchezo unaonekana kuwa mgumu kwake.

Safari hii mambo yalionekana kwenda vizuri kwa upande wake na Dele Alli akaanza kwa kufunga bao la kwanza kabla ya mapumziko, kabla ya Harry Kane na Serge Aurier wakafunga na kufanya matokeo kuwa 4-2.

Na baada ya mchezo huo, Mourinho alisema aliamua kumtoa mapema Dier ikiwa ni sehemu ya mbinu ya mchezo huo.

"Wakati mgumu zaidi kwenye mchezo haukuwa tu kwa namna walivyofunga mabao mawili, ulikuwa ni pale nilipofanya mabadiliko kipindi cha kwanza," alisema Mourinho akiiambia Sky Sports.

"Ilimuumiza mchezaji na pia mimi mwenyewe. Sio rahisi kwangu mimi na kwa mchezaji mwenyewe," alisema.



# Guardiola afikiria ubingwa EPL

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola sasa ameelekeza nguvu zake kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England wakati Manchester City ikiwa imefuzu kucheza hatua ya mtoano wa timu 16 katika Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya sare ya kufungana 1-1 na Shakhtar Donetsk, juzi Jumanne.

Pointi moja ilitosha kwa mabingwa hao wa England kufuzu kwenye hatua hiyo wakiwa vinara wa Kundi C na shukrani zaidi kwa Atalanta kuifunga Dinamo Zagreb.

City ilianza taratibu kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Etihad, lakini walipata bao la kuongoza kupitia kwa Ilkay Gundogan dakika ya 11 kipindi cha pili, na Manor Solomon akasawazisha.

Licha ya kikosi chake kutokuwa kwenye kiwango cha kuvutia, ikitoka sare mfululizo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Guardiola sasa ana furaha ya kufuzu hatua ya mtoano na akili yake ipo kwenye mbio za Ligi Kuu England.

"Tumefuzu na tulicheza vizuri zaidi kipindi cha pili," alisema Guardiola, ambaye ameshinda mechi tisa kati ya 12 dhidi ya Shakhtar, akiiambia BT Sport.

"Kipindi cha pili kilikuwa bora zaidi kuliko cha kwanza. Tulihitaji mashambulizi machache ya kushtukiza."

"Katika kipindi cha kwanza hatukuwa na haraka na tulicheza taratibu, lakini kipindi cha pili tuliimarika na kuweza kuonyesha kiwango bora."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SANTO AKARIBIA KUTUA ARSENAL

**Ni baada ya siku za Emery kuhesabika katika klabu hiyo ambayo msimu huu...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Wolves, Nuno Espirito Santo, anatajwa kuwa katika nafasi ya kwanza ya kurithi mikoba na Unai Emery ya kuiongoza Arsenal.

**Hatima ya Emery katika kikosi cha Gunners iko katika hali ya sintofahamu baada ya klabu hiyo kuanza vibaya kwenye msimu huu unaoendelea.**

Mhispania huyo amekuwa akifuatiliwa kwa kufanyiwa tathmini ya mchezo kwa mchezo na tayari Mkuu wa Kitengo cha Michezo cha klabu hiyo, Raul Sanllehi, huku ikielezwa pia ana uhusiano wa karibu na wa muda mrefu na wakala wa Nuno, Jorge Mendes.

Pia Mauricio Pochettino ambaye ameondoka Tottenham, naye anatajwa kuhusishwa na klabu nyingine za jijini London.

Lakini Nuno anatajwa wazi kwanza ameivutia Arsenal kutokana na kazi nzuri aliyoionyesha katika muda wote ndani ya kikosi cha Wolves.

Kocha huyo raia wa Ureno mwenye umri wa miaka 45, ameiongoza Wolves kutwaa taji la Championship miaka miwili iliyopita na uwezo aliouonyesha kwa kuifanya timu hiyo kumaliza kwenye nafasi ya sana katika Ligi Kuu England msimu uliopita.

Kwa kumaliza kwenye nafasi hiyo, Wolves ilipata tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Europa League, lakini kutokana na changamoto ya ratiba kwenye mashindano hayo, iliangukia kwenye kupambana kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Lakini ilijiondoka kwenye hatari hiyo na sasa iko kwenye nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuanza kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Europa.

Mashabiki wa Arsenal wanautaka uongozi wa timu hiyo kumtimua Emery kutokana na kikosi chao kuonekana kuelemewa katika mchezo uliochezwa Jumamosi baada ya kupambana kupata bao la kusawazisha katika dakika za lala salama kupitia Alexandre Lacazette, wakiwa nyumbani mchezo uliomalizika kwa sare ya magoli 2-2 dhidi ya Southampton.

Hata hivyo, Arsenal wanaamini kuwa kuajiri kocha katikati ya msimu kunaweza kuwaletea matatizo zaidi na hivyo wanahitaji kusubiri hadi msimu utakapomalizika.

Kutokana na uamuzi huo, Gunners huenda ikaamua kumtumia kocha Freddie Ljungberg na mkuu wa akademi yao, Steve Bould, kuiongoza timu hiyo mpaka katika kipindi cha majira ya joto mwakani, ambapo mrithi wa Emery, atakuwa amepatikana.

## ZISIKUPITE

### BARCA, MADRID VITANI

KLABU za Barcelona na Real Madrid ziko tayari kufanya mchakato wa kumsajili straika wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Mirror)***

### AUBAMEYANG ANUKIA BARCA

MABINGWA wa Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga, klabu ya Barcelona imetajwa inaongoza katika mbio za kuwania saini ya straika wa Timu ya Taifa ya Gabon na Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang (30). ***(Star)***

### JESUS KUTUA EVERTON

EVERTON inajipanga kumwajiri Kocha wa Flamengo, Jorge Jesus ili kuchukua nafasi ya Marco Silva. Jesus aliiongoza klabu hiyo ya nchini Brazil kuchukua ubingwa wa Copa Libertadores. ***(Telegraph)***

### MANCHESTER UNITED YA SANCHO

MANCHESTER United inaamini kuwa wao ndio klabu pekee waliobakia katika mbio za kuwania saini ya mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19). United imepanga kuwa na mchezaji huyo katika msimu ujao mwakani. ***(Telegraph)***

### STERLING KUIKAMUA CITY

MKATABA mpya wa mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, aliopewa na Manchester City utamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kupokea zaidi ya pauni 350,000 kwa wiki na kumzidi nyota Kevin de Bruyne, ambaye alikuwa analipwa pesa nyingi zaidi klabuni hapo. ***(Sky Sports)***

### BAYERN, SANE WATETA

WAKALA wa winga wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leroy Sane amekutana na mabosi wa Bayern Munich, lakini viongozi wa mabingwa hao wa Bundesliga wamesema watasubiri hadi katika kipindi cha majira ya joto mwakani ili kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Goal)***

### JONES AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United, Tottenham na Liverpool ni baadhi ya klabu zilizojitokeza kuwania saini ya straika chipukizi wa Peterborough United, Ricky-Jade Jones, ambaye ni raia wa England. ***(Mail)***

### BAYERN YAMKATAA POCHETTINO

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, ametajwa kuwa si chaguo la Bayern Munich, ambayo imeweka wazi kwamba Kaimu Kocha Hansi Flick, ataendelea kukiongoza kikosi hicho hadi mwisho wa msimu. ***(Goal)***

### POGBA AMVURUGA ZIDANE

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ameendelea "kuvurugwa" kutokana na changamoto ya kumsajili kiungo wa Manchester United Mfaransa Paul Pogba, licha ya Rais Florentino Perez, kumpa uhuru wa kumsajili nyota wa Tottenham, Christian Eriksen (27) au Mhispania Fabian Ruiz anayeichezea Napoli. ***(Mirror)***

### KOCHA AMTAMANI HAALAND

KOCHA wa Red Bull Salzburg, Jesse Marsch, anaamini straika wake raia wa Norway, Erling Haaland (19), atabakia katika klabu hiyo hadi ifikapo mwisho wa msimu. ***(CNN, via Manchester Evening News)***

# MIRAJI AJIPANGA KUFANYA MAKUBWA SIMBA, STARS

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Miraji Athumani "Sheva", ameahidi kuendelea kujituma zaidi ili kuisaidia klabu yake kutimiza malengo ya kutetea taji hilo wanalolishikilia hapa nchini.

**Miraji ambaye amerejea Simba akitokea Lipuli FC ya mkoani Iringa, amewataka mashabiki wa timu hiyo kwamba wasiwe na wasiwasi na timu yao licha ya ushindani uliopo katika msimu huu.**

Akizungumza na gazeti hili jana, baada ya mazoezi ya asubuhi yanayoendelea kwenye viwanja vya Gymkhana, Miraji alisema Ligi Kuu msimu huu ina ushindani ambao umetokana na kila timu kujipanga vizuri ili kujiepusha na janga la kushuka daraja.

"Nitaendelea kujituma ili kuifikisha mbali timu yangu kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu, naomba mashabiki wangu wazidi kunipa ushirikiano," alisema mchezaji huyo.

Miraji aliongeza kuwa anatajiria kuongeza umakini na kufuata malekezo kutoka kwa makocha wake kwa sababu bado anahitaji kutimiza ndoto za kwenda kucheza nje ya Tanzania.

"Kikubwa ni kumsikiliza mwalimu kwa makini tunapokuwa mazoezini hiyo ndio itanifanya nizidi kuwa bora zaidi, ndani ya klabu na kwenye Timu ya Taifa," alisema mchezaji huyo.

Aidha, alisema lengo lake ni kuona kipaji chake kinaendelea kuimarika na anaamini hilo linawezekana.

Mshambuliaji huyo sasa ameshafunga mabao sita katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajia kusimama kupisha mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati ambayo yatafanyika kuanzia Desemba 7 hadi 19, mwaka huu jijini Kampala, Uganda.




Wachezaji wa Azam FC, Shabani Chilunda (kulia) na Nicholas Wadada, wakishangilia bao la tatu la timu hiyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC iliyochezwa juzi jijini Mwanza. Azam ilishinda mabao 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# *Cheche ahitaji mabao zaidi Azam*

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya wenyeji Alliance FC, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema siri kubwa ya wao kupata matokeo hayo ni kucheza kwa kiwango cha juu, huku pia ikifurahia uwanja wa nyasi bandia ambao waliutumia katika mchezo huo.

Katika mchezo huo, mshambuliaji Mzambia Obrey Chirwa alifunga hattrick wakati Shabani Chilunda yeye alifunga mabao mawili.

Kufuatia ushindi huo, Azam FC ambayo imecheza mechi tisa, imefikisha pointi 19 na kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara inayoongozwa na Simba wenye pointi 25, wamepanda hadi katika nafasi ya nne.

Akizungumza na gazeti hili, Cheche, alisema kuwa wachezaji wake wamefuata maelezo kwa kiwango cha juu, lakini bado anahitaji kuwaimarisha zaidi na kutumia vema nafasi zote wanazotengeneza.

Cheche alisema kama wachezaji wake wangetumia nafasi zote walizotengeneza na kuongeza umakini, wangeondoka na ushindi mnono zaidi ya huo walioupata hapo juzi.

"Tunashukuru wachezaji wamefuata kile tunachokieleza mazoezini, leo (juzi) kwa kiasi kikubwa wachezaji wamefuata maelekezo, wamefanya asilimia 70 ya maelekezo tuliyowapa, lakini kama wangeongeza utulivu, wangestahili kupata mabao mengi zaidi, walionekana kuridhika, siku zote unapopata nafasi unatakiwa uitumie vema, hata kama ni kufunga mabao 50, hii ni kumtisha mpinzani anayekuja," alisema Cheche.

Aliongeza kuwa bado wanahitaji kuwaimarisha zaidi na kutoridhika na mabao wanayofunga kwa sababu wanahitaji pia kuweka rekodi.

"Nawapongeza pia vijana wangu, wametumia vizuri nafasi walizopata tofauti na michezo iliyopita, walikuwa hawawezi kufanya kama walivyofanya katika mchezo huu," Cheche aliongeza.

Kikosi cha Azam kilirejea jijini Dar es Salaam juzi usiku tayari kuendelea na maandalizi ya mchezo wao unaofuata wa ligi hiyo.

## Suluhu kuzindua Shimmuta Mwanza

**Na Shufaa Lyimo**

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu (pichani), anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa mashindano ya Shimmuta utakaofanyika Novemba 30, mwaka huu jijini Mwanza, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Shimmuta, Khamisi Mkanachi, alisema licha ya uzinduzi kufanyika siku hiyo, tayari mashindano hayo yalianza kufanyika jana baada ya wanamichezo wanaoshiriki kuwasili kwa wakati kama ilivyopangwa.



"Uzinduzi rasmi wa mashindano yetu utafanyika Novemba 30, lakini leo (jana), ndio mashindano yameanza, maandalizi yalikwenda vema na sasa tunasubiri siku ya uzinduzi, tunashukuru mwitikio umekuwa mkubwa sana tofauti na mwaka jana," alisema Mkanachi.

Aliongeza kuwa mwitikio wa mwaka huu umekuwa mkubwa kutokana na idadi ya kampuni zinazoshiriki ambazo zimechangia ushindani.

"Mwaka jana Dodoma tulikuwa na kampuni 26, lakini mwaka huu tumepata idadi ya kampuni 45," alisema kiongozi huyo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Shimmuta, Roselyne Massam, alisema kuwa amefurahishwa na mwitikio mkubwa ulioonyeshwa katika siku ya kwanza ya mashindano hayo hapo jana.

## Zanzibar Heroes yaanza majigambo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa timu ya soka ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), Ali Mtuli, amesema hawana wasiwasi na mashindano ya Kombe la Chalenji, kwa sababu kundi ambalo wamepangwa katika michuano hiyo inayotarajia kufanyika kuanzia Desemba 7 hadi 19 mwaka huu, ni la kawaida.

Zanzibar Heroes imepangwa katika Kundi C pamoja na ndugu zao Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), Djibouti na mabingwa watetezi, Kenya (Harambee Stars).

Mtuli alisema kuwa wanajiandaa kufanya vema katika mashindano hayo kwa sababu timu walizopangwa nazo, wameshawahi kukutana na kuwafahamu wachezaji wao.

"Hatuna mashaka na timu ya Kenya wala Tanzania Bara, kwa sababu tumeshawahi kukutana, tunawajua aina ya uchezaji wa timu hizo pamoja na uzoefu wao," alisema Mtuli.

Kocha huyo alimtaja Abdallah Sebo kuwa ndiye mchezaji pekee anayecheza katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambaye amesharipoti kwenye mazoezi ambayo yanafanyika kwenye viwanja vya Amaan na Mao.

# Michezo

Alhamisi Novemba 28, 2019

Nipashe





Santo akaribia kutua Arsenal UKURASA 30

ZUIA...




Kiungo wa Manchester City, Bernardo Silva (kushoto), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Shakhtar Donetsk, Ismaily katika mechi ya Kundi C ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, ALLIANCE WATAMBIANA

## ●●● Kila timu yajipanga kuingiza kikosi imara katika mchezo huo utakaochezwa kesho...

**Na Somoe Ng'itu**

MAPAMBANO yanaendelea! Hayo ni maneno ya Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Alliance FC, unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

**Tayari kikosi cha Yanga kikiwa na wachezaji wake 18 pamoja na benchi la ufundi lililoko chini ya kocha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), kimeshawasili jijini humo tangu juzi.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkwasa, alisema kuwa kikosi hicho kimeimarika na kimekwenda Mwanza kwa jukumu moja la kusaka ushindi.

Mkwasa alisema kuwa wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo, ambao anaamini utakuwa na ushindani kutokana na wapinzani wao kupoteza mchezo uliopita kwa idadi kubwa ya mabao.

Alisema pia anatarajia kuona wapinzani wao wakibadilisha aina ya mchezo waliouzoea kwa sababu ya kuhitaji kupata matokeo mazuri, jambo ambalo tayari amewaandaa wachezaji wake kukutana na hali hiyo.

"Tumekuja Mwanza kupambana, hakuna kingine, Alliance si wabaya, wamekuwa na mwenendo mzuri katika baadhi ya mechi zao, hatutawadharau kwa sababu wamefungwa mabao matano, huu ni mpira na kila siku timu huingia uwanjani ikiwa na mipango tofauti," Mkwasa alisema.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kuwa wachezaji wao wote waliokwenda Mwanza wako salama na jana jioni walitarajiwa kufanya mazoezi yake kwenye Uwanja wa Butimba.

"Timu iko katika hali nzuri, muda huu (jana jioni), wachezaji wako kwenye mazoezi Butimba, kesho (leo), ndio wataenda Kirumba kumalizika mazoezi ya mwisho ya mechi yetu dhidi ya Alliance," Bumbuli alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Alliance, Kessy Mziray, aliliambia gazeti hili kuwa mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa upande wowote kutokana na maandalizi ambayo wameyafanya kuelekea mchezo huo.

Mziray alisema kuwa ameshakaa na wachezaji wake na kuwataka wasahau matokeo ya mchezo uliopita, na kuweka mawazo na akili kwa mechi dhidi ya Yanga ambayo iko mbele yao.

"Tunajuana, tumejiandaa kucheza na Yanga kwa umakini, wasitarajie mteremko, wajipange kwa sababu tunaamini uwezo wa kuwafunga tunao," alisema kocha huyo ambaye kabla ya kufungwa na Azam FC, aliwachapa KMC FC ya Dar es Salaam mabao 2-0.

# Kitambi ataka mabao Simba

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, ameanza kutumikia adhabu yake ya kusimamishwa baada ya jana kushindwa kukiongoza kikosi cha mabingwa hao watetezi kwenye mazoezi yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Aussems anatarajia kuweka "kitimoto" na Kamati ya Maadili, katika kikao kinachotarajiwa kufanyika leo jijini hapa, kosa lake kubwa lilikuwa ni kuondoka nchini na kwenda kufanya mazungumzo na klabu nyingine kinyume na mkataba wake.

Katika siku ya kwanza, Kocha Msaidizi, Dennis Kitambi, ambaye amelazimika kuongoza mazoezi ya timu hiyo baada ya kutakiwa kufanya hivyo na mabosi wake, alionekana kuwapa mazoezi ya kumiliki mpira na kufunga mabao.

Kitambi alisema kuwa ametakiwa kusimamia programu za timu hiyo kwa muda wa wiki moja mpaka pale Aussems atakapomalizana na uongozi wa klabu hiyo ambao umepanga kukutana naye.

"Kitu ambacho nimeongea na Mkurugenzi Mtendaji, aliniambia anataka kuniambia ana kwa ana, nikujulishe kuwa Kocha Mkuu tumemsimamisha mpaka pale tutakapokuwa na kikao tarehe 28, kwa sasa wewe itabidi usimamie timu kwa wiki nzima," alisema Kitambi, ambaye ameshawahi pia kuzifundisha Azam FC na Ndanda FC za hapa nchini.

Hata hivyo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Masingiza, jana alivamia mazoezi ya vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini hakuwa tayari kutoa maelezo yoyote kuhusiana na kutoonekana kwa Aussems kwenye mazoezi hayo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >